ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais.
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu.
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa.
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa.
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa.

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa.
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi.
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole.
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais.
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi.
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae.
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

BARAZA LA NANE LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 3 April, 2013

Kikao Kilianza Saa 3.00 Asubuhi

DUA

Mhe. Spika (*Pandu Ameir Kificho)* alisoma dua

WIMBO WA TAIFA

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani nakala zote za gazeti rasmi la serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 25 January mwaka 2013. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa idhini yako nawasilisha mezani Mswada wa sheria ya kuanzisha kwa Mamlaka ya Udhibiti, huduma ya maji na nishati na mambo yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani juu ya hotuba ya maoni ya kamati ya Mawasiliano na ujenzi kuhusu, Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Maji na Nishati na Mambo Yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 14

Malipo Kwa Waathirika wa Ajali ya SPICE ISLANDER

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:
Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu Nam. 14 napenda kutoa pole kwa familia ya Marehemu Mhe. Salum aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Chambani, Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema Peponi.
Kwa kuwa katika Kikao cha mwezi wa Oktoba 2012 Mhe. Waziri alisema kuwa wale wote ambao wangestahiki kulipwa kifuta machozi katika ajali ya

MV SPICE ISLANDER tayari wamelipwa, na kama kuna yoyote ambae hajalipwa na anaushahidi kuwa ameathirika, basi apeleke jina lake katika Afisi ya Maafa, Serikali itachunguza na kuwalipa mafao hayo. Na kwa kuwa kuna watu ambao watu wao wamefariki na wengine wameathirika kwa njia moja au nyengine katika ajali hiyo na ushahidi upo na hadi leo hii bado hawajalipwa kifuta machozi hicho.

(a) Je, Serikali kwa kufanya hivyo si kuzihangaisha familia za wahanga hao.

(b) Kuzilipa baadhi ya familia na kuziacha familia nyengine zilizoathirika katika ajali ya aina moja si kufanya ubaguzi kwa raia wa nchi moja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, kabla ya kumjibu naomba Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 14 lenye vifungu (a) na (b) kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, ninakiri kwamba katika kikao cha mwezi Oktoba, 2012 niliwaomba Waheshimiwa Wawakilishi waniletee orodha ya wananchi wao ambao wanalalamika kuwa hawajalipwa malipo yaliyotokana na michango ya watu na taasisi mbali mbali kufuatia ajali ya kuzama kwa meli ya MV. Spice Islander 1, hata hivyo ni Wawakilishi wawili tu ndio walioniletea malalamiko yao ambayo yamefanyiwa kazi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 14 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, sio nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuzihangaisha familia zilizoathirika na ajali hiyo, bali utaratibu ni muhimu kufuatwa ili kupata ithibati wa wahusika.
Mhe. Spika, naomba nithibitishe kwamba watu wote waliostahiki kufanyiwa malipo na ambao majina yao yalikuwemo katika orodha ya Tume au Wilaya kama ilivyoagizwa na Serikali kwa waathirika wote kutakiwa kujiorodhesha katika Wilaya zao, watu hao wote wameshafanyiwa malipo yao. Waliokuwa hawakufanyiwa malipo ni wale tu ambao majina yao hayakuwemo katika orodha ya Tume au hawakujiandikisha katika orodha ya Wilaya kama ilivyotakiwa na serikali.

(b) Mhe. Spika, Serikali yetu haiwezi kuwabagua raia wake na wala haitovumilia kufanyika kwa jambo lolote la kibaguzi hapa nchini, na nia ya Serikali ni kuona haki inatendeka na kila muhusika anapata haki yake.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa miongoni mwa Wawakilishi wawili waliopeleka majina ya waathirika wa matokeo hayo na mimi nilikuwemo. Na kwa kuwa jina la marehemu Dokta Raya Nassor Suleman mkaazi wa Vitongoji Umangani, lilikuwemo katika orodha ya mwanzo na ndio maana alipokwenda Makamo wa Rais akapata pesa za mwanzo ile na viongozi wengine walipokwenda Makamo wa Kwanza na viongozi wengine wakapewa familia yao, lakini hadi leo hii familia ile haijapata malipo ya mwisho waliyopewa waathirika hawa.

Je, kwa kufanya hivyo Mhe. Spika, tuseme ni dharau au ni uzembe tu serikali yetu katika kusimamia mambo yake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nikiri kwamba Mhe. Saleh na Mhe. Hamad Masoud ndio Wawakilishi ambao wameleta majina kwetu na yamefanyiwa kazi.

Mhe. Spika, kwa upande wa Mhe. Saleh ni kweli ameleta jina la ndugu Raya Nassor Suleiman Vitongoji na kwa mujibu wa taarifa nilizonazo kwamba mtu huyu amelipwa haki zake kwa mujibu wa utaratibu uliokuwepo. Kama kuna tatizo lolote naomba baada ya kikao hichi baada ya maswali na majibu tukae na Mhe. Saleh anieleze kwa kina ni kwanini malipo haya aseme hayajafanyika, wakati taarifa ambazo nimepata kutoka Idara ya Maafa zinaonesha kwamba ameshafanyiwa malipo yake.

Waathirika wengine ambao Mhe. Hamad Masoud alileta kwetu na wao wamefanyiwa malipo yao walikuwa ni waathirika 21 kwa upande wa jimbo la Ole. Katika hao 17 majina yao yalikuwemo, wamepata malipo yao, isipokuwa ndugu yetu Jokha Khamis Juma ambaye fedha zake zipo lakini mpaka sasa hajenda kuzichukua. Na kwa upande wa Micheweni vile vile Mhe. Hamad Masoud alileta malalamiko naye ndugu yetu Said Omar Kombo naye jina lake halimo katika orodha.

Mhe. Omar Ali Shehe: Nashukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ili nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, tunavyofahamu kwamba meli ya MV. Spice Islander ilikuwa ina Bima na kwa taarifa tulizonazo kwamba meli hiyo ililipwa Bima yake. Lakini vile vile tunafahamu licha ya Bima iliyolipwa meli ile fedha za bima vile vile kulikuwa kuna michango mbali mbali ilitolewa na watu mbali mbali kwa ajili ya wahanga.

Mhe. Spika, tunafahamu kwamba licha ya kupoteza maisha ya kupata majeruhi, wahanga wale walipoteza mali zao nyingi sana katika ajali ile.

(a) Je, fedha zilizolipwa kwa wahanga fedha hizo ambazo zinatajwa zimelipwa kwa wahanga zinatokana na fungu gani, zinatokana na fungu lile la Bima au zinatokana na zile zilizochangwa kwa ajili ya wahanga.

(b) Kwa vile wahanga wale walipoteza mali nyingi ni nini hatima ya fidia kwa mali ile iliyopotea kwa wahanga.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika,

(a) Mhe. Spika, fedha zile ambazo zimetolewa kama kifuta machozi kwa waathirika wa ajali ni fedha ambazo zimechangwa na wananchi na taasisi mbali mbali ikiwemo na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nia ya fedha zile ilikuwa ni kusaidia shughuli za uwokoaji pamoja na shughuli nyengine ambazo zingesaidia katika kuwasaidia waathirika.

Uwamuzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba fedha zote zile zipewe walioathirika na ajali na serikali ya Mapinduzi ingebeba dhima ya kufidia gharama zote za shughuli ya uokoaji. Kutokana na uwamuzi huo fedha zilizochangwa ni kama shilingi bilioni moja na milioni mia mbili na sitini na saba alfu. Katika hizo mpaka sasa fedha bilioni moja, milioni mia moja na kumi na nane zimeshatumika kuwasaidia waathirika wa ajali hiyo.

Fedha zile sio za Bima, bado wananchi walioathirika wanayo haki ya kudai fedha zao kupitia kwa mwenye mali ili kuweza kulipwa Bima zao. Kwa kuwa kwa mujibu wa sheria yetu kama mwenyemali hakutimiza vigezo vinavyotakiwa vya kulipwa Bima ni mwenye mali anayewajibika kulipa bima za gharama zote ya mali hiyo.

Kuhusu mizigo vile vile hii inatokana na malipo ya bima. Kwa hiyo kama meli ile imetimiza vigezo vya masharti ya kukata bima, inabidi basi bima ilipe. Lakini kama hao wenye meli hawakutimiza vigezo hivyo maana yake bado mwenye mali anawajibika kulipa bima ya gharama za mizigo.

Nam. 18

Uhaba wa Vyombo Vya Kutilia Taka

Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Aliuliza:

Majengo ya Michenzani kutokana na ukubwa wake na kuwa na idadi kubwa ya watu kunapelekea kuwepo kwa taka nyingi zenye mchanganyiko wa chakula na takataka nyenginezo na zote huteremshwa chini kwa ajili ya kutupwa. Kwa kuwa uwezo wa chombo cha kutilia taka ni mdogo, taka hizo hulazimika kutupwa chini na kusambaa kwa upepo lakini pia baadhi ya siku taka hizo hukaa zaidi ya siku tano na kusababisha harufu mbaya na nzi.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kwamba vyombo vya kutilia taka ni kidogo na kusababisha taka kusambaa katika maeneo mbali mbali.

(b) Kwa nini taka zinachelewa kuondoshwa ambapo ni hatari kwa afya za jamii.

(b) Je, Michenzani kuna upungufu wa wafanyakazi wa kuhudumia usafi wa maeneo haya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 18 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba vyombo vya kutilia taka (vikapu) vimezidiwa kimatumizi na kuonekana ni vidogo na vyengine vimechakaa. Serikali kupitia Baraza la Manispaa imeliona tatizo hilo na ina mpango kuweka vikapu vipya vya kuwekea taka katika maeneo yote. Pale ambapo pataonekana kuwa na taka nyingi patawekwa vikapu viwili badala ya kimoja.

(b) Taka huchelewa kuchukulia pale inapotokea kuharibika kwa magari yetu ya kubebea taka. Hata hivyo juhudi za makusudi huchukuliwa kuhakikisha taka hizo hazikai zaidi ya siku moja. Tatizo hili tunatarajia litaondoka mara tu magari mapya matano yatakapowasili hivi karibuni.

(c) Tatizo la kuzagaa taka katika eneo la Michenzani halitokani na upungufu wa wafanyakazi bali kinacho jitokeza katika maeneo ya

Michenzani ni maeneo mengine ya Manispaa ya Mji, wananchi huwa wanatupa taka chini wakati kikapu kilichopo huwa mara nyingi ni kimoja huwa kimekwenda kutupwa Baraza litajitahidi kurudisha utaratibu wa zamani kama nilivyoeleza kuweka vikatu viwili au kuweka kikapu kitupu pale kinapoondolewa kikapu chenye taka kwenda kutupwa taka. Lakini pia naomba na wananchi nao wajitahidi sana kufuata utaratibu au utamaduni wa kutupa taka ndani ya vikapu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata nafasi yakuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, katika majibu yake Mhe. Waziri amekiri kuwa vyombo vinavyohusikana na kuzoa taka kwa jumla ni vipungufu na vyengine vimeshachakaa na kuna mpango wa kuagizishia vyengine pamoja na magari. Mhe. Spika, kwa kuwa suala hili ni la muda mrefu na hasa block Nam. 5 la michenzani kule nyuma kumewekwa jaa hasa la kudumu na wakati hali ni kama hii.

Je, Mhe. Waziri, haoni kuwa wakati huu wa mvua na ikiwa bado ana mipango tu iliyokuwa haijakamilika ni kuhatarisha maisha ya wananchi kwa sababu ya taka zile.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, si nia ya Baraza la Manispaa wala Serikali kuhatarisha afya au maisha ya watu. Kama nilivyosema matatizo tumeyagundua, *volume* ya taka sivyo tulivyoizowea zamani ambapo kulikuwa na magari ya kubururwa kwa mikono ya watu watatu. Sasa hivi *volume* imekuwa kubwa baada ya kuona hivyo serikali kwa kushirikiana au wenyewe tukaomba mkopo Benki ya Dunia na wakatuitikia. Kwa hiyo katika huo mkopo pia kuna suala la kuagiza magari mapya, tunatarajia tutapata magari saba kwa Mkoa wa Mjini Magharib pamoja na vikapu vya kuzolea taka vipatavyo 153.

Imani yetu kwamba tukipata vifaa hivyo tatizo hili tutaliondoa katiba, kwa sababu tatizo ni uondoaji wa taka. Ahsnte Mheshimiwa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri, pamoja na kukubali Mhe. Waziri na kukiri kwa kusema kwamba magari yake ni mabovu.

Mhe. Waziri huko nyuma mlikuwa mna mpango wa kuazima magari mengine ya serikali ili kunusuru magari kama haya na hasa wakati wa mvua. Je, una mpango gani wa kurejesha mpango huo wa kuweza kuazima magari ya serikali wakati wa mvua ili kuokoa maradhi ya mripuko.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakubaliana na yeyé kwamba huko nyuma tulikuwa tunafanya utaratibu huu na bado tunaendelea nao mpaka hivi leo. Juzi tu tulitumia kijiko chetu, tukaazima magari na tumejitahidi kwa kiasi kikubwa kuziondoa zile taka zilizorundikana katika maeneo ya Michenzani na kwengineko. Ahsante.

Nam. 1

Makabidhiano ya Vifaa vya Michezo

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Agosti mwaka 2012 Kampuni ya Vinywaji baridi imekabidhi vifaa vya michezo kwa Timu 12 zinazoshiriki Ligi Kuu ya Zanzibar bila ya kuwepo viatu wakati vilabu vingi vinakabiliwa na kilio kikubwa cha kushindwa kumudu gharama za viatu.

(a) Kwanini ZFA na Kampuni hiyo wameshindwa kuzingatia hilo kwenye Mkataba wa Udhamini wa Ligi hiyo.

(b) Vilabu vinavyoshiriki ligi hiyo vilishirikishwa vipi katika kutayarisha Mkataba wa Udhamini huo na kusababisha timu kupokea vifaa pungufu.

(c) Kwa kuwa suala la viatu ni muhimu ZFA na Serikali ina mpango gani wa kuangalia upya Mkataba huo ili kutatua suala hilo.

Mhe Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suala lake namba 1 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-
Mhe. Spika, ZFA na Kampuni inayotengeneza kinywaji cha *Grand Malta* hawakushindwa kuzingatia suala la upatikanaji wa viatu kwa Klabu zinazoshiriki Ligi Kuu ya Zanzíbar.

Mhe. Spika, kilichofanyika ni kuzingatia vipaumbele miongoni mwa mahitaji mengi ambayo vilabu walivyokuwa navyo. Hata hivyo kwa sababu udhamini huu ni wa miaka mitatu, suala la upatikanaji wa viatu kwa klabu linazingatiwa na kupewa kipaumbele na litashughulikiwa katika mwaka huu wa Pili wa udhamini. Tokea mwanzoni ZFA iliwapa taarifa viongozi wa vilabu vyake vinavyoshiriki ligi iliyodhaminiwa na iliwajulisha maendeleo ya mazungumzo, hatua iliyofikiwa na matumizi ya udhamini wenyewe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri vilabu vingi vilifanikiwa au vilifarijika kupata udhamini huo. Lakini chama dhamana hivi sasa ZFA, rais wake amejiuzulu. Je, kuna mpango gani au serikali itachukua hatua gani kutokana na raisi huyo wa ZFA kujiuzulu.

Mhe Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru, nikweli Rais wa ZFA amejiuzulu, lakini aliyejiuzulu ni ndugu Amani Makungu. Taasisi ya ZFA kwa mujibu wa Katiba yake ipo na utaratibu kwamba Rais akijiuzulu au akifariki ni namna gani nafasi hiyo itajazwa kwa muda hadi hapo uchaguzi mwengine utakapofanyika.

Ninachomuhakikishia ni kwamba shughuli za ZFA zinaendelea kama kawaida hata kwamba Rais amejiuzulu lakini utaratibu wa Kikatiba unaendelea na shughuli zinaendelea.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, mbali na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kuhusiana na suala zima la Rais wa ZFA. Chama cha Mpira wa Miguu ZFA kuna ofisi zake ndani ya jengo la Rais wa ZFA na mkataba wake wa jengo lile tarifa tulizonazo unamalizika mwezi ujao. Je. Waziri ataliambia nini Baraza hili na wapenzi wa mpira wa miguu Zanzibar, ZFA, itahamia wapi katika Afisi zake mpya baada ya kumaliza mkataba huo.

Mhe Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nakushukuru Mhe. Spika, ni kweli kwamba ZFA ilikodi jengo na linamaliza mwezi ujao. Sasa kama nilivyosema awali kwamba uongozi wa ZFA upo na ni jukumu lao kuona kwamba kama wana uwezo wa kifedha basi wataendeleza na mkataba hadi hapo ambapo uwezo wao utakapomaliza.

Sisi kama Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, tuliwapa ZFA afisi katika jengo la Bwawani, Afisi ile bado ipo, wakiamua kuitumia bado wataendelea kuitumia. Lakini pia tuliwapa vyumba katika uwanja wa amani juu ya matumizi yao, wakiona kama hawawezi tena kukodi jengo la binafsi

basi bado wizara ni mlezi wao, wakati wowote wapo tayari kuhakikisha kwamba ZFA wanakuwa na eneo la kufanyia shughuli zao.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Waziri hivi karibuni umefanya ziara ya kuonana na wadau wa mpira wa miguu wa Unguja na Pemba na ulikuwa ukitumia vyombo vya habari kutoa taarifa muhimu kwa ajili wa wadau wa mpira wa miguu. Wadau wote wa Unguja na Pemba wameonesha dhahiri kwamba ZFA imeshindwa kusimamia ipasavyo malengo ya serikali ya kunyanyua soka la miguu hapa Zanzibar na hivyo kutishia wafadhili wa soka hilo kuondoka.

Je, huoni kwamba sasa umefika wakati ZFA, kuivunja na suala la mpira kupelekwa Wizara ya Elimu.

Mhe Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru na kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Hija Hassan Hija, mwakilishi wa jimbo la Kiwani swali lake lanyongeza kama ifuatavyo:

Ni kweli kwamba mwezi uliopita nilifanya vikao vingi na wadau wa mpira wa miguu Unguja na Pemba, katika vikao viwili tofauti na katika vikao hivyo nilipata maoni ya wadau kwamba ZFA imeshindwa kutekeleza majukumu yake na wakanishauri kwamba niivunje. Mhe. Spika, maoni hayo nimeyapokea na nimeyazingatia bado na ninafurahi leo pia nimepata maoni mengine ya mdau wa mpira wa miguu Mhe. Hija kwamba nae anaungana na wadau hao wa mpira wa miguu kwamba ZFA niivunje. Basi ninamshukuru kwa mchango wake huo na kama ambavyo wengine wamenipa basi Wizara inazingatia maoni hayo tutayafanyia kazi.

Nam. 104

Uajiri wa Wafanyakazi Wapya

Mhe. Shadya Moh'd Suleiman - Aliuliza:

Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha asubuhi kufika hapa nikiwa katika hali ya uzima. Baada ya hapo nichukue fursa tena kuwapa pole wananchi wa Jimbo la Chambani kwa kuondokewa na Mbunge wao.

Kumejitokeza tatizo la upungufu wa wafanyakazi katika *section* tofauti katika Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hii ni kusababisha uzorotaji wa kazi na kutofanya kazi kwa wakati. Hii inatokana na kutoajiriwa wafanyakazi

katika sehemu husika, wakati wafanyakazi wengi wao wameshastaafu na wengine wameenda likizo bila ya malipo.

Mhe. Waziri naomba utueleze ni sababu zipi za msingi zinazopelekea kutoajiriwa
wafanyakazi hao wakati mishahara ya wafanyakazi hao walioondoka ipo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake 104 lakini kabla ya kujibu naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, Watumishi wa Umma huwa wanatoka katika Utumishi kutokana na kufikia umri wa kustaafu, kuacha kazi, kufariki dunia, kushindwa kufanya kazi kutokana na sababu za kiafya na uhamisho wa kudumu katika Utumishi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa watumishi wanaochukua likizo bila ya malipo wanahesabiwa bado ni watumishi hadi itakapotokea moja kati ya sababu nilizozitaja hapo awali.

Mhe. Spika inapotokea nafasi kuwa wazi, nafasi hiyo hujazwa na kufuata taratibu za ajira zilizowekwa na Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 na pia kwa kuangalia muundo na majukumu ya wakati husika ya taasisi ambayo mfanyakazi ametoka. Aidha, kifungu cha 56 cha Sheria ya Utumishi wa Umma kinataka kuwa na mpango wa rasilimali watu ufuatwe, hivyo ajira zinategemea zaidi mpangilio huo kuliko kujaza nafasi ya mtu aliyeondoka.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

Uajiri wa watumishi unaendelea kwa kufuata mpango wa rasilimali watu katika Mawizara na Taasisi zake kwa kuzingatia Ikama (*Norminal Roll*) zilizokubaliwa na kuidhinishwa. Aidha, naomba nimjulishe Mhe. Mwakilishi kuwa fedha za mishahara ni fedha za Umma na matumizi yake yanahitaji kufuata mpango uliowekwa na mahitaji halisi ya wakati husika katika Utumishi wa Umma. Ujazaji wa nafasi tupu unaendelea kwa kufuata matakwa ya kifungu cha 57 cha Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 na haujasitishwa.

Mhe. Shadya Moh'd Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri je Wizara yako inachukua hatua gani kukabiliana na tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kama nilivyosema kwenye jibu mama kwamba ujazaji wa nafasi haujasitishwa pale ambapo Wizara husika inaleta maombi kwenye Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma na kuwa inataka kujaza nafasi kutokana na umuhimu wa hiyo nafasi ambayo inataka kujazwa, basi serikali inachukua hatua au Wizara yangu huwa inachukua hatua ya kuwapa kibali cha kuweza kujaza hizo nafasi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ninakushukuru Mhe. Spika, na mimi naomba vile vile kabla ya kuuliza swali niungane na wenzangu kuwapa pole wananchi wa Jimbo la Chambani na familia ya marehemu Salim Hemed Khamis kutokana na kifo cha Mbunge huyo wa Chambani, ninamuomba Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi, awape subra wafiwa.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri. Mhe. Spika, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia kwa kushirikiana na UNDP ikishirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 2003 katika *study* iliyokuwa inaitwa *Public Expenditure Review* ilionesha kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni miongoni mwa serikali ambayo ukilinganisha na idadi ya watu ina watumishi wengi wa umma. Na katika rekodi za hivi sasa za serikali inaonekana kuwa tunakaribia au tumepita watumishi wa umma 39,000 katika nchi ambayo ina watu milioni moja na laki tatu. Hiyo Mhe. Spika, inatoa wastani wa wafanyakazi 39 wanaohudumia watu 130 katika nchi hii.

Swali langu kwa Mhe. Waziri, badala ya kwamba ina upungufu wa watumishi wa umma ina wafanyakazi wengi zaidi ambao kama ripoti hii ilivyoonesha inaitia hasara serikali kwa kutumia sehemu ya bajeti yake katika kulipa mishahara ya watu ambao wamekuja kuthibitishwa baadae na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi 2007 Mhe. Muombwa kwamba asilimia 18 tu ndio wenye sifa za kutumikia nafasi zao na wengi hawana sifa. Kwa hivyo tatizo sio upungufu wa wafanyakazi bali ni kuajiriwa watu ambao hawana sifa kutumikia nafasi za utumishi wa umma.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa kwamba upo utafiti ambao ulifanywa na Benki ya Dunia. Na *result* za utafiti huo ulisema moja kati ya mambo ambayo waliyasema ni hayo kwamba ukilinganisha na idadi ya watu wa Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilionekana kwamba ina watumishi wengi zaidi. Lakini ningependa nimhakikishie Mheshimiwa Jussa pamoja na Baraza lako Tukufu kwamba idadi ya watumishi wa umma hawategemei na idadi ya watu, inategemea majukumu yaliyopo katika wakati ule katika kufanya wajibu wao au katika kutekeleza majukumu yangu.

Wizara yangu kwa sababu huu utafiti upo hatukuupuuza, hivi sasa Wizara yangu inafanya mapitio ya majukumu ya kazi kwa watumishi wa umma ili kubaini kwamba hilo ambalo wametuonesha wataalamu lipo, na kama lipo; lipo kwa kiasi gani ili serikali iweze kuchukua hatua gani.

Nam. 23

Utanuzi wa Chelezo Bandari ya Malindi

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:

Natoa pongezi za dhati kwa Shirika la Bandari kuwa na chelezo ambacho kinatumika katika utengenezaji wa boti zetu kwa matengenezo yanayowezekana hapa chelezoni.

(a) Serikali inaipa umuhimu gani ile fursa ya kukirefusha chelezo hicho mpaka kufikia kina kikubwa cha maji ili vyombo vikubwa viweze kuhudumikiwa ipasavyo na hasa kutokana na kuwa Serikali ina mpango wa kuikuza Bandari ya Malindi na kuweza kutoa huduma ipasavyo.

(b) Kutokana na umuhimu wa Chelezo hicho, Serikali imechukua hatua gani katika kuwapatia Wataalamu wake mafunzo zaidi ili waweze kumudu vizuri kazi zao za matengenezo ya vyombo Chelezoni.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 23 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Shirika la Bandari ina azma ya kukirefusha Chelezo cha Malindi pale hali ya fedha itakaporuhusu, ili vyombo vyenye kina kikubwa (*Draft*) kuweza kupanda na kuhudumiwa kwa matengenezo mbali mbali pamoja na kukuza mapato ya Shirika kupitia chelezo hicho.

Kwa hivi sasa Shirika limetoa kipaumbele kwa miradi mengine ya Maendeleo ikiwemo ya ununuzi wa zana na kuhudumia Makontena na mizigo Bandarini, matengenezo ya sehemu ya kuwekea Makontena, ujenzi wa Afisi za Shirika, Mradi wa Ufungaji wa Taa za *Solar* katika Minara mikubwa ya Unguja na Pemba na miradi mengine.

(b) Kwa upande wa mafunzo Shirika limeandaa mpango (sera) wa mafunzo kwa wafanyakazi wake wote wakiwemo mafundi wanaofanya kazi katika Chelezo hicho kwa lengo la kuwazidishia ujuzi na kuleta ufanisi katika Shirika. Mpango huo wa mafunzo unatarajiwa kuanza rasmi katika mwaka huu wa 2013.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, chelezo hichi kiliopo kimejengwa muda mrefu uliopita na kimefanya kazi nzuri na ndio kukawa kuna sababu kirefushwe ili huduma za kutengenezea meli zinazokuja pale ziweze kufanyika kwa ufanisi zaidi.

Je ni kwa nini tokea chelezo hiki kuanza na chenye azma hiyo ikawa mpaka leo hakijatengenezwa na ikawa bado serikali ina azma tu.

Pili, kwa sababu kuna mpango na ukifanikiwa utakuwa mzuri wa kuongeza gati hii ya Malindi mpaka Mpiga Duri na vyombo vingi vitakuwa vinatia nanga hapa kwa shughuli kadhaa, haoni Mheshimiwa kuwa kuendelea na mpango huu vyombo vikubwa vinavyofika hapa na badala yake vikenda vikafanyiwa *service* kule Mombasa ni kupoteza pesa nyingi ambazo ziingie hapa kwa makusudi.

La mwisho, hivyo chelezo hichi kilipoanza kujengwa kwa azma hiyo hapakufanywa utafiti mpaka kikachelewa mpaka hivi leo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli kwamba serikali ilijenga chelezo na madhumuni makubwa ya chelezo ni kutoa huduma kwa vyombo vya usafiri wa baharini, na chelezo hicho anachokizungumzia Mhe. Mwakilishi kinatoa huduma, tatizo liliopo ni kwamba kuna matatizo ya kina cha maji. Azma ya serikali ni kuchimbua ili kuongeza kina cha maji tuweze kutoa huduma kwa vyombo vikubwa. Vyombo vikubwa pale vinavyoweza kuhudumiwa hivi sasa inategemea zaidi maji kama vile mfano *MV Sepideh* imefanyiwa marekebisho pale lakini ilizingatia zaidi taidi ya maji, maji yangekuwa hayako juu tungeshidwa kuipa huduma.

Lakini nimuhakikishie kwamba Mhe. Mwakilishi na Baraza lako tukufu kwamba maamuzi ya kujenga chelezo pale hayakuwa maamuzi ya kubeza wala sio kama maamuzi ambayo hayakulenga. Ni maamuzi yaliyolenga eneo zuri na matatizo haya tunayoyazungumza ya kurefusha chelezo ni masuala yanayohitaji uwekezaji wa fedha. Na mimi naamini kwamba malengo ya shirika ni kuona kwamba chelezo kile kinaimarika ili kuweza kutoa huduma kwa vyombo vikubwa kama madhumuni makubwa ya kuanzishwa kwake.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri wakati anajibu swali amesema kwamba wana mipango badala ya kuimarisha chelezo wana mipango ya kuweka sehemu ya makontena na kupanua mambo mengine. Wakati huku wazanzibari zaidi ya asilimia thamanini tunategemea sana usafiri wa baharini.

Je, kutengeneza sehemu ya makontena na kuacha kufanya ukarabati wa meli ambazo asilimia 80 tunazisafiria sisi hapa watu wa chini kwa kufanya hivyo si serikali inafanya mambo bila ya kuwa na kipaumbele.

Pili Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakubaliana nami kwamba serikali wakati inajenga kile chelezo haikufanya utafiti wa kina katika kukijenga.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri hebu jibu hili la utafiti wa chelezo kwa sababu ndio suali mama hili jengine liache.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, napenda kumhakikishia Mhe.Mwakilishi wa Baraza hili Tukufu kwamba ujenzi wa chelezo eneo la Malindi ulizingatia utafiti na hayo tunayoyaeleza kwamba uimarishaji wa huduma katika chelezo hicho kinatokana na huo utafiti ambao ulifanywa awali lakini mabadiliko ya tabia nchi, mabadiliko ya kimaendeleo nayo pia inawezekana ikawa changamoto katika kuona matatizo yanayokikabili chelezo kile.

Kama tunavyojua chelezo kile hivi sasa kimezungukwa na huduma nyengine muhimu pamoja na matumizi ya bandari ile. Aidha Mhe. Spika, suala la kuona kwamba bandari tunaimarisha maeneo ya kuweka makontena na badala yake hatuimarishi chelezo sioni kama tunaitia hasara Serikali. Kwa madhumuni kwamba tutakapoweza kuimarisha huduma ya kuweka makontena tutaongeza mapato kwa serikali.

Na suala la kwenda kufanya matengenezo kwa vyombo ni suala la kibiashara na Serikali sasa hivi vyombo tulivyokuwa navyo vinaweza vikahudumiwa pale na vyengine vinapelekwa katika maeneo makubwa kama vile Mombasa na kwengineko kulingana na matatizo ya chombo husika.

Nam. 32

Ongezeko la Maambukizi Mapya ya VVU/Ukimwi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-
Ugonjwa wa Ukimwi umekuwa ni tishio kubwa na janga la kitaifa na kimataifa hadi sasa ugonjwa huu haujapata kinga wala tiba licha ya wataalamu mbali mbali duniani kufanya tafiti nyingi ambazo bado hazijazaa matunda ya kupambana kikamilifu na ugonjwa huu.

a) Je, Serikali inasema nini juu ya hali hiyo kwa upande wa Zanzibar.
b) Je Serikali kwa kushirikiana na wananchi ina mikakati gani ya kupambana na kuzuia maambukizi mapya ya VVU/Ukimwi.
c) Suala la kuporomoka kwa maadili na athari za maingiliano ya watu zisizodhibitiwa zimekuwa zikichangia sana ongezeko la maambukizi mapya. Serikali inachukua hatua gani za makusudi kupambana na kuporomoka kwa maadili na kuzuia uingiaji holela wa watu usio na udhibiti katika visiwa vyetu, ili kudhibiti maambukizi mapya ya VVU.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 32 lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ukimwi upo na chanjo ya kukinga ukimwi haijapatikana hiyo ni sahihi, kilichobakia sitokijibu kwa sababu ameshakitoa na mimi nakitoa.

Mhe. Spika, ili tuweze kujua tuna kiasi gani cha tatizo la ukimwi tunahitaji kufanya tafiti, sasa utafiti wa viashiria vya ukimwi na VVU Tanzania uliofanyika mwaka 2011/12 ili kukusanya taarifa mpya za kiwango cha maambukizo ya ukimwi kwa ujumla kiwango cha maambukizi VVU Tanzania ni asilimia 5.1.

a) Kwa upande wa Zanzíbar kiwango cha VVU na Ukimwi kipo chini ya asilimia 1 yaani 0.6. Hata hivyo maambukizi yapo katika kiwango cha juu kwa makundi maalum yafuatayo:

Kundi la kwanza wanaume wanaojamiina na wanaume wenzao.

Kundi la Pili la wanawake wanaouza miili yao na

Kundi la tatu watu wanaotumia dawa za kulevya kwa njia za kujidunga sindano.

b) Serikali kupitia Wizara zake za Afya na Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, wadau wa maendeleo na wananchi ina mikakati ifuatayo:

Kuna mpango mkakati wa Pili wa kitaifa wa kupambana na maambukizi ya ukimwi na VVU.

Kuna Kamati za Wilaya, Shehia na Makundi maalum kupitia mfuko wa World Bank na TASAF.

Kunatolewa elimu ya rika ya ukimwi kwa makundi tofauti, vikundi vya dini, afya maskulini, elimu ya afya kwa njia ya mawasiliano, afya makazini na katika Baraza la Wawakilishi na siku ya ukimwi katika vyuo vya mafunzo.

c) Maadili kuporomoka hilo si la serikali, ni sisi wananchi kwa ujumla na kama wazazi tunawajibika kusimamia maadili ya watoto wetu, mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. Hebu na tujiangalie kwenye jamii yetu tunalizingatia hilo.Kwa wakati huu tulionao jambo moja muhimu ni kuwa wawazi na kuwafundisha watoto wetu ni njia ipi kuu ambayo ukimwi unaambukizwa ili kuwaepusha na hatari inayowakabili.

Elimu ya ukimwi kwa watoto ni kinga bora kuliko nyengine zote.

Maingiliano ya watu yasiyodhibitiwa na kuzuia uingiaji holela wa watu katika visiwa vyetu, hilo halina uthibitisho wa kitafiti na maradhi ambayo yametajwa katika sheria za kimataifa katika muingiliano wa watu, kudhibitiwa ukimwi haumo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, alipokuwa akijibu alisema kuna maeneo matatu ya hatari, watu wanatumia dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga sindano. Je serikali imechukua hatua gani kama dawa za kulevya umefika wakati zinasafirishwa Zanzibar kupelekwa nchi za nje na hapa hatuna mashamba ya kuzalisha unga sisi.

Pili, kamati ilipotembelea Bohari kuu ya madawa wamekuwa na kilio cha upungufu wa dawa za ukimwi analiambiaje Baraza.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, sisi Wizara ya Afya kazi yetu kuchunguza wagonjwa, kuchunguza watu wenye matatizo na wasiokuwa na matatizo. Lakini dawa za kulevya yakiingia kwa kiwango kikubwa au vipi ninafikiri hilo liko nje ya jukumu letu. Labda suala hili angelitafuta kwa wale ambao wanaohusika moja kwa moja.

Sisi tunashughulika na wale ambao wanaotuhusu na hao tunawatafuta wakati ule tunapofanya utafiti, wasipokuja katika kituo chetu wao kama wagonjwa sisi huwa hatushughuliki nao.

Lakini suala la Pili linalozungumzia upungufu wa dawa kwa wakati huu Tume ilipopita ililikuta hilo, lakini sisi tunafanya kazi pamoja na Bara kwa hivyo suala la dawa zinaletwa kitaifa, zikipungua nchini zinapungua kote, lakini huwa tunafanya mawasiliano kwa sehemu ambazo wanazo. Kwa hivi sasa dawa za ukimwi zote zinazohitajika zipo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa lengo la *millenium* katika kupambana na suala zima la ukimwi ni kufikia 0.3, 0.3 kwa maana kuondosha maambukizi mapya, kuondosha unyanyapaa pamoja na kutokuwepo kwa wagonjwa wapya wa ukimwi.

Kwa kuwa Mhe. Spika, mavazi ni suala moja ambalo kwa kiasi kikubwa hasa mavazi ya kinamama kwa kiasi kikubwa yanapelekea ushawishi wa kupatikana kwa ukimwi kutokana kwa kuvaa hivi vimini na nguo za kubana mno, je ni lini Mhe. Spika, serikali yetu katika kufikia 0.3 itaandaa sheria itakayopelekea kuweko kwa mavazi rasmi ili kupunguza maambukizi mapya, ili watu wasivutiwe na mavazi hayo wanayovaa kinamama ya kubana sana na hatimae kupata wagonjwa wapya wa ukimwi.

Mhe. Spika: Hili suala nadhani si la Wizara ya Afya kwa hivyo yeye ninamsamehe asilijibu, kwa hivyo kama hakuna wa kujibu Mheshimiwa tunakushukuru tunaendelea.

Nam. 6

Biashara ya Magendo ya Nishati ya Mafuta

Mhe. Nassor Salim Ali - Aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na tabia ya baadhi ya wafanyabiashara wa Nishati ya Mafuta ya Petroli kusingizia upungufu wa Nishati hiyo ya Petroli wakati

Petroli hiyo wakiwa nayo ya kutosha katika vituo vya *Petrol Station* zao na kuanza kuuza Petroli kwa magendo.

(a) Je, Wizara inayo taarifa hiyo.

(b) Na kama inayo ni hatua gani zilizochukuliwa kwa wale wanaofanya vitendo hivyo vya magendo ya Nishati ya mafuta ya Petroli.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:

Mheshimiwa Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 6 lenye vifungu a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, taarifa za upungufu wa nishati ya mafuta ya petroli kwenye vituo vya kuuzia mafuta kwa baadhi ya wakati na kwa baadhi ya wafanyabiashara wa nishati hiyo zinajulikana.

(b) Kiini cha matatizo hayo imeelezwa kuwa ni kuchelewa kuingizwa kwa mafuta ya petroli na makampuni yanayojihusisha na biashara hiyo hapa nchini.

Mhe. Spika, wizara yangu haijapata uthibitisho kuwa upungufu huo ni njama za wafanyabiashara kuuza mafuta yao kimagendo. Kwa ujumla wizara yangu hivi sasa iko kwenye mchakato wa kuanzisha taasisi inayojitegemea ya kusimamia biashara ya mafuta, umeme na maji (*ZURA*) kwa nia ya kufuatilia kwa karibu huduma hizo ili kuondoa ubadhirifu wa aina hiyo ikiwemo uchakachuaji wa mafuta ya petroli.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, mbali na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri katika jibu lake la msingi amekiri kwamba liko tatizo hilo. Lakini mbali na tatizo hili la kuuza petroli kwa njia ya magendo baada ya upungufu wa petroli, lakini kumekuwa na tabia ya wafanyabiashara au wafanyakazi katika vituo vya mafuta kuingiza mtambo ule wa kuingiza mafuta katika gari na kuingiziwa upepo.

Je, kadhia hii anaijua na kama anaijua ana mipango au mikakati gani kuhakikisha kwamba kadhia ile inaondoka.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwenye jibu langu mama na ndio dawa sahihi nimesema kwamba tunaanzisha taasisi ya kuratibu na kudhibiti uuzaji wa mafuta, maji na mambo mengineyo yanayohusiana na hilo.

Sheria hii Mhe. Spika, itaipa nguvu hii taasisi tunayoianzisha kushughulikia suala hilo alilolitaja, kwanza kuhakikisha kwamba *pump* zote ziko kwenye kiwango kizuri cha kufanya kazi, kuhakikisha kwamba mafuta yako katika *standard* ambayo ni nzuri inayoweza kutumika kwa ajili ya magari pamoja na kuthibitisha kwamba mafuta yanaletwa kwa wakati na yanauzwa yote na pia kushughulikia masuala ya bei. Mhe. Spika ndio maana chombo hiki ambacho leo sheria yake tutaisoma katika Baraza hili na Wajumbe watapata nafasi kuchangia.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kuingia hapa katika hali ya uzima na afya.

Mhe. Spika, kwa kuwa bajeti iliyopita nilizungumzia suala la mafuta na nikamtaka Waziri wa Fedha kwamba suala hili alizingatie vizuri, na kwa kuwa ndilo linaloleta matatizo hapa Zanzibar. Je, Mhe. Waziri analijua suala hili kwamba nilimtupia Waziri wa Fedha wakati wa bajeti?

Pili, na kwa kuwa mafuta haya yanayoletwa ndio yanayosababisha upandaji wa bei kiholela. Je, Mhe. Waziri ataliambia vipi Baraza hili tukufu ili wananchi na wao wasikie huko kutokana na suala la kupandishwa bei mafuta. Na kwa kuwa unapokwenda katika vituo…

Mhe. Spika: Mheshimiwa huishii hapo? Nadhani ishia hapo na nimruhusu Mhe. Naibu Waziri ajibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, najua na kwa sababu serikali tunafanya kazi pamoja ndio maana serikalini tukazungumza kwamba tutayarishe sheria hii ambayo tunaileta leo kushughulikia hayo matatizo ya mafuta na mambo mengineyo ambapo na maji pia tumeyaingiza katika masuala hayo hayo.

Sasa hilo suala la kupandishwa bei kiholela itakuwa sasa halipo tena kwa sababu hiki chombo tutakachokianzisha ndicho kitakuwa kina-*control* bei na kinaamua bei gani mafuta yauzwe na kitakuwa na nguvu ya kisheria kabisa ya kumshughulikia yeyote atakaeuza mafuta kwa bei anayotaka yeyé mwenyewe bila ya kufuata utaratibu uliomo humu.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja fupi la nyongeza. Pamoja na kuelekea kuanzisha Taasisi ya *ZURA* serikali inashindwa nini kutoa tarifa kwa umma endapo hutokea upungufu wa nishati ya mafuta badala ya kuwaacha wananchi kudhani kuwa wanafanyiwa usanii.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, serikali haishindwi kutoa taarifa, serikali inashughulikia kwa mujibu ya utaratibu matatizo yanayotokea kwenye mafuta. Kwa hivyo, bado namuomba Mheshimiwa aone kwamba tutapounda chombo cha kushughulikia masuala haya basi matatizo haya tutajua tunayapeleka wapi, sheria inatueleza nini na mambo haya ya kutangaza na kila kitu kwa sababu hiki chombo maalum kitashughulikia masuala ya mafuta.

Nam.29

Matokeo ya Mtihani wa Taifa Kidato cha Nne Mwaka 2011

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:-

Jumla ya wanafunzi 197 kutoka Skuli nne zilizopo katika Jimbo la Mtambwe walifanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne, *Form IV* mwaka 2011 na matokeo yakawa kama yafuatavyo:-

(i)	DIVISION I	0/197	=	0%
(ii)	DIVISION II	0/197	=	0%
(iii)	DIVISION III	0/197	=	0%
(iv)	DIVISION IV	109/197	=	55.33%
(v)	DIVISION 0	88/197	=	44.67%
	WASTANI WA GPA		=	4.767

(a) Kwa matokeo haya, wizara imejifunza nini.

(b) Wizara imeweka mikakati gani katika kuondoa tatizo hili.

(c) Kwa upande wa Skuli kumi za Wilaya ambazo zinatarajiwa kuwa za kisasa, wizara imejipanga vipi katika kuhakikisha kuwa zinatoa matokeo mazuri katika Mitihani ya Taifa ya Kidato cha nne.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 29 lenye sehemu (a), (b) na (c), lakini kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba jumla ya wanafunzi 197 wa Skuli za Sekondari nne katika Jimbo la Mtambwe walifanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne kwa mwaka 2011. Skuli hizo ni Skuli za Uondwe, Makongeni, Piki na Skuli za Mzambarauni. Pia ni kweli kwamba kati ya wanafunzi hao waliotahiniwa hajakuwepo hata mmoja aliyepata daraja la kwanza, la pili au la tatu.

Wanafunzi 109 sawa na asilimia 55.33 ya watahiniwa wote walifaulu na kutunukiwa cheti cha daraja la nne na wanafunzi waliobakia walipata daraja la *zero*. Ni kweli matokeo hayo si mazuri, sio kwa skuli za Jimbo la Mtambwe peke yake lakini kwa taifa zima.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

a) Wizara iliyatafakari matokeo hayo na kuona kwamba yalisababishwa na kuwepo walimu wachache wasiokuwa na uwezo, kuwepo juhudi ndogo za mashirikiano kati ya walimu, wazazi na wanafunzi, kutokuwepo vifaa vya maabara vya kutosha na kadhalika. Pia wizara ilibaini kuwa mazingira ya baadhi ya skuli zetu hasa za vijijini hayakuwa mazuri kumfanya mwanafunzi asome na apasi vizuri.

b) Katika kukabiliana na changamoto hizo, wizara imeangiza kuchukua juhudi zifuatazo: kwa mfano, wizara sasa imenunua vifaa vingi vya maabara, imenunua vitabu vingi vya sekondari kwa kila mwanafunzi

   Wizara yangu imechukua hatua hivi sasa kuajiri walimu wazuri wa sayansi na hivi karibuni itaajiri walimu wapatao 400 wa sayansi kwa skuli mbali mbali za vijijini.

c) Kwa upande wa Skuli mpya za Sekondari za Wilaya, ambazo skuli nane zimefunguliwa hivi karibuni skuli hizo zimeshapatiwa vifaa vya sayansi vya kufundishia vya kutosha. Skuli hizo zina walimu wa sekondari wazuri wa kutosha wenye *degree, diploma au degree* ya pili wenye uwezo wa kusomesha.

Hata hivyo, kutokana na kupanda gharama za ujenzi, ujenzi wa dakhalia ambao ulipangwa kujengwa kutoka kila skuli zilizofunguliwa hivi karibuni haukuwezekana, lakini mazungumzo ya awamu ya ya pili ya ujenzi huo yameshafanywa na taasisi ya benki ya Dunia na hivi karibuni tutakapopata kibali cha kuzitumia fedha hizo tutajenga dakhalia kwa kila skuli hizi tulizozifungua ili wanafunzi katika wilaya wapate kujiunga na skuli hizi kwa kuwa watapata kulala katika hizo dakhalia.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwanza natoa shukurani za aina yake kwa Mhe. Waziri kwa jibu lake zuri alilolitoa kwa kujibu swali hili. Mhe. Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na kwamba Mhe. Waziri ameeleza kuwa tayari amejitayarisha vya kutosha kwa kupata walimu wazuri, kununua vitabu, vifaa vya maabara na kadhalika lakini mtihani huu

wa Kidato cha Nne wa mwaka huu 2012 matokeo yake yamekuwa mabaya zaidi kuliko ule wa mwaka 2011.

(a) Kwa nini iwe hivyo wakati Mhe. Waziri kajitahidi kutafuta vifaa husika ili kuondoa tatizo hili.

(b) Kutokana na kuwa baadhi ya walimu hawana uwezo wa kusomesha masomo wanayopewa kama Mhe. Waziri alivyokiri, pamoja na kuwa walimu wengine wana elimu ya kutosha lakini uwezo wao ni mbaya, hili linaondoka kwa sababu ya ukaguzi bora na ulio makini wa walimu hao. Je, Mhe. Waziri haoni kuwa ukaguzi huu tulionao maskulini kwa Mwalimu Mkuu kumkagua mwalimu wake na kutaka sifa kwa kuandika ripoti ambazo si za kweli na siku zinakwenda na watoto wanaendelea kufeli, haoni kuwa iko haja ya kufanya mabadiliko ya kupata ukaguzi hasa ambao utaisaidia wizara kujua tatizo lilipo na namna ya kulitengeneza.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, swali la kwanza pamoja na jibu nililolitoa la kwamba tumenunua vifaa, vitabu, tumejitahidi kupata walimu wazuri wa kutusomeshea wanafunzi wetu kwa nini matokeo mwaka huu yamekuwa mabaya zaidi kuliko yale ya mwaka jana. Mhe. Spika, nakubaliana na *observation* zake, nakubaliana na hoja zake na hilo suala linamgusa kila Mzanzibari, kila Mtanzania. Kwa bahati mbaya na nataka niseme kwa bahati mbaya, mtihani wa *Form IV* ni mtihani unaosimamiwa na taasisi ya Muungano, tunashirikiana kusimamia na kutunga kwa kiwango kikubwa cha kuridhisha, lakini bado kunatokea kasoro za hapa na pale katika ile taasisi inayosimamia mitihani kasoro ambazo nakaribia kusema ziko nje ya uwezo wetu kuzirekebisha mpaka pale suala hili kwa jumla litakaporekebishwa.

Nataka nimueleze Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe kwamba imeundwa tume na Waziri Mkuu na katika tume hiyo mna wajumbe watatu wa Zanzibar, katika Wajumbe watatu hao mmoja anatoka katika Baraza la Wawakilishi na mna mjumbe mmoja katika ile sekretarieti itakayoweza kuandika hiyo taarifa, taarifa itaandikwa, italetwa, tutaiangalia na tutaijadili. Lakini ni kweli kwamba hayo niliyoyazungumza sio tu peke yake yanayosababisha watoto wetu kufeli, hata wanafunzi wenyewe na wao wenyewe wanasababisha kufeli kwa sababu hamu ya wanafunzi wetu kudurusu sasa hivi imepungua kuliko vile ilivyokuwa ile ya zamani. Huo ni ukweli usiofichika, lakini swali la pili nakuomba Mheshimiwa ulirejee.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, Mhe. Waziri alieleza namna alivyojitayarisha kupambana na ile hali ambayo ilisababisha wanafunzi kufeli

kwa wingi katika Mtihani wa wa Kidato cha Nne wa mwaka 2011. Lakini mimi nilimwambia pamoja na kuwa alisema kuwa kaajiri walimu waliokuwa ni wazuri nilimwambia kuwa ukaguzi ni moja kati ya sekta ambayo inaifanya wizara kujua hali ya elimu ilivyo kwa walimu na wanafunzi, lakini ukaguzi huu tunaoendelea nao katika skuli kuwa Mwalimu Mkuu kuwakagua walimu wake haoni kuwa walimu wakuu pengine ripoti wanazozipeleka sio sahihi kuidanganya serikali na wakati siko tunakokwenda na matokeo yanazidi kuwa mabaya.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwanza utaratibu wa ukaguzi si Mwalimu Mkuu anayewakagua walimu wake, kuna Afisa maalum wa ukaguzi wa skuli zetu, huyu ndiye anayekagua skuli zote pamoja na kumkagua huyo Mwalimu Mkuu unayemzungumza. Huyu ndiye anayetuletea ripoti na sisi tunafuatilia ili tujue ripoti yake amefanya nini. Ni kweli kabisa ukaguzi unaoendelea sasa hivi sio huo unaouzungumza wewe wa mwalimu mkuu kukagua walimu wenzake hapana, huo nilioutaja mimi kwamba kuna mkaguzi mkuu maalum wa kukagua skuli zetu tumeuona kwamba hauridhishi, tumeamua karibuni hivi tutatangaza mkaguzi mkuu kwa sababu aliyepo anastaafu tutamtangaza na tutatangaza utaratibu mzima tunaoubadilisha wa ukaguzi wa skuli zetu ili ripoti au taarifa ya ukaguzi tutakayoipata iweze kufanyiwa kazi kwa kina na tupate kuondosha moja katika hilo tatizo linalosababisha watoto wetu wengi kufeli.

Mhe. Omar Ali Shehe: Nakushukuru Mhe. Spika, kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kadiri tunavyoendelea kujenga mabanda ya skuli na kuajiri walimu pamoja na kununua vifaa, matokeo ya wanafunzi wetu kwa kweli hayaoneshi kwamba kuna dalili ya mafanikio katika suala hilo. Na inavyoonesha kwamba kuna tatizo la msingi ambalo bado hatujaweza kuligundua katika suala hilo.

Sasa je, serikali haifikirii kufanya tathmini au utafiti wa kina utakaowashirikisha wataalamu na wadau wengine wa Sekta ya Elimu kwa hapa Zanzibar ili kubaini tatizo la elimu kwa Zanzibar yetu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli kabisa nakubaliana na yeye mtazamo wake kwamba lazima tubadilishe utaratibu, kwa sababu pengine liko jambo bado hatujaligundua limejificha, kununua vitabu, kuweka walimu wazuri, kufanya hivi, kujenga mabanda haitoshi, nakubaliana na *observation* ya mjumbe moja kwa moja.

Napenda kukuarifu Mhe. Mjumbe na Baraza lako tukufu kwamba suala hilo tumeliona na hivi karibuni tutatangaza rasmi mkutano mmoja mkubwa sana wa wadau mbali mbali Unguja na Pemba. Mkutano huo utajadili kila

kinachoonekana kinachangia watoto wetu kufeli na hatimaye mkutano huo utatupa mawazo rasmi nini tufanye kama haya tunayofanya peke yake hayatoshi. Baada ya matokeo hayo tutarudi serikalini Baraza la Mapinduzi kuliarifu na hatimaye kupata maelekezo ya ziada ahsante sana.

Nam. 91

Ahadi ya Kuajiri Mwanasheria

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na ahadi ya muda mrefu ya kuajiri Mwanasheria atakayesaidia au atakayeshughulikia kesi za watoto huko Pemba.

(a) Ni lini serikali ahadi hiyo itaitekeleza.

(b) Ni sababu zipi zinazopelekea kituo cha Pemba kuwa na matokeo mengi ya ubakaji.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni swali lake nambari 91 lenye vifungu a na b kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli wizara iliahidi kuajiri mwanasheria atakaesaidia na kushughulikia masuala ya kisheria kisiwani Pemba. Mhe. Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia Tume ya Utumishi Serikalini tayari tumeshalichukulia hatua suala hili na Tume ya Utumishi Serikalini tayari imeshaitangaza nafasi hiyo ya mwanasheria kwa wananchi kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*) tarehe 12/03/2013. Wananchi wenye sifa zilizoelezwa kwa nafasi hiyo wametakiwa kuomba kwa muda wa wiki mbili.

(a) Mhe. Spika, Mwanasheria wa Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto atakaefanyia kazi Pemba ataajiriwa muda mfupi ujao mara tu Tume ya Utumishi Serikalini itakapokamilisha taratibu zake kwa mujibu wa sheria.

(b) Sababu kubwa ya kupatikana matokeo mengi ya ubakaji katika kituo cha *One Stop Center* huko Pemba ni kwamba hivi sasa wananchi wengi wamekuwa na muamko zaidi wa kuripoti kufuatilia kesi za

udhalilishaji zikiwemo za ubakaji kutokana na elimu na uhamasishaji uliotolewa na watendaji wa wizara hii ya ustawi wa jamii. Pia kwa kuwaka kituo hicho cha *One Stop Center* ambapo kabla ya hapo hakikuwepo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri ningemuomba kwa heshima ya hali ya juu kuwa hali ya Pemba hivi sasa hairidhishi hata kidogo kutokana na watoto wengi kubakwa. Kuingia tu kamati katika kazi zake Mhe. Spika, kufika ilikaribia kulia machozi kumkuta mtoto wa miaka sita (6) aliyeharibiwa vibaya na kamati ilikaribia kulia na kutoa mchango mkubwa wa kumpeleka hospital na kituo cha polisi. Kwa hivyo, naomba suala hili lichukuliwe *serious* na apelekwe mwanasheria.

Uzoefu unaonesha kwamba, watu wanaopelekwa Pemba wanataka kurudi, serikali imejiandaa vipi kuhusu vitendea kazi ikiwemo usafiri wa mwanasheria huyu kupata gari kwa wilaya nne kutumika.

Pili, katika kipindi cha mwaka 2010/2911 kuna kesi 127 zimefunguliwa, kesi 66 zimesikilizwa tatu tu, kwa masikitiko makubwa ndizo zilizopata hukumu. Ni sababu gani zilizopelekea kesi hizo kutupwa mahakamani.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwanza naomba nijibu hili la udhalilishaji. Mhe. Spika, taratibu zipo, zinafuatwa, watu wanapeleka malalamiko yao na kesi zao kupitia *One Stop Center* lakini kwa bahati mbaya sana kesi bado hazijahukumiwa. Hata hivyo, tunaona kwamba mwelekeo wa kuhukumiwa kesi upo na utakuwa mzuri, kwa sababu tumekubaliana tukae pamoja kila baada ya miezi mitatu na viongozi mbali mbali wanaohusiana na mambo haya ili kueleza kuna tatizo gani kwa mfano mtu amekatwa ulimi, ni ushahidi tosha kwamba yeyé kweli alikuwa katika ubakaji na hadi leo hajahukumiwa anasubiri nini.

Mambo haya ya magari au usafiri suala hili tutajitahidi ili mambo yetu yaende vizuri.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipa nafasi asubuhi hii kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Pamoja na majibu yake ameeleza hapa kwamba wananchi tayari wamepata muamko. Lakini je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kuwa sheria hii aliyokuwa nayo ina mapungufu na ndio maana watu wakaendelea kubaka.

La pili, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kuwa sasa hivi ipo haja serikali ikaunda rasmi Mhakama ya Wanawake na Watoto.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwanza nataka nikatae kwamba sheria yetu ina matatizo. Haina matatizo yoyote, ina mambo yaliyo wazi na tumeikubali sisi wenyewe kupitia chombo hiki. Kwa hivyo, tutajitahidi sheria ifuate mkondo wake.

Mhe. Spika, kuhusu Mahkama ya Wanawake na Watoto hivi karibuni imezinduliwa Mahkama ya Watoto, lakini ya wanawake naona vado suala hili kwa hivyo kwanza twende na hii hii ya watoto.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri tunakushukuru na hapa ndio mwisho wa maswali tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Maji na Nishati na Mambo Yanayohusiana na Hayo

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe kwa heshima na taadhima napenda kuwasilisha kwenye Baraza lako tukufu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Maji na Nishati ili kuimarisha usimamizi katika utoaji wa huduma bora za maji na nishati hapa nchini.

Mhe. Spika, chimbuko la mswada wa sheria hii ni utekelezaji wa sera ya nishati ya mwaka 2009 ambayo imeelekeza haja ya kuwa na Mdhibiti wa Nishati kama inavyojieleza kwenye mkakati Na. 2 katika hoja ya sera Na. 6, hivyo wizara kwa kutekeleza mikakati iliyojiwekea katika sera hiyo imeamua kutayarisha sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Matumizi ya Nishati na Maji.

Vile vile serikali imeona haja ya kuwepo kwa Mdhibiti wa Huduma za Maji hasa kwa vile sera ya maji ya 2004 inawataka wananchi kuchangia huduma ya maji, hivyo imeonekana ni vyema kuanzishwa kwa Mdhibiti ambaye atakayekuwa anashughulikia sekta zote mbili za maji na nishati. Kwa upande mwengine kuanzishwa kwa sheria hii kumekuja kutokana na azma ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kutaka kila nchi mwanachama awe na Mdhibiti katika suala la nishati.

Karibu nchi wanachama wote tayari wameshaanzisha taasisi za Mdhibiti wa Nishati na Maji. Upande wa Tanzania Bara tayari wameanzisha EWURA.

Zanzibar haikutaka kuwa nyuma katika kutekeleza suala hilo hasa kwa vile suala la nishati si suala la Muungano, hivyo Zanzibar imeona ipo haja ya kuwa na Mdhibiti wake mwenyewe ili aweze kuiwakilisha kikanda.

Mhe. Spika, madhumuni ya mswada huu wa sheria ni kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kudhibiti huduma za maji na nishati. Mamlaka hii imekusudia kutoa mchango mkubwa katika usimamizi wa upatikanaji wa huduma bora za maji na nishati kwa nia ya kuimarisha uchumi na hali ya wananchi.

Vile vile kutokana na msukumo wa sasa wa kuwa na huduma zisizoridhisha zimetoa sindikizo kubwa kwa kuwepo kwa chombo hiki hapa Zanzibar ambacho kwa kiasi kikubwa kinategemewa kutatua tatizo hili.

Mhe. Spika, mswada wa sheria hii umetungwa kwa ajili ya kuzuia ongezeko holela la bei na pia kuondosha tatizo la kutokuwepo msimamizi mahususi wa sekta ya nishati hasa katika suala la mafuta.

Vile vile ulazima huo unakuja kwa kuweza kudhibiti biashara ya gesi asilia hususan LPG, gesi inayouzwa kwa matumizi ya kupikia ambayo kwa sasa inayoonekana kutokuwepo na usimamizi mzuri wa biashara hiyo licha ya kukua kwa sekta hiyo kwa nguvu. Ama kwa upande wa nishati ya umeme, mamlaka inayoanzisha itasaidia kuimarika kwa Shirika la Umeme kiutendaji kwenye ukusanyaji wa mapato na huduma inayotolewa na shirika hilo ikizingatiwa kuwa mamlaka itakuwa inasimamia kwa karibu kiwango cha huduma ya umeme kinachotolewa sambamba na usimamizi wa bei ya umeme wenyewe. Kwani kuongezwa kwa bei ya umeme itahitaji ridhaa na uamuzi wa mamlaka ambapo katika kulitekeleza hilo, mamlaka inazingatia vigezo tofauti ikiwa ni pamoja na kusikiliza maoni ya wananchi.

Kwa upande wa huduma ya maji sheria itasaidia kuimarika kwa Mamlaka ya Maji katika ukusanyaji wa malipo yanayolipwa na wateja na pia kuangalia ubora wa utoaji wa huduma yenyewe. Kwa ujumla kuanzishwa kwa chombo hiki kunatarajia kuongeza ufanisi na uhakika wa huduma, uwazi na ushindani wa kibei katika huduma ya maji na nishati hapa nchini, na hivyo kutoa mchango mkubwa katika kuimarisha ubora wa huduma na kupatikana mahitaji ya wananchi kwa bei halisi kulingana na gharama za uzalishaji.

Kwa vile Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Maji na Nishati itakuwa inatoa leseni kwa madhumuni ya kudhibiti huduma kwa maslahi ya watoaji huduma wanaoendesha shughuli zao kwa ufanisi na kwa maslahi ya wananchi kwa jumla, kutakuwepo na mazingira yanayotambua haki za kila upande wa utoaji na unaohitaji huduma na kwa hivyo hali hiyo itapelekea kuwepo kwa huduma endelevu.

Mambo muhimu yaliyozingatiwa katika sheria:

Mhe. Spika, kwenye sheria hii suala la kuunda chombo ambacho kinakubaliana na miundo ya taasisi ziliopo hapa Zanzibar limezingatiwa kwa madhumuni ya kuwa na chombo ambacho kitaweza kutekeleza kazi zake bila ya kugongana na sheria nyengine za hapa nchini.

Vile vile masuala mengine muhimu yaliyozingatiwa ni pamoja na kuweka mfumo wa uwajibikaji, uwazi na kuijenga taasisi yenye gharama nafuu kiuendeshaji.

Uwakilishi wa Wadau:

Mhe. Spika, matayarisho ya mswada huu yalianza mara tu baada ya kupokelewa kwa maagizo kutoka serikali kuu mnamo mwishoni mwa mwezi wa Disemba, 2011. Vikao mbali mbali Unguja na Pemba vilifanywa kwa kuwashirikisha wadau mbali mbali ambao walitoa michango yao kwenye vikao hivyo wakitokea katika sekta binafsi, taasisi zisizo za kiserikali, taasisi za kibiashara, taasisi zinazotoa huduma ya nishati na maji, taasisi za serikali zinazosimamia kodi na kadhalika.

Vile vile vikao mbali mbali vya ndani ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati vilifanywa katika kutoa miongozo kwenye matayarisho ya mswada huu, mbali ya vikao hivyo pia mswada ulipata maoni ya Mshauri Mwelekezi ambaye alikuja maaluma kwa ajili ya kuupitia na kutoa maoni yake ili kwenda sambamba na viwango vya wadhibiti wa kikanda na kimataifa.

Katika hatua za mwisho wa utayarishaji wa mswada huu zilihitimishwa kwa kutolewa semina maalum kwa wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza lako tukufu tarehe 12 mwezi wa pili 2013.

Aidha tarehe 26 mwezi tatu 2013, kamati hiyo iliipitia mswada huu na kutoa maoni ambayo wamepelekea mswada huu kuwa katika hali nzuri zaidi.

Muundo wa Sheria:

Mhe. Spika, mswada wa sheria hii umegawika katika sehemu 8 na una jumala ya vifungu 53. Sehemu ya kwanza ni vifungu vya utangulizi vinavyotaja jina sheria yenyewe, sheria ya mamlaka ya udhibiti na matumizi ya maji na nishati *Zanzibar Utilitiy Regulatory Authority* (ZURA) na ufafanuzi wa baadhi ya maneno muhimu.

Sehemu ya pili kwenye kifungu cha 3 kinazungumzia uanzishwaji wa Mamlaka ya Kudhibiti Matumizi ya Maji na Nishati. Kifungu cha 4 kinazungumzia muundo wa mamlaka kuwa itaongezwa na Mkurugenzi Mtendaji ambaye atachaguliwa na Rais.

Mamlaka itakuwa na wakurugenzi wengine ambao watachaguliwa na bodi pamoja na wafanyakazi wengine.

Kifungu cha 5 kinaonesha majukumu ya mamlaka.

Kifungu cha 6 kinazungumzia uwezo wa mamlaka.

Kifungu cha 7 hadi 20 vinazungumzia viwango na malipo, kukasimu, kuanzishwa kwa bodi ya wakurugenzi wa mamlaka, muundo wa bodi, majukumu ya bodi, uwezo wa bodi, ukomo wa bodi, katibu, vikao vya bodi na maslahi.

Sehemu ya tatu ya mswada huu inazungumzia vifungu vya fedha. Kifungu cha 21 kinazungumzia mapato ya mamlaka. Kifungu cha 22 kinazungumzia bajeti. Kifungu cha 23 kinazungumzia mahesabu na ukaguzi ambapo mamlaka inatakiwa kuweka kumbukumbu za fedha.

Kifungu cha 24 kinazungumzia ripoti ya mwaka na mamlaka.

Mhe. Spika, sehemu ya nne ya mswada wa huu una vifungu kumi.

Kifungu cha 26 kinaonesha kutunza daftari. Kifungu cha 27 kinazungumzia suala la uwajibikaji na kifungu cha 28 vinaonesha umuhimu wa mamlaka kuwa na kanuni za maadili, yaani *Code of Conduct* ambazo zitaridhiwa na Waziri zinazoonesha kiwango cha utendaji kinachotakiwa kutekelezwa na watendaji.

Kifungu cha 29 kinaonesha suala la usiri wa taarifa, mgongano wa maslahi. Kifungu cha 30 na 31 hadi 33 Baraza la kuwakilisha watumiaji na Kifungu cha 34 kusikiliza jamii.

Sehemu ya tano inazungumzia kuhusu kutatua migogoro. Mamlaka itakuwa na uwezo wa kusikiliza na kutatua migogoro yote baina ya watumiaji, wasambazaji au taasisi ya serikali inayotumia sheria hii. Kifungu hiki cha 36 kinaonesha taratibu zitakazotumika katika kutatua migogoro hiyo.

Mhe.Spika, sehemu ya saba inazungumzia rufaa. Kifungu cha 40 mpaka 42 kwa mujibu wa sheria hii rufaa zitapelekwa katika Mahkama Kuu, lakini

sheria imeelekeza kabla ya kukata rufaa, mtu au kampuni ataomba kwa mamlaka amri ya kufanya tena mahesabu au kuyaangalia upya baada ya kufanyika hayo ndipo muombaji anaweza kupeleka shauri lake Mahakamani ikiwa hajaridhika.

Sehemu ya nane ambayo ndio ya mwisho na ambayo ni mengineyo pamoja na mambo mengine waziri atakuwa na uwezo wa kutoa mapendekezo ya jumla kwa mamlaka, lakini mapendekezo hayo yasiende kinyume na sheria hii au sheria zinazosimamia huduma hizi.

Kifungu cha 47 kinampa uwezo waziri kutunga kanuni ambazo hazitokwenda kinyume na sheria hii. Kifungu cha 51 kinaonesha kufutwa kwa baadhi ya vifungu vya sheria ya maji ya Nam. 4 ya 2006 na sheria ya Shirika la Umeme la Zanzibar Nam. 3 ya 2006.

Kifungu cha 52 kinaonesha uhalali wa shughuli zilizofanywa kabla ya kufanya kazi kwa sheria hii na kifungu cha 53 kinaonesha sheria itakayotumika ikiwa kutakuwa na migogoro au mgongano na sheria nyengine.

Mhe. Spika, ni matumaini yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wamepata muda wa kupitia mswada huu na hivyo naomba kuwasilisha Wajumbe wachangie na kushauri ipasavyo na hatimaye kupata muongozo wako kwa hekma na busara.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Marina Joel Thomas (Kny: Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi):

Mhe. Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake, kwani ni yeye ambaye ametuwezesha kukutana tena katika mkutano huu wa kumi na moja tukiwa na afya njema na uwezo wa kuwatumikia wananchi wetu, hivyo hatuna budi kumshukuru juu ya neema hii aliyoturuzuku.

Mhe. Spika**,** pili napenda nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa lengo la kuwasilisha maoni ya kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusiana na Mswada wa Sheria ya kuanzisha Mamlaka ya udhibiti wa huduma ya Maji na Nishati Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika**,** pia napenda nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pamoja na watendaji wake wote kwa mashirikiano

waliyotupatia wakati wa kuupitia na kuuchambua mswada huu, bila shaka mashirikiano yao yamefanya kazi hii iweze kufanyika kwa ufanisi mkubwa sana.

Mhe. Spika**,** katika kuuchambua mswada huu pia wananchi na taasisi mbali mbali zilishiriki katika kutoa maoni yao kwa lengo kuufanya uwe bora zaidi na ukizingatia kwamba mswada huu walengwa wakubwa ni wao, hivyo pia sina budi kuwashukuru na kuwapongeza wadau wote waliochangia katika uchambuzi wa mswada huu kwa namna moja au nyengine, michango yao imeisaidia sana kamati yetu kuweza kufikia lengo.

Mhe. Spika**,** nitakuwa sikutenda haki iwapo nitakosa kuwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa kazi nzuri na ya thamani waliyoifanya hadi kuniwezesha mimi leo hii kusimama hapa na kuwasilisha maoni ya kamati kwa niaba yao, hakika umoja na mashirikiano ndio ngao iliyopelekea mafanikio haya,

Mhe. Spika, naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Mwenyekiti
2. Mhe. Hassan Hamad Omar - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Salma Mussa Bilal - Mjumbe
4. Mhe. Subeti Khamis Faki - Mjumbe
5. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - Mjumbe
6. Mhe. Marina Joel Thomas - Mjumbe
7. Ndg. Aziza Wazir Kheir - Katibu
8. Ndg. Maryam Rashid Ali - Katibu

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo sasa naomba uniruhusu nianze kuuchambua mswada huu moja kwa moja, Mhe. Spika kuwepo kwa Sheria hii ni utekelezaji wa sera ya Nishati ya mwaka 2009 ambayo pamoja na mambo mengine imeelezea haja ya kuwepo kwa chombo cha udhibiti, sambamba na sera hiyo, kwa sasa Jumuiya ya Afrika Mashariki imezitaka nchi wanachama kuwa na chombo cha udhibiti wa nishati, hivyo basi takriban nchi nyingi tayari zimeweka utaratibu wa kisheria wa kuanzisha chombo hicho.

Mhe. Spika, kuwepo kwa chombo hichi katika nchi yetu kutasaidia kuzuia ongezeko la bei kwenye huduma hizo na pia kusimamia ubora wa huduma inayotolewa kulingana na viwango vilivyowekwa na Sheria hii.

Mhe. Spika**,** kamati yetu imeona umuhimu wa kuwepo kwa mamlaka hii katika nchi yetu kwani ni wazi kuwa itasaidia kusimamia masuala ya huduma ya maji na nishati ambayo kwa sasa tunaona kuna matatizo na usumbufu mkubwa katika huduma ya nishati ya petrol katika jamii yetu hali ambayo hupelekea kutolewa mafuta yasio na kiwango lakini pia usumbufu wa kupatikana kwake, kwa hiyo kwa kuanzishwa kwa mamlaka hii ambayo itasimamia masuala ya nishati ikiwemo petrol ni matumaini yetu kwamba kero na matatizo haya yataondoka kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Spika**,** ili kuona madhumuni ya kuanzishwa kwa mamlaka hii yanafikiwa, kamati yetu inashauri kwamba katika mamlaka hiyo kuchaguliwe bodi iliyo imara na madhubuti katika kusimamia uendeshaji wa shughuli za Mamlaka hiyo, hivyo kamati inapendekeza wajumbe wa bodi wateuliwe kutumikia mamlaka kwa kipindi cha miaka mitatu na waweze kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

Mhe. Spika**,** pamoja na mambo mengine kamati yetu inaipongeza Wizara kwa kuweka ndani ya mswada huu Baraza la kuwawakilisha watumiaji, kamati yetu imeridhika kwa kuwepo kwa Baraza hili ndani ya Mamlaka hii kwani itawapa fursa watumiaji kuwakilisha maslahi katika Mamlaka kwa kutoa mitazamo na taarifa zao

Mhe. Spika**,** kamati yetu imeona umuhimu wa kuwepo kwa kipengele kinachoelezea utaratibu wa utatuzi wa migogoro katika mswada huu kwani katika Mamlaka kama hii inayodhibiti huduma malalamiko na migogoro ni vitu visivyoepukika,hivyo ni busara kubwa kuweka utaratibu wa kushughulikia migogoro hiyo ili kuona udhibiti hasa unakuwepo katika huduma zilizokusudiwa.

Mhe. Spika**,** baada ya kuupitia mswada huo, kamati yetu imependekeza baadhi ya marekebisho kwa lengo la kuimarisha mswada huo. Kwa ruhusa yako Mhe.Spika naomba niainishe baadhi ya marekebisho kama ifuatavyo;

Mhe. Spika**,** katika tafsiri ya neno “Waziri” kamati imependekeza isomeke “maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Mamlaka ya udhibiti kama atakavyoteuliwa na Rais”, kamati imependekeza hivyo ili iendane na tafsiri ya mswada wa kiengereza, vile vile kamati imependekeza iongezwe tafsiri ya neno ‘ZBS”ambavyo inapatikana katika mswada wa kiengereza.

Mhe. Spika**,** katika kuweka ukomo wa kutumikia Mamlaka kamati imependekeza kifungu 4(4) kisomeke "Mkurugenzi Mkuu atateuliwa kutumikia Mamlaka kwa kipindi cha miaka minne na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja"

Pia katika kifungu cha 20 kamati imependekeza maneno ya pembeni yasomeke "bodi kujiwekea taratibu" hii ni kutokana na kwamba maneno yaliokuwepo hayaoneshi mantiki ya kifungu halisi.

Mhe. Spika**,** kamati yetu pia ilifanya marekebisho ya uchapaji kama yanavyoonekana katika waraka wetu tuliouwasilisha kwako na nakala za waraka huo kusambazwa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa msingi huo, na kwa kujali muda wako Mhe, Spika nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waupitie waraka huo ili kuona baadhi ya vifungu ambavyo sikuwahi kuvitolea maelezo hapa.

Mhe. Spika, kwa muhtasari hayo ndio mapendekezo ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusiana na Mswada wa Sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Maji na Nishati Zanzibar na mambo yanayohusiana na hayo. Sasa kwa heshima nawaomba Wajumbe wote wa Baraza hili nao wauchangie vizuri Mswada huu kwa lengo lile lile la kuuimarisha zaidi na hatimae kuukubali bila ya pingamizi yoyote.

Mhe. Spika**,** napenda kutamka bayana kuwa mimi binafsi na kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi asubuhi hii kuweza kuutilia baraka mswada huu ulioletwa kwa madhumuni mazuri na mwenyewe ukiongozwa na Mhe.Waziri pamoja na Katibu wake na Naibu wake na watendaji wake na wanasheria wake kutuletea hapa katika Baraza hili tukufu ili kuweza kuupitisha na kuunga mkono kwa nia nzuri tu.

Mhe. Spika, mamlaka hii imekuja wakati mzuri sana na hususan kwa Kamati yangu ya Mawasiliano na Ujenzi, hasa hivi karibuni tulipata bahati kwenda kupata zoezi zuri sana kwa wenzetu; tulikwenda kusoma jinsi gani wenzetu mamlaka wanavyoendesha, jinsi gani wenzetu wanavyokaa na mamlaka nyengine ili kufanikisha katika masuala ya upangaji, kutafuta huduma nzuri na halikadhalika na hasa kwenye mambo ya mafuta na maji.

Mhe. Spika, tatizo langu ni moja tu. Mara nyingi sana Mhe. Spika, tunaunda kamati hizi za mamlaka lakini baadae tunakuja kuzinyima power, hili mimi ndio ambalo ninalokuwa linanitia wasi wasi, tukubaliane hapa kwa kupitisha na kumrahisishia Mhe.Rais kutia saini hii mamlaka iwe, tumesema kutakuwepo na chombo cha bodi, kutakuwepo na mabaraza na kila aina ambazo vitengo vitakavyosaidia mamlaka.

Lakini la kusikitisha sana Mhe. Spika, tunaziunda mamlaka zetu lakini hatuzipi nguvu, na kwa nini nikasema hivyo. Tunafunga sana yale maeneo ya kutaka kujiendesha wanakuwa wanashindwa.

Mhe. Spika, tulikwenda kule tumeangalia National House. Wenzetu wale mamlaka ya nyumba serikali imewaachia kabisa na ndio maana wakaweza sasa hivi wana uwezo wa kuiendesha serikali hasa kwenye bajeti kwa kuweza kuchangia. Wamepewa vibali vya kuweza kukopa benki fedha wanazotaka wenyewe.

Lakini sisi tunakuwa tunashindwa Mhe. Spika, kufanya kitendo kama hicho. Mhe. Spika, sasa mimi hapa ndio hupata tatizo kubwa. Tunawataabisha wataalamu, tunamtaabisha Waziri anakaa anafikiri anawaza anasema hiki ni chombo nitapokileta Barazarani nitakapoungwa mkono na Mhe. Rais atakapotia saini, lakini hatimaye hakifanyi kazi yake bado tunaibana.

Mhe. Spika, wenzetu walitwambia kwamba wamepewa kibali cha fedha bilioni na kwa kuwa wameona taabu sana walianzia na zoezi la kuchukua kama bilioni mbili au tatu nyengine wameziacha kwenda kukopa. Hivyo ndivyo inavyotakiwa mamlaka lakini mimi ninashangaa mamlakaa hizi zina modern gani labda Mwanasheria atanisaidia, tuna muunda gani wa sheria ambazo hizi tunazitunga sheria tunazicha halafu tunazirudia kuzibana zile sheria zetu. Labda atanitafunia lugha Mwanasheria anisaidie *modern* gani tunakuwa hata tunafika pahali tunakubali sheria halafu tunazibana sheria.

Mhe. Spika, mimi hili suala huwa mkali sana tuwape uhuru mamlaka. Mhe. Spika, tukisema kwa mfano hivi karibuni tulipitisha mamlaka ya uwanja wa ndege lakini la kusikitisha wameitisha tenda mpaka leo hatujui mpaka leo imekwenda wapi. Lakini tetezi za midomo za hapa na pale tunaambiwa serikali bado ina masawazisho ni masawazisho gani, wale wameshaona kuwa hivi sasa tunataka twende katika *international airport* tutafufe wawekezaji waliokuwa *compentent* lakini hatimaye tunawaingilia kati.

Sasa hiki chombo nina wasi wasi nacho cha leo Mhe. Spika, ndio itakuwa yale yale na ni muhimu sana chombo chiki. Kwa sababu Mhe. Waziri kaona alete hiki chombo kwa sababu tayari wananchi kila siku tunauziwa mafuta

mabovu, hasara tupu. Sasa mimi naomba Mhe. Spika, tuzipe uhuru na tuziachie hizi mamlaka zijiendeshe wao wenyewe, wawe na maamuzi ya haraka sana wao wenyewe wasingojee mzunguko, sijui ipite wapi, ipite kwa waziri, ipite kwa Makamu au Rais aah! Wakati ikiwa ni jambo zuri waamue wao wenyewe taarifa tu zije kwenye serikali kuu, hapo Mhe. Spika, tutakuwa tumefanya haki.

Mhe. Spika, tulikwenda Arusha tuliona jinsi gani wenzetu AUSA, mamlaka ya maji hawa ni jinsi gani wanavyoshirikiana na mamlaka nyengine ambayo inayoitwa AWURA wanavyokwenda vizuri sana. Sasa na hili ndio lengo lake Mhe. Waziri. Hiki chombo cha ZURA lazima kiende sambamba na nishati yenyewe hasa, *quality* ya kutafuta mafuta yetu jinsi gani wananchi wanapata maji safi, jinsi gani mpangilio wa bei wanaokaa wakaupanga. Mhe. Spika, sasa hivi wananchi wetu tuwaombe radhi wakubali tu tusijekubadilika kuichangia hii ZAWA. Wenzetu huko sasa hivi wameshatuacha mbali sana, wanawalipa vizuri kwa mitandao mizuri. Wao nao wawe na *system* hii katika hiki chombo tutakachokipitisha basi na wao wenzetu wafuatilie na waende na *system* nzuri kama tulizoziona kule. Sasa hivi mita ziwe nyingi sana.

Mhe. Spika, kwa hilo ndio mimi nikaona niweze kuchangia kwa kuwatetea hawa mamlaka wapewe uhuru na serikali, tuwaachie wenyewe, wanasiasa tukae pembeni tuwaachie wafanye kazi. Vyengine vyovyote Mhe. Spika, tukijiingiza na sisi wanasiasa tutapata matatizo, tunawaendesha ovyo, tuwaachie pembeni ili wafanye kazi zao vizuri ili watuletee neema kwa sababu hii ni neema Mheshimiwa.

Mhe. Spika, tukija kwenye ukurasa wa 346 katika masuala ya mafuta. Mhe. Spika, hivi karibuni kulikuwa kuna matatizo ya mafuta na tulikuwa tunamtafuta nani tumlaumu ZRB, Wizara ya Fedha au Wizara ya Majenzi wenyewe kwa kupitia idara yake ya nishati. Lakini leo nani tutakwenda kumlaumu sasa na ndio uzuri huo Mhe. Waziri na watu wake, sasa tumtafute nani wa kwenda kumlaumu, tumeshampata na ninaamini Wajumbe wataunga mkono, naamini hivyo watakubali tu kupitisha bila ya tatizo lolote, sina tatizo na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kabisa.

Mhe. Spika, tulikuwa tuna utata mkubwa, bei zinapanda kiholela, mafuta yanakuwemo kwenye *deport* kule, lakini wanangojea bei zipandishwe eti ndio watoe mafuta. Hili lilikuwa ni tatizo kubwa sana. Sasa Wazanzibari wote watafurahi sana baada ya kusikia kuna chombo hiki sasa hivi. Ni maajabu kama alivyosema Mhe. Waziri, namuunga mkono hakuna kitu hiki, sisi kazi yetu ni kuleta vitu vya maajabu ajabu, utekelezaji ndio mgumu tu basi, lakini kwa kutunga sheria zilizokuwa nzuri, hata mwenyewe Mhe. Mwanasheria

Mkuu anastaajabu sana, kuwa tunatunga sheria nzuri lakini mwisho wake Mhe. Spika, unakuwa hauna utekelezaji mzuri.

Mhe. Spika, hii mamlaka ambayo itakayopitishwa hapa wasifanye mzaha, atakayechezea tu anyang'anywe leseni, atakayetuletea mafuta mabovu basi anyang'anywe leseni. Mhe. Spika, hatufanyi hivyo, leo unga ule pale mpaka leo umeng'ang'anaa tu pale Bandarini, mtu anajulikana aliyeleta lakini hajanyang'anywa leseni, si kakusudia kuja kutumaliza, hilo ni kweli ni lazima tuseme ukweli Mhe. Spika. Sasa na hawa ni lazima wawe *strict* kabisa. Mtu ambaye analeta mafuta mabovu asiachiwe anyang'anywe leseni tu. Mara ngapi gari zilikufa chungu nzima, mafuta yalichanganywa yale, lakini mpaka leo mtu hajanyang'anywa leseni. Sasa hili ndio tatizo letu Mhe. Spika, kuwa tunatunga sheria lakini zinaishia kwenye *briefcase* hazifanyi kazi. Haya mambo yanasikitisha sana.

Leo unga una sumu ukisogea pale pua inakatika, *automatic* unga upo ndani ya kontena basi pua inakatika kwa sababu ya unga mbovu. Mtu anajulikana na anadharau serikali mpaka leo hajatii amri kuondoa pale, tunangoja nini Mhe. Spika. Ndio pale tunapoambiwa huyu mtu ana mkono ndani ya serikali kwa nini anaogopwa, anyang'anywe leseni, atumalize Wazanzibari haiwezekani, kama katumwa ni huko huko, lakini tunasema kuwa lazima mtu kama huyo anyang'anywe leseni mara moja. Wahusika wa vyombo mnahusika mnyang'anyeni leseni mara moja huyo mtu muondoweni.

Basi Mhe. Spika, hii ndio maana ya kuzitungia sheria mamlaka kama hizi zifanye kazi, lakini sio kuwa tunatunga sheria halafu zinamuonea haya mtu. Sasa tunawaambia chombo hiki kifanye kazi kwa madhubuti kabisa, asiyeweza aondoke mara moja, wako wengine wanataka kazi, kabisa hakuna kumuonea haya mtu. Kama mtu hawezi kuleta mafuta *quality* muondoe, hatuwezi kupata maji safi mnyang'anye leseni hivi ndivyo tunavyotaka Mheshimiwa.

Mhe. Spika, tunajua hali halisi ya umeme sasa hivi ni matatizo kwetu, lakini chombo hiki kitakuwa na nguvu ya kuweza kuwaamuru watu kuleta umeme. Mhe. Spika, wako watu wanataka kuleta umeme hapa Zanzibar kusaidia. Leo nilikuwa namuonea huruma sana Dk. Mwinyihaji anajibu maswali maskini ya Mungu. Je, ingekuwa ile Kampuni ya Secrona ameshaikubali sasa hivi, taka zote Zanzibar zingekuwa zimekwisha. Lakini ni tatizo gani Mhe. Spika, samahani ningekuambia unipelekee salamu kwa Mhe. Rais, hebu mwambie anichague mimi niwe Mwenyekiti wa Miradi ya Zanzibar aone, anipe siku tatu tu Zanzibar uone kama haijabadilika hapa. Tuna uzito wa kuamua kitu chochote cha maendeleo kwa wananchi. Ajira hakuna, mishahara midogo

lakini tunazuia miradi kwa nini. Nchi ziendeshwe na miradi bwana, kila miradi ikiwa mingi na nchi ndipo inapopata faida na kodi nzuri.

Mhe. Spika, namalizia kidogo.

Mhe. Spika: Una dakika tatu kumaliza.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante. Sasa hivyo ndio tunasema kwamba mswada huu Mheshimiwa lengo lake kufanikisha kwa walengwa, tumepanga malengo mazuri, tuna wataalamu wazuri wa utafiti wa kujua hiki kitu kizuri na hiki kibaya. Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kitope wameniambia niunge mkono kwa asilimia mia kwa mia, kwa sababu ni kitu kizuri, kinakuja kwa wakati wake. Wale wananchi wamenituma na wameniambia nikakamae kabisa, suala hili la kupitisha sheria halafu mtu anyang'anywe leseni, wameniambia nisikubali hata siku moja. Mhe. Spika, sikubali kama mtu kafanya uzembe anatuletea vitu vibovu tusimseme wala tusimnyang'anye leseni. Mhe. Spika, tutamnyang'anya leseni mara moja. unga uondoke, mafuta yaletwe ya *quality* mara moja.

Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwanza nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyetujaalia neema yake hii ya uzima tukaweza kutoka majimboni kwetu na hatimaye tukafika hapa kwa ajili ya kujipangia mambo yatakayotusaidia katika maisha yetu ya kila siku.

Lakini pili nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii na mimi kutia fikra zangu katika mswada huu muhimu sana kwa jamii yetu.

Mhe. Spika, labda nianze kwa mawazo ya jumla jumla. Kwanza nataka niseme maisha yetu, wala sio Wazanzibari tu lakini maisha yetu kwa jumla binadamu tunategemea sana huduma hizi za nishati, nishati ya umeme, mafuta ya petroli, gesi, maji na nishati nyengine ni muhimu sana katika maisha yetu. Kwa sababu ya umuhimu huo basi, mimi nataka niungane sana na Waziri kuleta chombo hiki ambacho kitazingatia kwa undani, kudhibiti na kuweka viwango ilimradi nishati hizi ziwe zinapatikana na zinapatikana kwa bei inayokubalika na kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, mazingira yetu bila ya kuyawekea mikakati tunaweza tukafika siku moja tukajikuta tunapoteza rasilimali muhimu sana katika maisha yetu. Kwa hivyo, mawazo yangu mimi chombo hiki pia kitalenga huko, nimeona huku kwenye vifungu kuna udhibiti wa vyanzo vya nishati hizo.

Jambo jengine la msingi sana ambalo pia nimelikuta katika vifungu humu ni kuhusiana na hivi viwango vya bei, vya ubora na kadhalika. Mhe. Spika, hivi karibuni gari zetu nyingi ziliharibika na tukalazimika wengine kuziweka bandani, kwa sababu ya kutumia petroli isiyokuwa na viwango. Wafanyabiashara wetu wamekuwa wakitulengea tu bidhaa ambazo mara nyengine zinatutia hasara sana. Kwa hivyo, matumainio yangu chombo hiki miongoni mwa kazi zake basi kitaangalia sana ubora wa bidhaa tunazouziwa, hasa hizi za nishati kama zilivyokusudiwa humu.

Mhe. Spika, nataka nianze katika kifungu cha 8 ambacho kinataka sana kuhusu viwango na ubora. Lakini niliposoma kifungu hichi kwanza, nilikuwa napata tabu sana namna kilivyoandikwa. Maana yake ufafanuzi wa haya mambo yaliyoelezwa humu hayakufafanuliwa vizuri, kiasi ambacho huwezi kujua kiwango ni kitu gani na ubora ni kitu gani, wala kusimamia na udhibiti ni kitu gani. Maana yake ukisema kusimamia, mimi najua kusimamia ndio kudhibiti, lakini kuna kusimamia na kudhibiti. Sasa mara nyengine inakuwa labda ni hawa wanaotayarisha miswada pengine lugha inawapiga chenga kidogo. Lakini nashukuru sana nilipokuwa nasoma waraka huu wa Kamati umenisaidia sana marekebisho haya, wamejaribu kufafanua kiasi ambacho sasa unajua kiwango ni kitu gani. Kumbe kiwango kilichokusudiwa hapa ni kiwango cha bei, mimi nilidhani ni kiwango cha ubora. Ndio nikawa najiuliza, kiwango na ubora si ni jambo hilo hilo moja, kumbe ni mambo mawili tofauti baada ya ufafanuzi wa Kamati, naomba sana niipongeze Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi iliyofanya kazi hii.

Katika hilo Mhe. Spika, tunapata kuona ule umuhimu wa kamati kukaa kwanza wakapitia hii miswada inayoletwa hapa. Lakini kwa lugha nyengine niliwahi kusema wakati mmoja hapa, kwamba sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi sio wanasheria, sisi kazi yetu kubwa hapa ni *endorsement* ya sheria basi, lakini utaalamu wa sheria hatuna, wengi wetu ni wauza madodo kule mitaani, kazi yetu kuuza madodo kwa hivyo taaluma hizo za sheria hatuna. Nilikuwa nadhani sana hawa wanasheria wao wametuzidi kwa maarifa ya sheria, wasiandike jambo ambalo hatimaye sisi wauza dodo hapa tuje tukae tulitoe makosa. Mimi sidhani kama ni busara, kwa hivyo wafanye utafiti wakiandika, waandike kitu kizuri wao ni wataalamu. Mimi mbele ya mwanasheria siwezi kusema kitu, kwa sababu sina taaluma ya sheria. Lakini sasa mwanasheria aandike kitu kisha aje hapa nimwambie hapa umekosea andika vingine. Mhe. Spika, mimi nadhani wanasheria wetu wangekuwa makini zaidi.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo labda niende kwenye kifungu cha 9(l), naomba nikisome kidogo hapa. Hizi ni miongoni mwa kazi za mamlaka, inasema;

Kifungu cha 9(l)

> "Kuzingatia kwa ukamilifu utunzaji na uhifadhi wa mazingira, uhifadhi wa vyanzo asilia, afya na usalama wa watumiaji".

Mhe. Spika, ni ukweli usiopingika kwamba miongoni mwa matatizo yanayotukabili ni ukosefu huu au kutokuwa makini katika kuhifadhi mazingira yetu hasa vyanzo vya maji. Mhe. Spika, vyanzo vyetu ya maji kwa sababu ya kutokuwa waangalifu tumeviharibu sana, na sasa mitaa mingi ambayo zamani ilikuwa inapata maji kwa ukamilifu mwaka mzima, sasa maji yameadimika sana. Maji kwa kawaida yake huwa yanakaa kwenye mashimo lakini kuliko kuwa na vivuli, kule kwetu huwa tunaita mito. Kwa bahati mbaya sana wakulima wetu, sijui kwa kukimbilia rutuba ya mule pembezoni mwa mito wakawa wanafanya kilimo chao mule na wakawa wanakata miti ile iliyozunguka yale mashimo ya maji, matokeo yake maji yanapata jua na upepo yanakauka.

Mhe. Spika, sasa kwa sababu pamoja na taasisi nyengine za kuhifadhi mazingira, kama Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na hata hii mamkala ya maji ZAWA, lakini kwa sababu na mamlaka hii nayo imepewa kazi hii, mimi naomba sana suala hili kwa pamoja walishughulikie ipasavyo na ikiwezekana kurudisha hadhi ya maeneo yale ambayo zamani yalikuwa yanakaa maji ya kutosha kabisa mwaka mzima hayakauki, ili tuone ule uhalisia wa hii huduma ya maji kwa kweli inarudi kwenye hali yake ya kawaida. Lakini tukiendelea kulinyamazia hili, basi kwa kweli tutakuja kujikuta siku moja tumepoteza rasilimali muhimu sana ya maji.

Mhe. Spika, kifungu cha 10 kimetaja leseni. Mamlaka hii itatoa leseni gani. Itakuwa na uwezo wa kutoa leseni kwa ajili ya hawa watoa huduma wa mambo ya nishati hizi. Sasa ukisoma kifungu cha 10(1) unakuta pale kwenye nishati ya umeme itatoa leseni ya uzalishaji, usambazaji, uuzaji, upitishaji, upitishaji sijui maana yake nini lakini ilimradi ni katika mambo hayo hayo ya kusambazaji. Lakini nilipo mimi kwenye nishati ya umeme, leseni ya uzalishaji itatolewa, lakini ukiangalia kwenye nishati ya mafuta, leseni ya uzalishaji hapa haikutajwa, maana yake hakuna leseni itakayotolewa kwa ajili ya kuzalisha mafuta, isipokuwa kuna leseni ya usambazaji na uagiziaji. Lakini pia ukiangalia kwenye huduma ya maji, leseni ya uzalishaji maji pia haikutajwa hapa. Sasa mimi nafikiri nayo kwa sababu tunatunga sheria tukaiweka hii, japokuwa kanuni zitazuia kwanza, kwa sababu muda haujafika au vyenginevyo, lakini huwenda huko mbele ya safari tukaona uko umuhimu au haja ya kutoa leseni ya uzalishaji petroli katika nchi yetu. Au ikajakuonekana kuna umuhimu wa kutoa leseni ya uzalishaji mali ukiachia hii Mamkala ya ZAWA.

Mhe. Spika, kutunga sheria ni lazima u-*focus* mambo mengi huko mbele. Kwa hivyo, nadhani hapa napo yangewekwa hayo mambo, leseni ya uzalishaji maji hasa kwa wakati huu ukizingatia ZAWA yenyewe bado haijajitosheleza wala haijakuwa na uwezo wa kuzalisha maji yatakayoenea nchi nzima. Ndio maana japo ni kinyume na utaratibu, lakini watu wengi sasa hivi wanajichimbia visima vyao wenyewe mitaani, tena wanajisaidia kweli kweli, maana mtu mmoja akichimba kisima anaweza akawasaidia wenzake waliomzunguka wengi sana, ambapo ZAWA haijawa na uwezo wa kuwafikishia watu wale huduma hiyo ya maji.

Sasa kwa sababu mamlaka hii ndio itakayokuwa na mamlaka ya kutoa leseni, huwenda kama hii leseni ya uzalishaji maji haitawekwa hapa, vitakuja kuwa vile visima vyote ni haramu viko nje ya sheria na pengine kuwa na kisima bila ya kuwa na leseni itakujakuwa ni kosa la jinai, hofu yangu ni hiyo, tukifika huko tutasababisha matatizo makubwa sana katika nchi yetu hasa kwa wakati huu ambao ZAWA haijawa na uwezo vizuri. Kwa hivyo, nilikuwa nadhani hili ni muhimu hapa Mhe. Waziri alilenge kabisa.

Mhe. Spika, kifungu hicho hicho cha 10(3) kinasema;

Kifungu cha 10(3)

> "Mamlaka itahakikisha kuwepo kwa usawa baina ya maslahi ya watumiaji na mahitaji ya watoa huduma".

Hili ni jambo muhimu sana kwa sababu wananchi wetu hali zao ni dhaifu kiuchumi, lakini pia na ZAWA uwezo wake ni mdogo sana wa kuweza kutoa huduma. Kwanza hapa nataka niungane na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk aliyewanasihi wananchi wachangie maji kwa ajili ya kuiwezesha ZAWA iweze kutoa huduma vizuri.

Mhe. Spika, kutokana na upungufu wa maji uliopo katika nchi, sasa hivi mtu wa kawaida kwa ile siku moja tu anaweza akanunua maji yale ya kwenye madumu kwa ajili ya kukidhi mahitaji yake ya siku moja, akalipa si chini ya shilingi 5,000 kwa siku moja tu. Kwa sababu ZAWA haikumfikishia maji pale na yeye maji ni lazima ayapate, kwa hivyo anatoa karibu shilingi 5,000 kununua maji ya siku moja. Sasa ikiwa ZAWA imeweka kiwango, nafikiri sasa hivi ni shilingi 2,500/= kwa mwezi mzima. Mhe. Spika, mimi nadhani hii bado ni *offer* kubwa sana. Sasa kinachotokea hapa ni kimoja, wananchi wanasema hatulipi kwa sababu ZAWA haitufikishii maji, lakini na ZAWA nayo haiwezi kufikisha maji kama haijakuwa na uwezo, uwezo ni hii michango. Sasa tuangalie katika akili ya kawaida lipi lianze mwanzo, tufikishiwe maji bila ya pesa au kwanza tutoe pesa ZAWA wawe na uwezo watuletee maji. Nafikiri mtu wa kawaida anaweza kufikiri tufanye nini.

Maana yake mimi nikitaka maji ni lazima nigharamike kwanza nichimbe kisima, kwa hivyo bila ya kupata yale maji kwanza ni lazima nitoe pesa niwape watu wanichimbie kisima.

Mhe. Spika: Unazo dakika tano.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Inshaallah. Kile kisima kikishakuwepo ndio sasa maji yatatoka. Kwa hivyo, nawaomba sana wananchi ili hayo maji wayapate basi waiunge mkono ZAWA kwa kutoa hii michango midogo sana kwa kweli ukilinganisha na huduma ya maji na umuhimu wake.

Mhe. Spika, muda unakwenda mbio sana. Sasa naomba niende kifungu cha 37 ambacho ni makosa na adhabu. Imeelezwa hapa katika kifungu kidogo (1) kinasema;

Kifungu cha 37(1)

> "Mtu yeyote mfanyakazi wa mamlaka au mjumbe wa bodi atakayevujisha taarifa au atakayesababisha kuvuja kwa taarifa za mamlaka au za bodi bila ya idhini ya mamlaka, atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni 5 na isiyozidi milioni 10 au kifungo cha miaka isiyopungua 5 na isiyozidi 7 au vyote".

Sasa kilichonishangaza mimi ni kwamba yule anayevujisha siri za mamlaka yeye anakuwa ni mkosa. Lakini mtu anayetega sikio kupewa taarifa za siri za mamlaka na yeye anakuwa mkosa. Sasa hivi mtu atoke huko Mhe. Spika, aje anihadithie jambo ambapo mimi sijui kama lile analonihadithia ni kosa au laa, lakini hivyo kulisikiliza tu mimi ninakuwa mkosa, ndio ilivyo katika kifungu hiki cha (2). Kwa hivyo mpokeaji au mnufaikaji yeyote wa taarifa zilizotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki atakuwa mtenda kosa na atakapotiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni 2 au kifungo cha miezi 3 au vyote kwa pamoja. Mimi nadhani kifungu hiki Mhe. Spika, hakina mantiki, wa kubanwa hapa ni yule aliyevujisha siri, aliyetoa taarifa. Lakini mtu aliyeambiwa jambo mimi sidhani kama anaweza kuwa mkosa, vyenginevyo na yeye akishaambiwa aende akamuhadithie mtu mwengine. Kwa hivyo, naona hiki kifungu ni afadhali Mhe. Waziri angekisamehe akakitoa.

Vile vile kuna kifungu cha mgongano wa kisheria hapa, kifungu cha 53 kinasema;

Kifungu cha 53

> "Mamlaka itakuwa na uwezo, majukumu, kazi na wajibu uliowekwa na sheria hii, endapo kutakuwa na mgogoro, mgongano baina ya sheria za kisekta, kanuni au taratibu, sheria hii ndiyo itakayotumika hadi pale Waziri atakapoelekeza vyenginevyo".

Mhe. Spika, hili ni suala la kiutafiti na ninafikiri wanaotunga sheria wangeangalia sasa sheria tunayoitunga inagongana na kifungu gani na gani cha sheria ipi, ili kirekebishwe. Kama walivyofanya hapa kwa kusoma kifungu cha 51, kuna baadhi ya vifungu vya mamlaka ya Shirika la Umeme vinafutwa na baadhi ya vifungu vya sheria ya maji navyo vinafutwa. Sasa ukiweka hii basi maana yake kama kutakuwa na muingiliano na sheria nyengine zisizokuwa hizi mbili zilizotajwa, maana yake sheria hii ndio inakuwa na nguvu. Sasa huu ni mgogoro wa kisheria.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nadhani wafanye utafiti kwanza ili wagundue ni sheria gani ambazo zitagongana na sheria hii wazitaje humu kuwa zinafutwa kabisa, sio wakati wa kutumia sheria hii au kutumia sheria nyengine hizo za kisekta kunakuwa na matatizo, sheria hii inasema hivi na sheria hii inasema hivi. Kama ambavyo tunavutana sasa hivi katika tume za utumishi za mihimili yetu hii.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nadhani Mhe. Waziri atayazingatia na mimi kwa umuhimu wa mamlaka hii naunga mkono, kwa niaba ya wananchi wangu kwa asilimia mia moja ahsante sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Spika na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia mswada huu ambao uko juu ya meza yetu. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutuwasilishia mswada huu muhimu kwani ni moja ya mambo yaliyokuwa muhimu ni maji katika uhai wa mwanadamu. Kwa hivyo, leo kutuletea sheria hii ya kuanzishwa mamlaka ni jambo la kumpongeza Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, kwa vile nilikuwa najitayarisha kuchangia hili suala ili kuchangia vizuri, lakini kwa bahati haijafika nafasi yangu kwa maombi ambayo nimeyaleta huko juu, ukaona kwamba unipe nafasi hii, kwa kweli nashukuru na ninamuomba Mwenyezi Mungu anisaidie kwa hilo, kwani nilikuwa nimo katika matayarisho.

Mhe. Spika, katika mswada huu sehemu ya kwanza nikienda kwenye ufafanuzi inasema kwamba kuna taarifa za siri, maana yake ni taarifa zinazothibitishwa na mamlaka kuwa kutoka kwa taaarifa hizo kunaweza

kuathiri ushindani au biashara ama hadhi ya mtu yeyote na hapa imesemwa tu kuathiri.

Sasa ningependa tuongeze kuathiri huko kunaweza kuathiri na athari tunaijua maana yake ni nini, kwa hiyo taarifa hiyo ikitoka basi kama ni mtu ametoa ile taarifa ya siri kuwe na adhabu ambayo itamthibitikia yule mtu ambaye ametoa ile taarifa ya siri.

Nikiendelea mbele sehemu ya pili kuhusu muundo wa Utawala wa Mamlaka, nikienda kwenye kifungu cha 6(1)(a) naomba kunukuu Mhe. Spika.

Kifungu cha 6(1)(a) cha mswada kinaeleza hivi:-

> "(a) Mwenyekiti atateuliwa na Rais.
> (b) Mkurugenzi Mkuu,
> (c) Wajumbe watano watakaoteuliwa na Waziri angalau wajumbe wawili miongoni mwao wawe ni wanawake".

Mhe. Spika, hapa mimi nione kwamba bado wanawake hawajatambuliwa mbali ya hii, maana yake hapa kilichoweka msisitizo angalau. Sasa inaonekana kwamba bado ushiriki wa wanawake kwenye mambo mbali mbali, kwa sababu hapa tumetiliwa angalau. Kwa hivyo, inaonekana kwamba hizi nafasi zote zilizopo hapa zinalengwa zaidi wanaume kuliko wanawake.

Kutokana na hali hiyo, nitoe malalamiko yangu kwamba bado haujaonekana hasa ule ushiriki wa mwanamke katika nafasi hizi.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu kwenye kifungu cha 8 kuhusu Uwezo Maalum wa Mamlaka katika Sekta ya Petroli, kifungu cha 8(1) naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 8(1) cha mswada kinaeleza hivi:-

> "(1) Mafuta:
> - kutoa kupitia na kufuta vibali vya petroli;
> - kusimamia viwango kwa kushauriana na Waziri;
> - kukosa ushindani na ufanisi bora wa uchumi;
> - kudhibiti viwango na ubora kwa kushauriana na *ZBS*".

Ni kweli kwamba kuanzishwa kwa mamlaka hii inaonekana na ndio maana nikampongeza Mhe. Waziri kwa kuona kuwa kuna umuhimu wa kuanzisha mamlaka hii, ili kuwe na usimamizi mzuri wa mambo ambayo yameainishwa humu.

Vile vile kwenye kifungu cha 8(2) ambacho naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 8(2) cha mswada kinaeleza hivi:-

"(2) Maji:
- Kudhibiti ubora wa viwango vya maji kwa kushirikiana na *ZBS*;
- Kusimamia viwango vya malipo, bei, kushauriana na Waziri;
- Kudhibiti ubora wa maji;
- Kutoa matangazo ya usimamizi wa maji na leseni na usambazaji maji".

Mhe. Spika, hapa kidogo ningeomba hii kudhibiti ubora kwa sababu kitu ukikidhibiti kwa tafsiri yangu mimi labda sijui tutumie lugha gani au kuimarisha na kudhibiti inakuwa ni sawa. Kwa hivyo, ningeomba hapa udhibiti kusema kweli sijafahamu. Kwa maana hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika wakati atakapokuja aje kunifafanulia zaidi.

Pia mamlaka hii itakuwa kazi yake ni kupitia mikataba ya manunuzi. Kwa hivyo, ni kweli kwamba lazima kuwe na mikataba ya manunuzi kwa sababu tunaona kuwa mara nyingi mikataba hii ya manunuzi inakuwa haikamiliki, na hivyo kama chombo hichi kitakuwa kinapitia mikataba ya manunuzi. Mhe. Spika, naomba kiwe na uadilifu chombo hichi, ili yale manunuzi yanayofanywa basi yawe na ubora na ile mikataba iwe imekamilika na wala isiwe na mapungufu ambayo yatajitokeza yakaathiri yale mambo ambayo yatanunuliwa kwa kufuata utaratibu wa mikataba.

Mhe. Spika, niseme kwamba kutakuwa na udhibiti kama walivyokwisha kusema wenzangu petroli, yaani kwenye mafuta. Kwa mfano, tunaona hivi sasa ni changamoto iliopo ni kwamba mafuta bado haujakuwepo udhibiti kwa sababu mara kwa mara tunaona mafuta yanapotea kwa visingizio vya wafanyabiashara.

Kwa hivyo, mimi naomba itakapokuwepo mamlaka hii, basi mdhibiti wa nishati hii na serikali kupitia chombo hichi kuwe na udhibiti na ijue hasa pamoja na kufuatilia na kuhakiki kwamba kwenye vile vituo vya biashara ya mafuta kuwe na takwimu, yaani kila wiki kulikuwa na petroli kima hichi na kimeuzwa hichi na kimebakia hichi.

Kwa maana hiyo, kwa wafanyabiashara kuwe na udhibiti kwamba kujulikana ni mafuta kiasi gani wanachukua kwa kila mwezi au wiki na lita ngapi za

mafuta zimetumika na zilizobakia ni ngapi, kwa sababu ya kuondoa hili tatizo la kuwa mafuta yanapotea kwa visingizio tu.

Mhe. Spika, suala hili litadhibiti hata zile bei, kwa sababu wafanyabiashara wanaonekana kuwa wanafanya hivi kwa kuongeza bei kiholela. Kwa mfano, anaweza kuwa na mafuta pengine aliyokuwa nayo mwezi mmoja kabla huko nyuma, lakini baada ya kufanya hili la mafuta yameongezeka bei basi labda akachukua ile *stock* ya zamani na kuuza kwa bei ya sasa ambayo ni kisingizio tu.

Sasa kwa namna mafuta hivi sasa hamna au mafuta haya niliyoyapata hapa na bei hii ninayouza sasa ni kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta, lakini *stock* ile itakuwa ni ile ya zamani na kwa sababu watu si waadilifu na wala hawamuogopi Mwenyezi Mungu.

Kwa kweli kufanya mambo mengine, kwani biashara nayo pia ina uhalali wake hata mbele ya Mwenyezi Mungu, hivyo ni lazima watu wawe waadilifu na waone hii ni dhuluma kwamba unafanya biashara kwa bei ambayo si sahihi na imewekwa.

Kwa hiyo, kuwepo kwa chombo hichi Mhe. Spika naunga mkono sana tena naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani. Mhe. Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, ahsante na nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia mswada huu wa kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Maji na Nishati Zanzibar.

Kwanza nishukuru Wizara kwa kutuletea mswada huu, ili kuona namna ya udhibiti wa viwango bora katika nchi yetu, jambo ambalo kwa muda mrefu lilikuwa likitusumbua na kiliwapelekea tabu wananchi wa nchi hii katika mambo mbali mbali ya nishati katika hali zao.

Mhe. Spika, mimi naomba nichangie mswada huu katika ukurasa wa 351 kifungu cha 18. Kwa kweli hapa naomba litafutwe neno la kutia nguvu juu kuitisha vikao vya dharura. Mara nyingi sheria zetu tunakuwa tunatunga na tunaweka mambo ambayo baadhi ya wahusika huwa wanatumia sheria vibaya. Sasa kifungu hichi kinatoa mamlaka kwa Mwenyekiti na katibu juu ya namna ya kuitisha vikao vya dharura pale ambapo litakapotokea jambo la dharura.
Kwa hivyo, naomba pawe na msisitizo wa neno juu ya vile vikao vya dharura, kwa sababu baadhi ya taasisi Mhe. Spika kama nilivyosema kwamba

wanatumia vifungu hivi vya vikao vya dharura kwa namna ya kujinufaisha wao wenyewe binafsi zaidi pasipo na kuiangalia taasisi katika lile jambo halisi la dharura. Kwa maana hiyo, naomba litafutwe neno la kutilia nguvu katika jambo la dharura ambalo linajitokeza.

Vile vile naomba nichangie kwenye ukurasa wa 353 kifungu cha 24 naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

> Ukurasa wa 353 kifungu cha 24(1) cha mswada kinaeleza hivi:-
>
> > "Mamlaka itatunza hesabu yenyewe na kumbukumbu za mapato na matumizi na ihakikishe fedha zinazopokewa na zinazolipwa na Mamlaka zinawekewa mahesabu ipasavyo".

Mhe. Spika, kuna neno limeandikwa ipasavyo. Sasa neno ipasavyo katika masuala ya mahesabu naomba neno hili liondoke baada ya kuweka neno mahesabu ipasavyo basi lisomeke mahesabu kwa mujibu wa sheria za kimahesabu, kwa sababu ukiweka neno ipasavyo halina nguvu kisheria katika masuala ya udhibiti wa mahesabu.

Nikiendelea katika ukurasa wa 357 sehemu ya sita kuhusu makosa na nidhamu, naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

> Ukurasa wa 357 sehemu ya sita Makosa na Nidhamu kifungu cha 37(1) kinaeleza hivi:-
>
> > "Mtu yeyote, mfanyakazi wa Mamlaka, mjumbe wa Bodi atakayevujisha taarifa au atakayesababisha kuvuja kwa taarifa za Mamlaka au za Bodi bila ya idhini ya Mamlaka atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano na isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo cha miaka isiyopungua mitano na isiyozidi saba au vyote".

Mhe. Spika, kifungu hichi kinanipa mashaka kwa sababu katika taasisi zetu bado huo uaminifu wa bodi haupo na baadhi ya bodi wanakuwa wanafanya mambo ambayo hayastahiki. Sasa mashaka ninayopata mimi Mhe. Spika ni pale ambapo bodi itakwenda kinyume na maadili, watu watatumia fedha za bodi pasipo na utaratibu.

Kwa hivyo, kama mtu anayo imani na taasisi na ameshauona ule ubadhirifu na anataka kuisaidia taasisi kueleza ule ubadhirifu, lakini sitegemei Mhe. Spika kama bodi wenyewe watafanya makosa na halafu wao wenyewe

wakaelezee makosa yao suala hilo haliwezekani, bila ya shaka atatokezea mtu ambaye atayaona makosa na kama anataka kuisaidia taasisi juu ya makosa yaliyotokezea. Kwa maana hiyo, kama tutaweka kifungu hichi cha kuwachukulia hatua na kutaka kulipa faini, Mhe. Spika hapa nadhani kidogo patakuwa na matatizo.

Naomba kutoa mfano Mhe. Spika wa uhalisia kabisa, kuna kikao hapa niliwahi kuchangia juu ya utafiti uliofanywa na mtafiti katika Mamlaka ya Maji kuhusu mashaka ambayo aliyaweka Mamlaka ya Maji kutokana na matatizo ambayo yanatokezea kwa mashine za mamlaka kuungua mara kwa mara. Kwa kweli mtafiti yule aliielezea mamlaka juu ya athari ambazo zinaonekana na mawazo aliyoyatoa alielezea kwamba anayo mashaka na mashine zinazonunuliwa na mamlaka hazina viwango.

Sasa lile wazo amelileta kwetu sisi, ili tuisaidie serikali juu ya kadhia za wafanyakazi ambao wanatumia fedha za serikali kwa kununua bidhaa ambazo hazina viwango na kama leo tutaweka *penalty* hii Mhe. Spika mimi napata mashaka sana.

Kwa maana hiyo, imani yangu kwamba kifungu hichi kitaendelea kuwepo basi huenda taasisi zetu zinaweza kukumbwa na kadhia za ubadhirifu au matendo ambayo hayastahiki, kwa sababu kila mtu ataogopa kukumbwa na faini hii na huku ataona maovu yanaendelea kufanyika.

Mhe. Spika, kifungu hichi naomba bado kitazamwe katika hali nzuri na tuone namna gani au tuelezwe basi ni siri ama taarifa gani zile ambazo hazistahiki kutolewa, lakini kama kuna taarifa za ubadhirifu hazistahiki kutolewa Mhe. Spika naona hapa itakuwa hatukutenda haki na kidogo sheria itakuwa haina nguvu au ime- *base* sehemu moja tu.

Jambo jengine ambalo nataka kulizungumzia liko kwenye ukusara wa 358 kifungu cha 40(3) naomba kunukuu Mhe. Spika.

Ukurasa wa 358 kifungu cha 40(3) kinaeleza hivi:-

> “Pamoja na adhabu zilizoelezwa katika kijifungu cha (1) cha (2) cha kifungu hiki, Mamlaka inaweza kutoa amri nyengine inayoona inafaa”.

Mhe. Spika, ningeomba wazi kwamba hii amri nyengine inayoona inafaa ikaondoshwa kabisa ikawekwa hukumu ambayo itakuwa iko *transparent* Mhe. Spika, kwa sababu kumpa mamlaka mtendaji ya kutoa hukumu ambayo akaona yeye inafaa, Mhe. Spika dunia hii tunaishi watu wengi sana kama vile

kuna watu tunaishi kama ni binadamu, lakini wapo watu ambao wanaishi kwa chuki na husda.

Kwa kweli suala hili mimi napenda nilitolee ushahidi Mhe. Spika, katika Bodi ya Usafiri na Leseni kiliwahi kutokezea kitendo kama hichi kwa historia yao kama hivi kwamba wakatoa hukumu nyengine ambayo inaonekana inafaa.

Sasa kukawa kuna hukumu ya gari ambazo hazifiki mwisho wa *route*, yaani wanakatisha *route* na hukumu yake ilikuwa ni kuzuia gari kwa wiki mbili. Lakini kwa sababu mjumbe wa bodi alipoona kuna mtu ana chuki naye Mhe. Spika kwa kutumia mwanya wa sheria hii basi aliweza kuizuia gari ile kwa muda wa miezi mitatu kwa makusudi ya kumkomoa yule mtu ambaye ana kisasi naye nje ya kawaida. Kwa hiyo, kuiweka sheria bila ya kuwa wazi kabisa Mhe. Spika nahisi haitaleta kitu kizuri.

Nadhani ni vyema tutafute kitu ambacho kitakuwa wazi na ieleze tu kwamba pamoja na adhabu zilizoelezwa kwenye kifungu hichi labda kama ilikuwa ni mwezi mmoja, basi tunaweza kuongeza miezi miwili lakini kuweka adhabu itakayokuwa inafaa. Suala hili Mhe. Spika kidogo naona lina mashaka kwa watu ambao watakuwa si waaminifu katika kutumia sheria hizi.

Baada ya hayo, Mhe. Spika nakushukuru kwa dhati na naunga mkono mswada huu mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia mambo mawili matatu kuhusiana na mswada huu uliopo mbele yetu Mswada wa Kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Maji na Nishati Zanzibar.

Kwanza Mhe. Spika, nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa kuwasilisha mswada huu mbele ya Baraza hili kwa kuanzisha mamlaka hii, mswada ambao tunatarajia baadaye kama utapitishwa utakuwa sheria.

Mhe. Spika, tulikuwa na kilio cha muda mrefu juu ya namna ya kudhibiti hasa masuala haya ya mafuta, kama tunavyofahamu kwamba mafuta ndio nyenzo ya kila kitu na yanapoadimika mafuta basi nchi yetu tunaona jinsi inavyohamanika.

Lakini hata upandaji wake wa bidhaa hii basi huwa unakaribisha mambo mengi kupanda, mifumko ya bei na kila wakati inaonekana kwamba hakuna chombo madhubuti ambacho kina-*control* bei hususan za nishati. Ilikuwa mara nyingi *ZRB* ina-*control* bei hiyo kwa kushirikiana na waletaji wa mafuta

na mambo mengine, lakini wao tulichokuwa tukijua wana-*control* ni kwa ajili ya kudhibiti kodi. Kama tunavyofahamu kuwa serikali huwa inakusanya kodi kubwa, na moja kati ya kianzio chake kikubwa cha mapato ya serikali kinatokana na kodi ya mafuta.

Kwa hivyo Mhe. Spika, kwa kuanzisha chombo hiki tayari tutakuwa na chombo ambacho sasa ni mas-uul juu ya masuala haya. Lakini pamoja na kuanzishwa chombo hiki na kuanzisha sheria ya kusimamia chombo hiki kwa kweli Mhe. Spika sheria hii ni muhimu na ina mambo mengi sana.

Mhe. Waziri hatujui hali yake ilikuwaje lakini kwa uzito wa sheria hii na mambo yaliyokuwemo humu nadhani Mhe. Waziri ilikuwa atutayarishie mafunzo, ili aweze kutuelimisha zaidi juu ya jambo hili.

Kwa kweli humu mna mambo mengi ya kitaalamu na kama wenzangu waliotangulia kwamba, sisi ni watunga sheria lakini sio wanasheria, sasa sijui kama hakuona umuhimu wa kufanya jambo hilo.

Lakini mimi kwa upande wangu Mhe. Spika naona kulikuwa kuna haja ya kutoa mafunzo kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kabla ya kufanya kazi hii ya kupitisha au kutunga sheria hii. Sasa pamoja na kwamba hatukupata mafunzo tumejaribu kutumia uzoefu tuliokuwa nao na muda tulioupata katika masuala mazima ya kutunga sheria.

Mhe. Spika, tumekuwa na malalamiko mengi, vyombo vingi, taratibu nyingi juu ya suala zima la mafuta, mambo ambayo yamekuwa yakileta mzozo. Kwa mfano, tumeshuhudia mafuta yakiuzwa baharini meli kwa meli, yaani wenyewe wanaita *ship to ship,* na baadaye serikali ikapiga marufuku biashara hiyo kutokana na magendo.

Vile vile tumekuwa tukishuhudia bidhaa hii ya mafuta ikiwa na viwango tofauti kama vile ukienda kwenye kampuni hii mafuta yake yako hivi, yaani unayakuta mafuta ya *petrol* utafikiri ni *diesel* au mafuta ya taa na yamekuwa na rangi tofauti na kumekuwa na mkanganyiko mwingi. Kwa hivyo, hata sisi ambao wenye vyombo vinavyotumia mafuta haya tumekuwa na malalamiko mengi, kama vile mafuta yana maji au unakuta mafuta ya *diesel* yamechanganywa na mafuta ya taa na kumekuwa na malalamiko mengi.

Sasa kuanzishwa kwa vyombo au sheria hii tunavyoamini kutaweza kusaidia kuondosha haya matatizo yaliopo ikiwa ni pamoja na tatizo la upandaji wa bei za mara kwa mara.

Mhe. Spika, mswada huu umeeleza mambo mengi, kama vile umeeleza juu ya muundo na utawala wa mamlaka, pia kuanzishwa kwenyewe kwa mamlaka kwa mujibu wa kifungu cha kwanza, vile vile imeeleza namna ya Mkurugenzi Mkuu na upatikanaji wake na sifa zilizopo.

Mhe. Spika, Mkurugenzi wa Mamlaka amewekewa sifa nyingi ambazo sifa hizi zitamuwezesha Mhe. Rais kumteua. Lakini Mhe. Spika, kwa mujibu wa sheria hii sifa hizi zimekuwa ni nyingi mno, ambapo mimi binafsi nimekuwa na wasi wasi kwamba tunaweza tukampata Mkurugenzi ambaye pengine halingani kabisa na sifa za jambo lenyewe.

Kwa mfano, kifungu cha 4(3) naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 4(3) (b) kinaeleza hivi:-

> "Mkurugenzi Mkuu atakuwa na sifa zifuatazo:
>
> (b) Awe na taaluma ya shahada ya pili au kiwango kinacholingana nacho kutoka katika chuo kikuu kinachotambulika na hapo sina tatizo, lakini katika fani ya mafuta na hapo ni sawa au maji au umeme au uongozi au biashara au uhandisi au sheria au fani nyengine zinazofanana na hizo na uzoefu usiopungua miaka mitano".

Mhe. Spika, utaona pamekuwa na wigo mpana juu ya kumpata Mkurugenzi jambo ambalo linaweza kuhatarisha kumpata Mkurugenzi ambaye si wa fani hii ambayo hasa imekusudiwa. Kwa hivyo, nadhani twende katika maeneo ambayo ni *specific* yanahusika na chombo chenyewe, ili tumpate Mkurugenzi ambaye anaweza kukiongoza chombo hichi bila ya kuwa na matatizo.

Kwa mfano, suala la biashara, sheria haya tukaweza kuyapunguza, yaani mtu mwenyewe shahada ya pili ya sheria akawa Mkurugenzi wa mamlaka hii kwa kweli naona mambo haya yanaweza kupunguzia chombo hichi uwezo wa yale mambo ambayo tunayatarajia.

Mhe. Spika, kifungu cha 8 kinazungumzia uwezo maalumu wa Mamlaka ambapo kimegawanya maeneo makubwa matatu. Eneo la kwanza linazungumzia mafuta kutoa, kupikia na kufuta vibali (petrol). Hapo hata sielewi wamekusudia kitu gani. Mhe. Waziri hebu utakapokuja kutoa ufafanuzi tufafanulie eneo hili limekusudiwa vipi.

Lakini ukiangalia pia katika kufungu cha (8) Sehemu ya Pili inayozungumzia masuala ya maji. Inazungumzia juu ya kusimamia viwango, malipo, bei kwa

kushirikiana na Waziri. Bei hizi za maji, kwa sababu tunajua sasa hivi Mamlaka ya Maji inatoza kodi kwa ajili ya huduma ya maji. Je, viwango hivi vya bei vitapangwa na Tasisi hii, au itakuwa ina *control* au vipi. Hapo tunataka tuweze kujua. Lakini *statement* kama hii kwenye umeme haipo.

Lakini kama tunataka ku-*control* bei zinazotokana na ada ya maji basi na hata kwenye umeme nako kunahitajika. Kwa sababu kumekuwa na kilio kikubwa kwa wananchi wetu na hata sisi Wajumbe wa Baraza juu ya upandaji wa bei za umeme kiholela ambazo inapangwa na ZECO. Sasa kama chombo hiki kinakusudia ku-*control* kwa kushauriana na Mhe. Waziri, juu ya malipo ya bei ya maji, basi hata kwenye malipo ya bei ya umeme pia yanahitajika. Kwa hivyo hili nalo sheria hii nadhani ilikuwa na haja ya kuzingatia jambo hilo.

Mhe. Spika, eneo jengine kifungu cha 10, kinasema Leseni, Kwamba Mamlaka itatoa leseni kwa watoahuduma na ikaelezea kwa mpangilio ufuatao, pia ikagawa kwenye makundi matatu. Kwenye nishati ya umeme itatoa leseni ya:
(a) Uzalishaji
(b) Usambazaji
(c) Uuzaji
(d) Upitishaji

Hapa panahitaji tupate kidogo elimu. Tunapozungumzia uzalishaji, umeme wetu sasa hivi uzalishaji wake unazalishwa Tanzania Bara. Unakuja hapa ZECO inapokea, inasambaza. Tunataka ufafanuzi kwa Mhe. Waziri, uzalishaji huu ni upi. Au tunakusudia tutakapokuwa na vyombo vyengine ambavyo vitazalisha, tunakusudia uzalishaji wa vyombo hivyo vyengine kwa mujibu wa sheria. Hebu tupate ufafanuzi, tunapozungumzia neno uzalishaji tunakusudia nini.

Hili neno upitishaji nalo linakusudia ni kitu gani. Ndio maana Mhe. Spika, maelezo yangu ya awali nilisema kwamba kulikuwa kunahitaji semina. Kwa sababu haya mambo yanahitaji maelekezo. Tusije tukapitisha kitu ambacho sisi hatukielewi, baadae tukaja tukapata matatizo. Kwa sababu hii tayari ni sheria, sheria hii inasimamia mambo makubwa. Kwa hiyo tulikuwa tunahitaji hasa tupate mafunzo ili tujue kitu gani tunakipitisha hapa.

Sehemu ya Pili inazungumzia kwenye Nishati ya Mafuta. Kwenye Nishati ya Mafuta itatoe leseni ya usambazaji, uagizaji, usambazaji wa jumla na rejareja na mambo mengine yanayohusiana na nishati hiyo.

Sisi tunavyofahamu Mhe. Spika, hapa tuna Makampuni ya Mafuta ambayo makampuni yale ama yanatoa mafuta yao kutoka Tanzania Bara au yanatoa

Kenya ama wakati mwengine yanapata mafuta ya baharini yanachukua kwenye mameli. Hebu tupate ufafanuzi juu ya jambo hili. Na huu usambazaji unaozungumziwa hapa unakusudiwaje, ni zile Kampuni zinazoingiza mafuta *Deport*, zitapewa leseni za kusambaza kwenye vituo kwa kuwauzia wenye vituo. Au usambazaji huu unakusudiwa vile vituo vyenyewe zinavyowauzia wenye vyombo vya usafiri. Kwa sababu hizi *times* zinaweza zikatumika kila wakati katika kila eneo. Tunapozungumzia Mamlaka itatoa leseni, kwa sababu sasa hivi leseni za kwenye vituo vya mafuta zinatolewa na ZRB. Sasa je, leseni zile ndio zitatolewa na mamlaka hii au vipi.

Hebu Mhe. Waziri uje utupe ufafanuzi wa kina juu ya jambo hili na hii sio inayosema usambazaji wa jumla na rejareja. Usambazaji wa jumla ukoje, na usambazaji wa rejareja ukoje. Lakini hali kadhalika kwenye Sehemu ya Tatu kwenye huduma ya maji vile vile. Tunazungumzia usambazaji, mtatoa leseni ya usambazaji. Hapa chombo kinachotoa huduma ya kusambaza maji ni Mamlaka ya Maji kwa mujibu wa sheria, ndiyo inayosambaza maji kwa wananchi.

Katika visiwa vyetu sasa hivi kumekuwa na visima vidogo vidogo ambavyo wananchi wenyewe wamejitolea wanachimba na wanapata nafasi ya kuwasambazia wananchi, iwe kwa malipo madogo madogo au kwa bure. Lakini na wao pia wanasambaza maji. Hii inatokana na uhaba wa maji uliokuwepo katika visiwa vyetu. Wanazimika wananchi kuchimba visima vidogo vidogo.

Sasa hapa kunazungumzia suala la usambazaji. Lakini ukuzaji wa nishati ya maji safi na salama. Hii nayo mtu itabidi apewe leseni juu ukuzaji wa nishati ya maji safi na salama, itolewe leseni na kwa wateja wapya watoa huduma ya umma au sekta binafsi.

Mhe. Spika, kwa kweli hii sheria imetuchanganya sana. Kuna hatari ya kuweza kupitisha sheria hii halafu baadaye wananchi wakawa wanailalamikia. Kwa sababu haikupata ufafanuzi wa wazi wa kutosha, hatukupata muda wa kujiridhisha juu ya vifungu hivi ambavyo vimetolewa. Zaidi Mhe. Spika, tukizingatia kwamba mambo haya ni ya huduma kwa wananchi. Inahitaji tuwe makini Waheshimiwa Wajumbe, wakati tunapopitisha sheria hii tuwe makini juu ya upitishaji wa sheria hii. Vyenginevyo huko mbele tunaweza kuja kupokea malalamiko mengi.

Mhe. Spika, mimi nimeshakuwa mzoefu juu ya mambo haya ya sheria. Wakati mwengine tunapitisha sheria hapa kijuu juu ambayo inakuwa imefunikwa funikwa. Lakini baada ya siku mbili tatu tunaanza kuona matatizo

yanajitokeza, tunawambia wenzetu si mmepitisha sheria hii, sheria iko hivi na hivi. Sasa sheria hii imekuja imebanabana.

Mhe. Spika, mimi ningeshauri watunga sheria wenzangu, sheria hii ili tuweze kuipitisha basi Mhe. Waziri atufanyie semina, hili niwashauri wenzangu. Kwa sababu sheria hii ina mambo mengi yanayowagusa watu. Inagusa huduma za maji ambayo ni matatizo, inagusa huduma za umeme, inagusa huduma za mafuta. Tunahitaji mafunzo ya kutosha ili tuielewe vya kutosha, vyenginevyo tunaweza tukakipitisha kitu ambacho hatukielewi na hatimaye tukasababisha manung'uniko na migogoro mingi katika jamii ambayo sisi ndio viongozi wa jamii hiyo. Na kama jambo ambalo sisi wenyewe tunaolipitisha hatulielewi sidhani kama wananchi waliokuwepo kule nje watakuwa wanalielewa.

Kwa hivyo hapa tufanye kazi ile ya kutunga sheria tunayoielewa, sio kupitisha sheria. Nimuombe sana Mhe. Waziri, atutayarishie mafunzo juu ya sheria hii, ni sheria muhimu na ni sheria inayohusu huduma kwa wananchi wetu, ili tuweze kumpitishia.

Mhe. Spika, kuna sehemu hapa kifungu cha 21 cha sheria hii kinazungumzia maslahi. Ambapo kinasema kwamba Wajumbe wa Bodi watalipwa maslahi na posho kama inavyopendekezwa na Bodi na kukubaliwa na Waziri anayeshughulikia masuala ya fedha. Hapa ndio kwenye tatizo. Kwa sababu mamlaka hii itakuwa na bodi kama ilivyotajwa au kama ilivyoundwa kwa mujibu wa sheria hii kwamba kutakuwa na bodi. Bodi hizo zinakuwa zinalipwa maslahi na maposho mbali mbali. Lakini penye matatizo hapa kwamba Waziri anayeshughulikia na masuala ya fedha, mara nyingi bodi hizi ambazo zinaundwa katika Mamlaka basi masuala yao ya madukhuli yao huwa yanapangwa na Waziri anayesimamia jambo lile.

Sasa naona sheria hii inamsukumia Waziri wa Fedha anayashughulikia masuala ya fedha. Hapa nimekuwa na wasi wasi, kwa nini bodi hii ipo chini ya Waziri anayeshughulikia masuala haya ya Nishati lakini madukhuli yao yapangwa na Waziri wa Fedha. Hebu Mhe. Waziri utakapokuja kutoa ufafanuzi utueleze imekuwaje mamlaka hayo yakatoka huku yakapelekwa kwenye taasisi nyengine.

Mhe. Spika: Haya una dakika tatu kumalizia hotuba yako.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Namalizia Mhe. Spika.

Halafu kifungu cha 22 kinazungumzia masuala ya fedha, kimeeleza fedha za Mamlaka zinajumuisha (a) Fedha zinazotolewa na serikali. Hapo sina wasi wasi ambazo zinapitishwa hapa na Baraza la Wawakilishi. Lakini kuna

kifungu cha aina hiyo (d) kinachosema Fedha zinazotolewa na serikali tena kwa ajili ya mamlaka kwa muda ulioainishwa kama itakavyokubaliwa na serikali. Sasa naona kama ni *repetition*. Kwa sababu tunaweza kusema fedha zinazotolewa na serikali ndio fedha hizo hizo zinazotolewa kwa ajili ya mamlaka na sio kwa ajili ya mambo mengine, imejirudia.

Halafu kuna kifungu cha (f) kinasema fedha ambayo mamlaka imelipwa kama ada. Hii sina tatizo kama ada chini ya sheria hii. Lakini haya maeneo mawili naona kama yamejirudia rudia.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa katika kifungu cha 31 kuna Baraza la Kuwawakilisha Wateja lakini Kamati imebadilisha, imezungumzia watumiaji. Hiki ni chombo muhimu sana lakini naona kwenye sheria hii hakikupewa uzito unaostahili. Ningehitaji kupewa uzito unaostahili katika sheria hii, lakini kama vile kimezungumzwa zungumzwa tu.

Mhe. Spika, muda wangu umekwisha lakini kama utangulizi wangu ulivyotangulia kwamba sheria hii ni muhimu, ilikuwa inahitaji mafunzo kwa waheshimiwa wajumbe, waielewe. Kwa kweli mafunzo hatuna, hatujui na hali ya kuwa inagusa masuali mengi yanayohusiana na ada na bei na mambo mengine.

Mimi nimekuwa nina wasi wasi kwani inaweza ikatuletea matatizo baadaye. Mimi nadhani waheshimiwa wajumbe siwashawishi, lakini pengine wenzangu wameielewa ipasavyo. Lakini ni vyema Mhe. Waziri akatuandalia semina tukapata nafasi ya kumuuliza kifungu kwa kifungu, tukaielewa ili kuweza kuipitisha. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa kuweza kunipatia nafasi hii kuweza kuchangia Mswada huu wa Sheria ambayo imewagusa jamii moja kwa moja.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako niruhusu nisome madhumuni, na sababu nitasoma kidogo hapo. Madhumuni ya Mswada huu ni kuanzisha sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati. Kuwepo kwa sheria hii ni utekelezaji wa sera ya nishati ya mwaka 2009, ambayo pamoja na mambo mengine inayoeleza haja ya kuwepo chombo cha udhibiti.

Mhe. Spika, nimpongeze kwanza Mhe. Waziri, kwa kuuleta Mswada huu. Ninalojiuliza Mhe. Spika, ni kweli huko nyuma tulikuwa na sera na tulikuwa tunazijadili. Lakini sasa hivi sera hazipitii kwenye Baraza la Wawakilishi zikajadiliwa, zinabakia mawizarani. Wasi wasi wangu Mhe. Spika, niungane mkono na wale wenzangu ambao wamesema kwamba hii sheria na kwa

sababu inamgusa mwananchi moja kwa moja kwa sehemu zetu, maji na nishati ni sheria muhimu sana kwa nchi yetu.

Wasi wasi wangu ni kwamba je, haya Mamlaka kweli yataweza, huo ndio wasi wasi wangu. Kwa sababu sasa hivi tuna matatizo kwa upande wa nishati na kwa upande wa maji. Mimi nitachangia kwa sababu ndio tulivyosema kwamba sera ndio muhimu, tungepata hizi sera ndio tungejua nini tunachangia. Lakini ni Mswada tu umeletwa hapa kifungu hiki na kifungu hiki, hatujui Mswada ule umeelekeza nini na nini.

Mhe. Spika, nishati tu peke yake ina matatizo, maji ndio hayo. Mimi nina wasi wasi kwamba sasa hivi tunatunga sheria ya mamlaka. Huko nyuma kuna baadhi ya wananchi wanadaiwa fedha za maji kulipia wakati watu hawajayaona maji. Naiomba Wizara Mhe. Spika, ikae izingatie na itafakari, kutunga sheria sisi ni kazi yetu, lakini utekelezaji wake ndio matatizo. Sheria tunazitunga nyingi sana Mhe. Spika, na nyengine zinajirudia zile kwa zile lakini nitizamie kwenye utekelezaji.

Mhe. Spika, mimi nimuunge mkono mjumbe aliyekaa kitako sasa hivi. Masuala kama haya ya sheria tufanyiwe semina na semina hiyo sio wafanyiwe wenye viti tu. Maana siku hizi umeingia mtindo wa kufanyiwa semina wenye viti wakaalikwa. Si haki kwa sababu mimi nikija hapa kama mwenyekiti wa uwezeshaji nakuja kuchangia mimi mwenyekiti. Sipati na mimi wakati wa kuchagua wajumbe wangu wa kamati yangu nikaweza kuwaeleza mambo ya mswada au ya kitu chochote ambacho nimekwenda mimi mwenyekiti.

Mhe. Spika, huu Mswada nimuunge mkono mwenzangu tupate semina. Huu si mswada wa kuchezea ni mswada ambao unamgusa mwananchi moja kwa moja, nishati na maji na mambo mengine yanayoambatana na hayo.

Mhe. Spika, mimi huwa nashangaa, mwenzangu hapa aliyekaa kitako ameeleza mambo mengine moja baada ya moja, mimi nitachangia kwa jumla.
Mhe. Spika, tatizo letu usimamizi wetu ni mbaya wa majukumu ambayo tunapewa. Tutachagua wakurugenzi, tutachagua mameneja, tuwatwike ya dhamana lakini matokeo yake dhamana ile haifanyi kazi ipasavyo. Narudia tena kwamba mamlaka, tukishakutoa kitu Mamlaka panataka usimamizi wa hali ya juu. Niseme tu kwamba Mswada huu ni mzuri tena mzuri sana ili kuwaondolea matatizo ya kijamii watu wetu wa Zanzibar. Mimi sifikiri kwamba nishati tuna uwezo wa kuzalisha nishati, sifikiri, kweli tunao uwezo wa kuzalisha nishati siye hapa. Sifikiri.

Maji Mhe. Spika, hivi sasa watu wameshaota kipara sio cha kupewa na Mwenyezi Mungu ni kipara cha ndoo za maji. Si kipara cha kupewa na Mwenyezi Mungu kwamba anaakili huyu lakini vipara kwa kutafuta maji kila mtu katika sehemu yake.

Mhe. Spika, mimi nilikuja nikauliza suala hapa kwamba tunataka maendeleo katika nchi yetu, na wale ambao tunawapa dhamana ya kutuletea maendeleo kama ni ma – *contractor* manani, lakini waangalie ile sehemu waliyowakuta watu leo mpaka hivi sasa Mazizini pale na hii ni mara nyingi kuliulizia hili suala. Wachina waliokuwepo pale wamekata maji yote, wananchi sasa hivi wanapata tatu na nyengine wamezichukua wamezi *block* sijui wenyewe ndio mnaita nini ya kwamba yasitoke hasa. Hili nimelizungumza si mara moja na masuala nimeuliza si mara tatu.

Mhe. Spika, jana nimemwambia Mhe. Naibu Waziri kwa sababu jana Mhe. Waziri sikumuona. Nikamwambia *Wallahi Laadhimu* naapa kwa Mwenyezi Mungu bajeti ya maji na nishati itakuwa tabu sana kwangu. Kwa sababu ni kitu ambacho kinamgusa kila mwananchi, na sisi tupo hapa kwa ajili ya kutetea maslahi ya wananchi wetu. Leo hapa kulikuwa na mradi mkubwa wa maji, sijui umeishia wapi ule, wengine wamepata, wengine hawakupata.

Mhe. Spika, kuna haya ya serikali pamoja na Mswada huu wakafanya utafiti wa hali ya juu kwa sababu huu mji umeshajengwa sio ule wa zamani wa watu laki tatu, sasa hivi tuko milioni moja na laki tatu. Nyumba nyengine zimepitia kwenye *main pipe* za maji. Kwa hivyo naomba wizara hii na kwa sababu hii wizara ina watendaji wengi sana tena wasomi, kufanya utafiti maalum wa sehemu baada ya sehemu ili watu wajue maji wanayapata wapi.

Mhe. Spika, lakini nisiwe mwizi wa fadhila nichukue nafasi hii adhimu kabisa kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zake ambazo amezifanya kupitia kwa Wizara hii pamoja na waziri wake kuhakikisha kwamba tunaondokana na mgao wa umeme. Niipongeze sana serikali tena sana.

Mhe. Spika, imani yangu tusifanye maskhara fedha nyingi sana serikali imetoa kwa ajili ya kufanikisha umeme kwa ajili ya Zanzibar, Unguja na Pemba. Maana juzi jamaa zangu walinitania Mhe. Spika, walisema mnachoooo! Maana sisi tulivyokuwa hatuna umeme kule Pemba mlituona bwiiiipwi! Sasa zamu yenuuuuu! Nawambia na sisi hatuna tena zamu sasa, umeme tutakuwa nao wa uhakika.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo niseme kwamba nimuombe Mhe. Waziri na watendaji wake kwamba tuwe makini na sheria hii kwa kuisimamia

ipasavyo lakini pamoja na kwamba tunataka kuipitisha namuomba bado Mhe. Waziri atupe semina ya Sera inavyosema haidhuru tunakwenda kinyume maana ilikuwa upate mafunzo kwanza ujue namna ya kuchangia halafu baadae ndio upitishe semina. Lakini kwa vile lengo na madhumuni ya sheria hii ni nzuri Mhe. Waziri utupe semina kwa sababu huko tukirudi tutaulizwa na wale tunaowawakilisha humu, sio tusimamie hapa tuseme tu kifungu kimoja, kifungu cha pili tunazungumza kwa kuona huu mswada lakini mimi *wallahi* sifahamu sera inasemaje.

Kwa hivyo baada ya kusema hayo Mheshimiwa nichukue tena nafasi hii niishukuru sana serikali kwa jinsi ilivyopigana kuhakikisha kwamba umeme sasa hauna mgao. Lakini naomba Mhe. Spika, kupitia kwako na Baraza lako Tukufu tuwe macho na watu ambao hawaitakii mema serikali hii, kwa sababu kuna watu kwa makusudi wanafanya kwamba ionekane serikali hii haikufanya kitu, lakini serikali hii imefanya mengi ambayo tunayaona bila ya tochi, mengi yamefanyika Mhe. Spika.

Sasa suala hili la umeme ni suala nyeti maana ni maficho ya kila mtu, wengine wezi ndio wanatafuta sababu hapo hakuna umeme mtu afanye anavyotaka. Watu wengine wenye mambo yao ambayo si ya kawaida wanangoja umeme ukizimwa wafanye wanayotaka. Kwa hivyo ninakuomba Mhe. Waziri umeme uendelee kama mlivyotuonesha kwamba sasa hivi hakuna tena mgao wa umeme. Nasema naitakia kila la kheri serikali yetu ambayo imefanya juhudi kubwa sana kwa umeme.

Baada ya kusema hayo sijui niunge mkono, maana naona haya maelezo, naunga mkono mswada.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kupata nafasi hii kuchangia mswada huu wa sheria ya kuanzisha mamlaka ya udhibiti wa huduma ya maji na nishati Zanzibar. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu *subhana llahu wataala* alionijaalia mchana huu kuwa katika hali ya uzima na afya inaruhusu.

Mhe. Spika, pili nitakuwa mchache wa fadhila kama sijakupongeza wewe uliyenipa fursa hii kuchangia mswada huu. Lakini vile vile nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Ardhi Makaazi, Maji na Nishati kwa kuleta mswada huu muhimu ambao hapa tunapozungumza ni mahali pake.

Mhe. Spika, tukiangalia maji ni muhimu sana kwa uhai wa viumbe vilivyo hai, Mhe. Spika, kwa kweli Kamati yetu ya Mawasiliano na Ujenzi imewasilisha hotuba yake asubuhi hii, sisi tumepata kujifunza mengi katika hotuba hiyo. Lakini vile vile tumepata fursa kwenda kutembea kwa wenzetu

Arusha, Kamati yetu tulijifunza mengi yanayohusiana na mambo ya maji. Kwa kweli wenzetu wa Arusha wamejipanga vizuri namna hata mambo ya udhibiti jinsi walivyojipanga, lakini na sisi tuige kwani jambo jema ukiliiga basi ni vyema.

Mhe. Spika, mamlaka kama mamlaka lazima tuipe uhuru wa kufanya shughuli zake kama mamlaka hapo tukiipa uhuru basi mambo mengi yatakwenda vizuri, lakini tusitaje tu Mamlaka ikawa haina uhuru wowote. Tunaiomba serikali mamlaka hii inayoundwa au inayonzishwa iipe uhuru wa kufanya kazi zake kwa ufasaha kabisa.

Mhe. Spika, tunazungumzia maji na nishati ni kweli kumekuwa na changamoto nyingi kuhusu maji na tunasema udhibiti, lakini mimi napata mshangao mkubwa unataka kudhibiti kitu ambacho hakipo. Ili tupate kudhibiti basi kile kitu kiwepo lakini leo tunasema tunadhibiti lakini ukiangalia maji hayapatikani tunadhibiti nini.

Mhe. Spika, ni ukweli usiofichika Zanzibar hii huko tunakotoka ilikuwa haina tatizo la maji, lakini sasa ukiangalia kila pembe kuna tatizo la maji. Mhe. Spika, kama kuna udhibiti basi kwanza tuviangalie vyanzo vya maji viko vipi, tukiangalia vyanzo vyetu vya maji kuna changamoto nyingi sana. Vyanzo vya maji watu wanajenga kiholelaholela ambapo ndio sehemu zinazopata maji kwa hivyo tunavyojenga kiholela hatuwezi tukapata maji kutokana na vyanzo vyetu vya maji.

Halafu Mhe. Spika, kwa kweli na matumizi mabaya ya maji yanachangia maji kutopatikana kwa ufanisi kwa wananchi wengine. Ukiangalia wenzetu wa Arusha kule mtu anakwenda kulipia vifaa vyote anavyotaka kuungiwa maji tofauti na petu hapa Zanzibar. Hapa Zanzibar mtu anakwenda na vifaa vyake mwenyewe. Lakini wanaloliangalia wenzetu Arusha ni *quality* za zile paipu wenyewe za kuungia maji, lakini hapa mtu anakwenda kuungiwa maji mpira wenyewe hauko katika *quality* akiunga siku ya pili unapasuka. Na ukipasuka basi inaweza kuchukua muda wa siku sita maji yanapotea tu, sasa niwambie, Mhe. Spika, na Mhe. Waziri anayehusika, wenzetu kule wamejipanga vizuri wana gari yao ina mawasiliano kila kitu katika pembe zote wanawasiliana kuangalia kuna tatizo gani, sisi nina imani hatujafikia huko. Lakini kwa sababu tumekuwa tunajifunza mamlaka ya maji ndio waliotupeleka wameona vitu kama vile tunawaomba wafikie malengo kama hayo ili tupate ufanisi mzuri wa kutosha.

Mhe. Spika, mambo haya ya maji yanategemeana sana na umeme kama hakuna umeme maji yanakuwa pungufu kupatikana. Sasa mambo haya yapo katika Wizara moja tunaomba umeme nao hapa tulipofikia tumeshaambiwa

kutakuwa na umeme wa uhakika usizimike mara kwa mara. Kwa hivyo tukipata mambo haya yakiwa pamoja basi maji yatapatikana.

Lakini vile vile tuangalie watu na upotevu huu wa maji unaotokea ni watu wenye uwezo kujiungia maji kiholela nao mtu ana *tank* mbili za maji ana *tank* ya juu na ya chini, sasa katika njia inayopita maji wanyonge hawapati mpaka yeye ajaze ndio aruhusu sasa kupata watu wa chini hili ni tatizo, Mhe. Spika, hili liangaliwe kwa uangalifu au kutengwe muda maalum watu wenye ma-*tank* aina hiyo wajaze ma-*tank* yao kwa muda maalum tena usiku sana lakini wananchi walio wengi wapewe uhuru wa kutosha katika upatikanaji wa maji.

Mhe. Spika, Zanzibar hii imeshamiri biashara ya maji, biashara hii imeshamiri kwa upungufu wa maji kwa sababu kama hakuna upungufu wa maji mtu asingenunua dumu la maji ingekuwa anayapata lakini maji tunayonunua katika madumu hayana usalama na uhakika. Mtu kwa kukuza biashara yake tu apate matumizi basi anaweza kutuchotea hata maji yaliyokuwa si safi akampa mtu akatumia na hatima yake kukaribisha maradhi aliyokuwa hakuyategemea. Lakini kama tutaweka mitandao mizuri basi kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na juhudi zetu tunazozifanya maji yatapatikana kwa wingi.

Mhe. Spika, kumekuwa na uungwaji kiholela wa maji, kuna mafundi wa mitaani mtu akiwa na paipu zake anakwenda kuungiwa tu hili nalo ni tatizo, kwa sababu mpira unatobolewa sehemu ambayo hazistahili kutobolewa, inakuwa ina-*effect* katika yale maji hayapati njia yake ya kufika yanakokusudiwa. Kwa hivyo iangalie sana hapa Wizara husika hii. Mhe. hizi *water pump* zinachangia hizi wengi Zanzibar hii

Mhe. Spika: Mheshimiwa changia zaidi mamlaka hii iliyotajwa hapa na sio mamlaka ya maji. Mamlaka hii inayotengenezewa sheria hii. Hiyo unayozungumza iko zaidi kwenye Mamlaka ya Maji ZAWA.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. ndio kama ilivyoelezwa katika kifungu hiki cha 8.2 naomba ninukuu kwa ruhusa yako, kudhibiti ubora wa viwango vya maji kwa kushauriana na ZBC, kusimamia viwango, malipo, bei kwa kushauriana na Waziri, kudhibiti na ubora wa maji, kutoa matangazo ya usambazaji wa maji na leseni za usambazaji wa maji.

Mhe. Mswada huu ni mzuri kama ulivyoelezwa na unawagusa jamii, kwa hivyo mimi naomba kama walivyozungumzia wenzangu basi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwapatia semina wakapata uelewa zaidi ni bora kuliko kufanya jambo tulilokuwa hatulijui, baadae kupitisha mswada ikawa ni kero kwa wananchi, baada ya siku mbili tatu ukafanyiwa marekebisho haiingii maanani.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi niseme tu kwa sababu Kamati yetu imepitia vya kutosha imetoa ushauri niunge mkono hoja na mswada huu ni mzuri na nimpongeze Waziri husika kwa mara nyengine.

Mhe. Spika, naunga mkono mia kwa mia.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuchangia mawili matatu katika haya pamoja na kwamba ulikuwa umenisahau lakini najua kusahau kwako kunatokana na kwamba kiti changu kimesogezwa sana huku, sasa imekuwa siku hizi hukioni kidogo.

Mhe. Spika, na mimi nianze kwa kutoa mkono wa pole hususan kwa misiba ambayo imetokezea katika nchi yetu ndani ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla na tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu wote waliopatwa na matatizo hayo Mungu awape moyo wa subira.

Baada ya hapo Mhe. Spika, mimi niseme tu kwamba kwa niaba yangu mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa jimbo ninaloliongoza Jimbo la Kikwajuni tunaunga mkono mswada huu pamoja na kwamba umetengenezwa kitaalamu zaidi, na ndio maana wenzangu waliokuwa wamenitangulia wakaomba kwamba hawa wataalamu waje watusaidie uwezo zaidi ili tuweze kuufahamu vizuri zaidi mswada huu na kuweza kutoa maamuzi yaliyo sahihi kwa manufaa ya wazanzibari wote kwa ujumla.

Mhe. Spika, nianze vile vile kwa dibaji ambayo itakuwa inatanguliza kusema kwamba nimejaribu kuupitia mswada huu na nimeona maeneo mengi ambayo yamezungumzwa lakini pia nimeshindwa kuona eneo ambalo kuna utaratibu mzima katika sheria hii inayoelezea juu ya wale watu ambao wamechimba visima na kuweka katika nyumba zao kwa manufaa yao ambapo hata ile mitandao ya ZAWA haikuhusika na matumizi hayo. Kitu hicho sijakiona na hii ni sheria ambayo tunataka kuipitisha kwa matumizi ya nchi yetu.

Lakini pia katika mswada huu wa sheria sikuona vile vile utaratibu gani ambao utatumika katika uchimbaji ovyo wa visima ambao hauzingatii yale matakwa na uhalisia sahihi unaotakikana katika uchimbaji wa visima katika nchi yetu. Napenda kuwakumbusha wazanzibari kwamba Zanzibar ni visiwa, visiwa ambavyo kwa ukubwa wake haulingani na ongezeko la visima ambavyo vinaendelea kuchimbwa siku hadi siku katika utaratibu ambao haueleweki. Ningeliomba hili nalo tulizingatie ili tuweze kujua tunachokifanya tunafanya kwa kuona kwamba hili eneo siku moja lisije ikatokezea kama yaliyotokezea pale mshelishelini pale Jan'gombe.

Mhe. Spika, kwa kuendelea zaidi nianze na ukurasa wa 344 katika muundo na utawala wa mamlaka sehemu ya pili, hapa kuna maelekezo ambayo yanasemwa kwamba muundo na utawala wa mamlaka inaanzishwa mamlaka inayojulikana kama mamlaka ya udhibiti wa huduma ya maji na nishati kwa Zanzibar. Mamlaka itakuwa ni chombo kitakachojitegemea cha kudumu chenye muhuri wake na kutumia jina lake na kitakuwa na uwezo wa kupata, kutwaa, au kutoa mali inayoimiliki inayohamishika au isiyohamishika.

Lakini Mhe. Spika, nikija katika ukurasa wa 345 huku na katika kifungu cha sita naona vile vile kutakuwa kuna bodi ya wakurugenzi ambayo itakuwa na wajumbe saba, wajumbe ambao watatumikia bodi kwa kipindi cha miaka 3 na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine cha miaka 3 kama ambavyo imeelekezwa mwanzo huku, isipokuwa Mwenyekiti wa bodi ambaye kaitumikia bodi hiyo kwa kipindi cha miaka 4 na anaweza kuteuliwa tena.

Sasa Mhe. Spika, hapa kidogo mimi ninahisi pana tatizo, tatizo ambalo naliona huku kutakuwa kuna mamlaka ambayo itaweza kufanya mambo haya ambayo niliyasoma mwanzo. Lakini huku kutakuwa kuna bodi ambazo kazi zake hazikuainishwa hapa, hii bodi itakuwa inafanya kazi gani na mamlaka gani. Lakini vile vile bodi hii ambayo itakuwa imeteuliwa itakuwa na uwezo wa kufanya kazi wajumbe wake ndani ya miaka 3 lakini kwa huyu Mkurugenzi Mkuu ambaye atakuwa anateuliwa yeye anateuliwa kwa muda wa miaka 4. Sasa hapa sijafahamu uwezo na mamlaka ya mfilisi yatakuwa vipi, kwa sababu ninavyoelewa kwa bodi ambazo nimezoea kuziona bodi ambayo itakuwa iko pale imeteuliwa ndio itakayokuwa na mamlaka ya kufanya shughuli za ufilisi, ikiwa kama kutatokezea tatizo la namna yoyote bodi ndio inayowajibika. Sasa kwa utaratibu huu ambao uko hapa ningeliomba nipate maelezo zaidi hapo ambapo pengine tutakapopata hiyo semina tutaweza kufahamu vizuri zaidi na tutaweza kwenda vizuri kwa mujibu wa taratibu ambazo tumejiwekea.

Jengine nakuja katika ukurasa wa 348 uwezo wa jumla wa mamlaka. Katika kifungu cha 11(a) inasema kwamba kupokea, kutoa, kubadilisha au kufuta leseni kwa mujibu wa sheria hii. Lakini (g) kuna kupanga bei, tunzo na malipo mengine yote yatakayoelekezwa na mwenye leseni kwa mujibu wa taratibu zilizotolewa katika kanuni na sheria nyengine za huduma. Sasa huyu mwenye leseni hasa ni nani? Naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie zaidi kwa sababu bado kuna vitu vinatukanganya.

Halafu chengine katika ukurasa wa 357 kifungu cha pili, mamlaka itashughulikia mambo yote ya ushindani yatakayotokea wakati wa utekelezaji wa kazi zake na inaweza kuchunguza na kuripoti kuhusiana na mambo hayo na kutoa mapendekezo kwa mamlaka ya viwango Zanzibar au chombo

chengine chochote chenye mamlaka. Sasa hapa sijafahamu vile vile Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mamlaka haya yatakuwa ni ya bodi au mamlaka yenyewe ambayo iko pale vile vile hapa pananipa utata kufahamu kidogo, naomba kupewa maelezo zaidi ili niweze kujua nini hasa tunachokusudia kukifanya hapa.

Halafu jengine Mhe. Spika, ukurasa wa 360 kinga dhidi ya kushtakiwa. Mhe. Spika, hapa tunasema kwamba Mwenyekiti Mkurugenzi Mkuu, Mjumbe au Afisa yoyote wa mamlaka hatokuwa na dhima ya madai au jinai kuhusiana na tendo lolote alilolifanya au aliloacha kulifanya kwa nia njema. Sasa hebu ningeliomba tafsiri ya nia njema katika hili. Mimi kidogo hapa pananipa utata na Kiswahili hapa kidogo kimenipenya. Sasa ningeliomba nifahamishwe zaidi maana halisi ya nia njema kwa sababu naona hapa hii nia njema tutaijua inakuja vipi kwa wakati gani na kwa nani. Sasa hapa vile vile ningelipenda kufahamu zaidi.

Lakini kwa ujumla wake Mhe. Spika, mimi nahisi kwamba niungane na wenzangu kuona kwamba iko haja ya kukaa pamoja kama semina kuona kwamba suala hili tunalijadili kwa kina na kuweza kujadili kifungu baada ya kifungu ili tuweze kupitisha mswada huu na baadae kusiwe na marudio ya kusema kwamba labda mswada huu urejeshwe tena umekosewa katika eneo hili na lile.

Baada ya maelezo hayo kama nilivyokwisha kusema mwanzo naunga mkono hoja. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuturuzuku neema zake za uhai na uzima na tukakutana tena kwa mara nyengine hapa kuzungumza masuala mbali mbali yanayohusu wananchi wetu. Mhe. Spika, naomba vile vile nimshukuru na nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuleta mswada huu unaohusu udhibiti wa sekta hizi za maji na nishati.

Mhe. Spika, kabla ya kuingia katika mswada wenyewe na mimi naomba niungane na wale waliozungumza kwamba kabla ya kuzungumzia udhibiti ilikuwa kwanza tuhakikishe kwanza hizi huduma wanazotaka kudhibiti kwanza zipo. Mhe. Spika, ukiutazama mswada huu umejikita katika sekta tatu kubwa. Ni mafuta, maji na umeme, mafuta kwa kiasi fulani imeachiwa sekta binafsi kuingia kati, lakini sekta hizi mbili za maji na umeme mpaka hivi tunavyozungumza serikali ndio ambayo imechukua jukumu la kutoa huduma hizi.

Mhe. Spika, tukiifuatilia mijadala ya chombo hiki chombo cha wananchi si katika kipindi hiki tu, katika vipindi vyote Wawakilishi wa wananchi wamekuwa mara kwa mara wakija hapa wakiwasilisha au wakiwakilisha malalamiko ya wananchi kutokana na kutopata huduma hizi kwa hali ya kuridhisha. Sasa leo tunapoleta chombo cha kudhibiti ninajiuliza serikali imeridhika kwamba sasa imeshamaliza au imefikia kiwango kizuri sana cha kutoa huduma hizi kwamba sasa inaleta mamlaka ya kudhibiti utoaji wa huduma hizi? Mimi ninafikiri ni suala la msingi ambalo tungepaswa tujiulize.

Lakini jengine Mhe. Spika, wamezungumza hapa Wawakilishi wengine kwamba hakuna ubaya wa kuleta chombo ambacho kitasaidia udhibiti hasa wa utoaji huduma ambazo zinawagusa wananchi moja kwa moja. Lakini kiasi gani kwamba baadae tunazitekeleza sheria hizi? Na hili kaka yangu Mhe. Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kwamtipura Mhe. Hamza mara nyingi analisema katika Baraza hili, kwamba tatizo letu si sheria, tatizo letu ni utekelezaji wa sheria na pengine kwa sababu hatuweki taratibu mapema za kuona tumejipanga vipi kutekeleza hizo sheria kabla hatujazitunga. Niliwahi kusema mara humu na najua karibuni mmepata bahati ya kwenda Zambia bila shaka na hilo mmeliona kwamba wenzetu Zambia Serikali ikipeleka mswada inatakiwa ipeleke na *cost implications* za utekelezaji wa mswada ule. Yaani gharama ambazo serikali na tukisema serikali maana yake ni walipa kodi watazopaswa kuingia katika kuutekeleza mswada au sheria itakapokuwa sheria.

Sasa Mhe. Spika, sisi si katika gharama hata mara nyengine katika kujipanga kwa maana ya rasilimali watu katika kuona vyombo vile vinavyotakikana, tumepitisha sheria Mhe. Spika, kutoa mfano tu hapa mwaka jana ya viwango Zanzibar *Bureau of Standards* na sheria ile Mhe. Spika, ilichukua muda mrefu sana tangu ilipotiwa saini mpaka kuwapata kwanza huyo mkurugenzi mkuu na bodi yake na mpaka leo tunavyojua hata matayarisho ya utekelezaji wa sheria ile imekuwa bado.

Kwa hivyo Mhe. Spika, hata ofisi imekuwa hakuna wanavutana tu baina ya Wizara na serikali kuu ya kuwapatia ofisi, Mhe. Spika, nilikuwa nataka kusema hili kwa sababu ndio maana najiuliza tumejipanga kiasi gani kwanza hizo huduma zenyewe zipo zinazotaka kudhibitiwa. Lakini la pili je tumejipanga kuona sheria hizi zinatekelezwa?

Sasa Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba kidogo niende katika mswada wenyewe na Mhe. Spika, utaniwia radhi zaidi nimetumia uliogaiwa wa kiingereza lakini nitaazima kwa wenzangu wa Kiswahili ikiwa nitahitaji kufanya mapitio.

Mhe. Spika, niseme moja vile vile kabla sijaingia kifungu kwa kifungu kwamba mara nyengine tunapata tabu Wajumbe wako tulipoingia leo hapa baada ya miswada ile tukakabidhiwa nyaraka mbili. Moja mapendekezo ya marekebisho kuhusiana na mswada wa sheria ya kuanzishwa kwa mamlaka ya udhibiti ya huduma ya maji na nishati Zanzibar na mambo yanayohusiana nayo ambayo yametoka kwenye Kamati na ina saini ya Mwenyekiti wa Kamati. Lakini baadae tukapewa na karatasi nyengine marekebisho ya mswada wa sheria ya ZURA huu hauna saini hatujui umetokea wapi waraka huu, lakini haya yaliyokuwepo humu na yaliyokuwemo humu baadhi ya maeneo yanatofautiana. Sasa mimi ninajiuliza nikichangia hapa ninasoma yote hii pamoja na ule mswada na kipi hasa ambacho kinasimama katika mswada huu Mhe. Spika, kidogo ninahitaji kujua hii inatupa tabu sana Wajumbe wako mara nyengine tunataka kujua tunachangia kipi hasa ambacho kimekubalika ambacho ndio kipo mbele ya Baraza sasa kinajadiliwa itatupa shida sana Mhe. Spika.

Nikiingia katika mswada wenyewe Mhe. Spika, kwanza naomba nizungumzie kifungu cha 4 kuna baadhi ya maeneo yameshazungumzwa, naomba nikizungumzie kifungu cha 4 cha mswada huu. Na katika hili Mhe. Spika, niseme pointi yangu ya jumla halafu ndio kwa nini ninakigusia kifungu hiki.

Mhe. Spika, nilisema mwanzo katika maelezo ya utangulizi wangu kwamba watoaji wa huduma mbili kubwa zinazotakiwa kudhibitiwa na mswada huu au sheria hii maji na umeme ni serikali yenyewe. Chombo hiki kinacholetwa mamlaka ukitazama kimelimbikiza mamlaka yote kwa serikali ambayo ndiye mtoaji wa huduma hizi, sasa najiuliza serikali inayotoa huduma inataka kujidhibiti yenyewe, inataka kuji-*regulate* yenyewe.

Mhe. Spika, katika misingi ya utawala wa sheria kuna *checks and balances* na ungetegemea uwe na chombo hata kama ni cha umma lakini sicho ambacho kinadhibitiwa kwa kiasi na serikali kiweze kudhibiti watoaji huduma ambao kwa sasa ni serikali. Sasa Mhe. Spika, haya yanaonekana vipi, kwanza ungetizama kifungu cha nne kifungu cha 4 Mhe. Spika kinazungumzia muundo wa mamlaka kinaanza pale na Mkurugenzi mkuu huyu anateuliwa na Rais kwa mujibu wa kifungu cha nne cha kwanza.

Lakini halafu ukisoma kifungu cha tano hichi sasa kinazungumzia kuanzishwa kwa bodi, cha sita kinazungumzia muundo wa bodi wenyewe, sasa hicho cha muundo wa bodi Mhe. Spika, kinazungumzia kutakuwa na wajumbe 7, Mwenyekiti ambaye anateuliwa na Rais na Mkurugenzi Mkuu ambaye anaingia kwa nafasi yake ambaye huku nyuma pia keshateuliwa na Rais halafu Wajumbe wengine watano ambao wanateuliwa na waziri angalau wawili katika hao wawe wanawake wote hao Mhe. Spika, wanachaguliwa na

serikali kuja kuidhibiti serikali. Tena ninaloliona mimi balaa liko wapi kwamba Waziri anaeteua Wajumbe watano hawa ndie yeye Wizara yake inayotoa huduma hizi kwa sababu maji na umeme inatolewa na wizara hii hii. Sasa ninajiuliza hapa kweli patapatikana uadilifu, patapatikana utawala wa sheria wakati yule anayekuteua wewe kuingia katika chombo cha kudhibiti yeye mwenyewe ndiye mwenye dhamana ya utoaji wa huduma hizo hizo katika wizara hiyo, hapa inanipa shida sana Mhe. Spika.

Na ili nisipoteze wakati huko mbele nikizungumzie kabisa Mhe. Spika, kuna kifungu kile kinachohusu lile baraza lililoitwa la wateja ambalo sasa limerekebishwa sasa linaitwa baraza la watumiaji kifungu cha 31, hili pia Mhe. Spika, ukilisoma linasema kifungu cha 31.2 Baraza litaongozwa na Mwenyekiti na wajumbe wasiopungua watano na wasiozidi saba watakaoteuliwa na Waziri kutoka kwenye taasisi zinazotambulika kisheria kuwa zinawakilisha maslahi ya sekta binafsi na sehemu nyengine za umma kama Waziri atakavyona inafaa. Sasa Mhe. Spika, mswada huu umelimbikiza madaraka makubwa sana kwa Waziri na kwa maana hiyo kwa serikali ambayo ndio inayotoa huduma hizo hizo. Huku kwenye chombo chenyewe kifungu cha 6 bodi sehemu kubwa ameiunda Waziri, Baraza la Watumiaji analiunda Waziri sasa Mhe. Spika, hiyo *checks and balances* inapatikana wapi katika mswada huu. Hao utaosema unataka kuwalindia huduma zao wanawakilishwa vipi Mhe. Spika, mimi napata shida sana katika hili. Na nitaomba maelezo ya kina kama mswada huu kweli niridhike niweze kuupitisha.

Mhe. Spika, madaraka hayo hayaishii hapo, ukitoka hapo kile kifungu nilichosema cha tano hii nimezungumzia uteuzi tu wa wajumbe sasa uwajibikaji kifungu cha tano Mhe. Spika, kinasema kwamba kunaundwa mamlaka hiyo na ili tufahamiane naomba nikisome kile cha Kiswahili kinasema, inaanzishwa bodi ya wakurugenzi ya mamlaka ambayo kwa kuzingatia sheria hii itakuwa jukumu la kusimamia shughuli za mamlaka na itawajibika kwa Waziri. Na kwa kiingereza iko hivyo hivyo Mhe. Spika, sasa bado kila unapokwenda Waziri, Waziri, sikatai kwa mfumo wetu wa utawala na mara nyingi tumelijadili hili kwamba Waziri ana madaraka ya kusimamia sekta hizi kwa hivyo ana mamlaka fulani lakini huu Mhe. Spika, huu umelimbikiza madaraka yote kwa Waziri hicho chombo kipo kipo tu kwa mtazamo wangu mimi au kitapoundwa kitakuwepo tu lakini hakina mamlaka yanayokusudiwa.

Mhe. Spika, ukija katika kifungu cha nane kile nilichokitaja cha mwanzo cha sita cha wale wajumbe watano hakuna Mhe. Spika, kifungu kinachomzuia Waziri kwamba atatakiwa kushauriana na chombo fulani kuwapata wale wajumbe watano achague mwenyewe tu, lakini hicho nikiache, tujadili

kifungu cha nane Mhe. Spika, ambacho hata kaka yangu Mhe. Salmin Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni kakizungumzia sana hapa, hiki Mhe. Spika, kina mashaka mengi, kwanza katika kuzungumzia hizo *specific powers* ambazo mamlaka imepewa, kinataka kwamba ni pamoja na kufanya mambo yafuatayo:

Kwenye mafuta Mhe. Spika, kuna kifungu pale kusimamia viwango kwa kushauriana na Waziri lakini hapa imetajwa viwango katika kiingereza imeandikwa *to regulate tariff in consultation of the minister, tariff* sio viwango *tariff* ni bei. Lakini ukija katika maji vile vile inasema cha 8(2) kinasema kusimamia viwango, malipo, bei kwa kushauriana na Waziri. Ukija kwenye umeme Mhe. Spika, ni hivyo hivyo 8(3), kusimamia viwango kwa kushauriana na Waziri lakini humu imetafsiriwa viwango ukija katika kiingereza unaikuta imeweka vizuri zaidi *to regulate tariff in consultation of the minister.*

Sasa Mhe. Spika, ninajiuliza kwa utaratibu wetu wa utendaji kazi tunaujua hapa ukisema ushauriane na Waziri maana yake unaifunga mamlaka kwamba haiwezi kufanya maamuzi peke yake bila kukubaliana na Waziri hata kama itatumika lugha ya kushauriana iliyokuwa imewekwa hapa. Sasa nilikuwa ninajiuliza Mhe. Spika, katika sheria hii kweli tumekusudia kuwalinda watumiaji au tunawadanganya na kuwalaghai kwa kuwaundia chombo ambacho kitaondosha manung'uniko yao na malalamiko lakini bado mamlaka yote na yule mtoaji wa huduma yenyewe ambaye ni serikali.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo naomba kidogo bahati mbaya suala la muda Mhe. Spika, lakini naomba hayo mengine niyaache niende kwenye masuala mawili ya haraka haraka ili niwahi muda. Moja Mhe. Spika, kuna kifungu nadhani cha 22 kile kinachozungumzia vyanzo vya mapato ambavyo au vyanzo vya fedha za mamlaka. Hiki kinasomeka Mhe. Spika, fedha za mamlaka zitajumuisha fedha zinazotolewa na serikali imeandikwa na kuidhinishwa na Baraza la Wawakilishi, fedha zote zitakazopatikana na mamlaka kutokana na ada, tozo, ruzuku, misaada, mikopo na malipo mengine itakayolipwa mamlaka kutokana na leseni kama itakavyoelekezwa na sheria nyengine za kisekta, halafu kuna na mambo mengine ambayo yametajwa.

Sasa Mhe. Spika, mimi hofu yangu ipo hapa katika kifungu hiki cha (b). Mhe. Spika, kule kwenye kifungu cha nane imetajwa katika moja za mamlaka ni kutoa *license* na ukishaanza kutoa *license* au leseni unaongezea gharama za uendeshaji ambazo hao wanaotoa leseni watawabinya wanaotumia huduma hizi. Kwa sababu ukimwambia mtu ongeza leseni hapa hatoi mfukoni mwake Mhe. Spika, atakwenda kuongeza bei ya gharama kwa hivyo badala ya kwamba unamsaidia mtumiaji unamkamua zaidi. Lakini ukija ukisoma 22 (b)

kwa sababu mmoja katika fedha zake ni hizo, ada, malipo misaada, sasa Mhe. Spika, nataka kuuliza swali moja hapo naomba Waziri akija naomba anisaidie, tulipokuwa tukijadili ripoti ya ZECO katika kikao kilichopita nilihoji suala moja kwamba inaonekana ZECO pia ilikuwa inatozwa tozo fulani ambayo inalipwa EWURA kule na nikawahi kuhoji siku ile hapa kwamba EWURA haina mamlaka Zanzibar wala haitoi huduma yoyote kwa Mzanzibari, kwa nini ZECO ikatwe fedha asilimia fulani asilimia tatu ninafikiri ilikuwa inayokwenda kwa EWURA.

Sasa hofu yangu Mhe. Spika, katika vyanzo hivi utakuja kuwa watoaji wa huduma ni ZECO na ZECO huyu atapewa atoe fedha ambayo tunaiendesha ZURA lakini ZECO huyu huyu sasa analipa asilimia 3 kuipa EWURA wote huu ni mzigo kwa mlipa kodi wa Zanzibar ambaye anatumia huduma hizi. Na itakuwa vile vile kwa ZAWA na kwa wengine. Sasa hili serikali ikija ituwekee wazi hapa kwamba jee kwa kuanzisha ZURA zile asilimia 3 ambazo zilitajwa katika ripoti ya ZECO tuliyojadili kikao kilichopita zinaondoka kwenda EWURA sasa zitakuwa zinalipwa ZURA na mzigo ule utakuwa hauwi mara mbili kwa walipa kodi wa Zanzibar. Nilikuwa hilo naomba Mhe. Spika, liwekwe wazi.

Mhe. Spika: Muda umemalizika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ninakushukuru Mhe. Spika, sitaunga mkono hoja mpaka nipate maelezo ya kina juu ya mswada huu. Ahsante.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe ninakushukuruni kwa kuanza shughuli zetu leo vizuri na kuna tangazo moja dogo. Waheshimiwa Wajumbe nimeombwa niwatangazie wale wachezaji na wapenzi wa timu yetu ya mpira wa miguu kwamba tunakumbusha kuwa mazoezi yatakuwa yanaendelea kila siku ya Alkhamis, Ijumaa na Jumamosi katika uwanja wa Mao wakati wa asubuhi ili vile vitu mlivyoonesha juzi muendelee kuwa navyo katika miguu yenu. Kwa hivyo shime tuhudhurie kwa wingi katika mazoezi hayo siku ya Alkhamis, Ijumaa na Jumamosi mapema asubuhi.

(Saa 7.00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutufikisha hapa lep siku ya Jumatano katika kufungua Baraza letu hili la Mwezi wa Aprili. Pia nikushukuru wewe kunipa fursa hii ya kuchangia Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Matumizi ya Huduma ya Maji na Nishati Zanzibar ya mwaka 2013.

Mhe. Spika, mswada huu ni mzuri lakini sasa tukitizama ni kwamba maji kwa Zanzibar sehemu nyingi bado zina matatizo ya maji na kukitungia sheria kitu ambacho hakipo au kina upungufu basi sheria inakuwa na matatizo. Tukiangalia hususan katika majimbo yetu ya Matemwe maji yana matatizo makubwa. Kwa hivyo, Sheria hii ya udhibiti wa maji hususan kwa Jimbo la Matemwe kuna mabomba matupu hakuna maji, sasa Mheshimiwa tutadhibiti maji au tutadhibiti mabomba kwa kule kwetu. Sasa Mhe. Waziri namuomba kwamba atufike au Mamlaka ya Maji (ZAWA) itufike Matemwe hakuna maji tutakuwa tunadhibiti mabomba tu hayana maji na sheria ya kudhibiti maji basi yawepo na hatuna maji.

Hivi sasa nishati nyingi zinatoweka kwa sababu kuna nishati za miti zinatoweka, nishati nyengine nazo zinatoweka. Kwa hivyo, vile vile sheria hii iangalie sana udhibiti wa nishati, miti haiku hivi sasa na miti ndio nishati kubwa kwa Zanzibar.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, sheria hii tutapoikubali basi iambatane na vile vitu kwamba viwepo na viwe vya uhakika kwamba hivi vitu vipo ndio tunavitungia sheria. Ningeiomba sana serikali kupitia Wizara ya Maji kuangalia wananchi wanavyopata tabu kutokana na maji kuwa yana shida na hii sheria tukiitunga tutaitunga wapi wakati maji hakuna. Namuomba Mhe. Waziri alifikirie sana na afanye ziara hasa makusudi ya kuja kututembelea kuangalia maji, maji yakiwepo tutaitunga sheria, maji hakuna sheria haitungiki kwa sababu wananchi hivi sasa hasa ukienda kule kwenye Jimbo langu la Matemwe kama Mwenyekiti wangu Bi Asha Bakari alivyosema kwamba wanawake wametoka vipara basi si kwa maumbile ni kwa madoo ya maji hii ni kweli. Hivi sasa maji yana tabu sana hivyo naiomba wizara, namuomba Mhe. Waziri afanye ziara makusudi pamoja na wafanyakazi wa ZAWA waangalie matatizo ya maji, maji yatapokuwepo madhubuti na sheria itafuata.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi mchango wangu huu namsisitiza Mhe. Waziri atufike katika majimbo yetu kuangalia matatizo ya maji. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe wachangiaji wangu wawili ambao nimekuwa nao katika orodha mmoja ameniarifu kwamba amepata dharura kidogo na mwengine ni Mhe. Hamza Hassan Juma simuoni, basi majadiliano yanaendelea.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, nami kupata fursa ya kuchangia mswada huu angalau maneno mawili matatu. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni hii kukutana hapa katika shughuli zetu za kawaida za Baraza. Kadhalika nikushukuru na wewe kwa uongozi wako unaotuongoza katika Baraza hili. Pia nitoe shukurani kwa Waziri kwa kutuletea mswada huu ambao kama ukipita utakuwa ni sheria ambao utatawala taasisi nyengine zitakazokuwa chini yake.

Mhe. Spika, nianze na muundo kwa hii Mamlaka ambayo nataka kuijadili, kwanza nitoe kidogo mambo ambayo kuwa mimi nimeona yameandikwa kwa mimi niliyesoma *Waminkimaupaku* sivyo. Sisi tuliosoma huko kwa mwanadamu tunaandika ambaye na hatuandiki ambae. Kwa hivyo, hapa Mkurugenzi kaandikwa mtu ambae sasa mimi ningetaka isomeke mtu ambaye, iwangawaje masomo ya skuli ni tofauti lakini kwa Kiswahili cha zamani iwe hivyo isiwe ambae, ambae iwe ni mnyama au mdudu, lakini kwa mwanadamu tutumie neno ambaye.

Halafu kuna pahala ‘okana’ hii iwe ni ‘akiona’, pale palipoandikwa Mhe. Rais okana kuna haja ya kumteuwa Naibu Mkurugenzi sasa imeandikwa sivyo ilivyo ni akiona kuna haja. Kifungu hicho hicho kuna pahala pameandikwa ‘nne’ iwe ‘minne’.

Halafu Mhe. Spika, niende kwenye sifa za Mkurugenzi Mkuu wa hii Mamlaka kifungu nambari 4(3) (b) naomba hii sehemu niinukuu.

Kifungu cha 4(3) (b) kinasema kwamba:

> “Awe na taaluma ya shahada ya pili au kiwango kinacholingana nacho kutoka katika chuo kikuu kinachotambulika kati ya fani ya mafuta au maji au umeme au uongozi au biashara au uhandisi au sheria au fani nyengine zinazofanana na hizi na uzoefu usiopungua miaka mitano”.

Mhe. Spika, zogo lote hili lingeandikwa kwa lugha fupi tu awe na shahada ya pili basi, kwa sababu fani zote zimetajwa kuwa awe na moja angalau hiyo, ingetajwa awe na shahada ya pili ingekuwa tayari imekidhi haja hakuna haja ya kutoa mzunguko wote huo wakati ambapo lugha fupi anavyotakiwa Mkurugenzi Mkuu awe ni mtu wa shahada ya pili, tena kama anafanyia maji

sawa, umeme sawa, iwe uongozi au biashara sawa. Kwa hivyo, ilikuwa hakuna haja ya mzunguko wote huo wa uandishi.

Mhe. Spika, huyu Naibu Mkurugenzi Mkuu ametajwa kuwa Rais akiona iko haja ya kumteua anaweza kufanya hivyo. Mimi nahisi hii taasisi haina haja ya kuwa na Naibu Mkurugenzi ni kuongeza zogo tu au wingi wa watu katika taasisi za uongozi. Taasisi zenyewe Mhe. Spika, inaongoza mamlaka ambazo zina mamlaka kamili inavyotajwa, kuna Shirika la Umeme ni Shirika ambalo kamili linajitegemea, kuna Mamlaka ya Maji ZAWA ni mamlaka kamili inayojitegemea halafu juu yake inawekewa mamlaka nyengine. Kwa hivyo, mamlaka inayojitegemea inawekewa mamlaka nyengine ije itegee hivyo hizi mamlaka za mwanzo hizi zitakuwa chini ya mamlaka hii sasa sijui kama hakutakuwa na mgongano wa utendaji kati ya mamlaka ambazo zipo na ni mamlaka za serikali na hatimaye serikali hiyo hiyo ikaweka mamlaka nyengine juu yake.

Huko mbele Mhe. Spika, kumechomoza kitu Bodi ambayo imepewa wajibu tu, lakini katika muundo kwenye sheria hii haikuonekana sheria hii imeundwa kwa misingi gani lakini imewekwa tu wajibu wa bodi. Sasa hii bodi nayo imekuwa ni kubwa kuliko mamlaka zote hizi tatu. Kwa hivyo, bodi, mamlaka tumejadili kuna Mamlaka ya Maji, kuna Shirika la Umeme wote hawa watatawaliwa na hii bodi ambayo muundo wake haupo imejitokeza tu kuwa hii bodi ina majukumu ya bodi, lakini muundo wa bodi ukoje, wajumbe wake wamepatikana vipi katika sheria hii haikuelezwa. Sijui bodi hii imetoka wapi ambayo katika sheria hii bado haijaundwa lakini bado itakuwa inatawala hivi vyombo ambavyo vipo.

Mhe. Spika, kwa maoni yangu mimi nadhani mamlaka hii ambayo kuna sehemu inasema itatoa leseni katika mambo ya kukabili ushindani wa kibiashara. Lakini katika maji Mamlaka iliyopo ni ZAWA sijui ni nani atakaepewa leseni ya kuendesha shughuli za maji na kukimbia kushindana na nani? ZAWA ni Taasisi ya Serikali sasa tunasema tutoe leseni ili kuweza kukabiliana na ushindani tushindane na nani na ZAWA ndio mamlaka iliyopo wala hakuna chombo chengine chochote kisheria kiliopo kinachohusiana na usambazaji na utoaji wa huduma za maji.

Kadhalika katika umeme hivyo hivyo. Shirika la Umeme Zanzibar ndio pekee sasa tukisema kuwa kuna ushindani na tutoe leseni tunashindana na nani, mtu aliyekuwa peke yake katika chombo anafanya anavyotaka sasa sisi tunashindana na nani. Kwa hivyo, hapa Mhe. Spika, bado hii lugha ya kuwa zitolewe leseni kwa ajili ya kukabiliana na ushindani wa aina hii nadhani utakuwa haupo.

Mhe. Spika, nije kidogo katika kifungu cha nane (8) Uwezo wa Mamlaka, hiki kipo katika ukurasa wa 346. Mamlaka itakuwa na uwezo wa kusimamia huduma zifuatazo: mafuta, maji na umeme; hizi ndizo ambazo mamlaka hii inataka kukabidhiwa kisheria kusimamia uwezo wa huduma hizo. Lakini Mhe. Spika, taasisi hizi zipo kisheria zinajiendesha na ni taasisi za serikali. kwa maoni yangu ni kuongeza msongamano katika utendaji wa shughuli zetu na huenda kukatokea migongano baina ya taasisi mbili hizi. Kwa sababu kila moja ni kubwa na ina mamlaka ya kujitegemea lakini pia zote hizi hatimaye zinasarenda mambo yake kwa Mhe. Waziri mhusika. Sasa taasisi ambayo imeambiwa kuwa inajitegemea lakini mwisho wa siku mambo yake yote yanamalizia kwa waziri sasa huo utegemezi wa taasisi hii uko wapi.

Mhe. Spika, kadhalika nitizame kazi za Mamlaka Kifungu cha 9(d), tayari nimezungumza kuwa ni ushindani ambapo hapana ushindani. Nije kwenye kifungu cha 10 sehemu ya 3(b) Ukuzaji wa Nishati ya Maji Safi na Salama.

Mhe. Spika, hapa mimi itabidi nipate maelezo, kwa sababu maji safi kwa uoni wangu mimi si nishati, maji yanakuwa nishati pale yanapotayarishwa kutoa umeme ndio yanageuka kuwa nishati ya maji, lakini maji safi na salama kwa ajili ya matumizi hapa haiwi kuwa ni nishati inabaki kuwa ni maji tu safi na salama na hapa imeelezwa kuwa ukuzaji wa nishati ya maji safi na salama. Ningependa nifafanuliwe haya maji imekuwaje kuwa ni nishati wakati ambapo ni maji safi tu na salama kwa ajili ya matumizi.

Mhe. Spika, nije katika kifungu cha 13 ukurasa wa 350 ambapo nimetaja kuwa kuna bodi iliyojichomoza tu, lakini haina muundo na ina majukumu tu, isipokuwa imetajwa mwisho wa kifungu cha 12 naomba nikinukuu kifungu hicho ili nieleweke ninachokusudia kusema.

Kifungu cha 12(5) kinasema kwamba:

> "Mamlaka itatangaza katika Gazeti viwango vya bei na tozo ndani ya siku thelathini kuanzia siku Bodi iliporidhia viwango hivyo".

Sasa hii bodi inaridhia viwango vya vitu ambapo huku nyuma haijatajwa kuwa ipo imetokea wapi? Mhe. Spika, niendelee kidogo kifungu cha 23 ukurasa wa 352 kifungu kidogo cha pili.

Kifungu cha 23(2) kinasema kwamba:

"Kwa kuzingatia masharti ya kifungu (1), Bodi itawasilisha kwa waziri kwa kuidhinishwa nakala ya bajeti ya mwaka unaofuata".

Mhe. Spika, mamlaka hii tunayoizungumza hivi sasa haina uwezo wowote kwa sababu kila kitu chake kinatawaliwa na mamlaka iongezwe juu yake. Wao wanatayarisha bajeti hatimaye bajeti yao wanaipeleka kwa Bodi, bodi ambayo mimi sijaiona na baada ya bodi kuridhia wanai-*hand over* kwa waziri kwa uamuzi wa mwisho. Lakini kwenye mazungumzo yote hayo inaweza kuwa hii bodi ina uwezo wa kujitegemea sasa kujitegemea huku kuko wapi, kuwa kila hatua inayokwenda kuna chombo chengine kilicho juu yake kinachoshughulikia masuala haya.

Mhe. Spika, baada ya machache hayo niliyoyaeleza naomba niseme kuwa niishie hapo ahsante sana.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, kwanza na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia jioni hii kuwepo hapa katika kuendeleza majukumu yetu ya kitaifa. Lakini pia nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kunipa nafasi jioni hii na mimi kutoa mchango wangu ijapokuwa kimuhtasari katika mswada huu wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Matumizi ya Huduma ya Maji Zanzibar ya mwaka 2013.

Pia nataka nitoe shukurani za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyengine katika mazishi ya Mbunge wa Jimbo la Chambani Marehemu Salum Hemed Khamis, Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema, Amin.

Lakini pia Mheshimiwa kwa hili niseme natoa shukurani pia kwa ujumbe wa Baraza la Wawakilishi uliofika pale ukiongozwa na Naibu Spika pamoja na Mwenyekiti. Kwa niaba ya wananchi wa Chambani nasema kwamba nawashukuru wote wale walioshiriki katika mazishi pamoja na mambo mengine yaliyohusiana na mazishi yale na mwisho nasema, *Innalilahi Wainna Ilayhi Rajiuun.*

Mhe. Spika, niende katika mswada ukurasa wa 345 kifungu cha tano. Ukurasa huu unasema kwamba, Rais kama akiona ipo haja anaweza kuteua Naibu Mkurugenzi Mkuu. Mhe. Spika, mimi hili naona kwamba ni tatizo kwa kuwa mamlaka hii kuna Wakurugenzi wa Idara watakaoteuliwa na bodi kwa mujibu wa masharti ya sheria ya Utumishi wa Umma basi hakuna haja ya kuteua Naibu Mkurugenzi Mkuu. Kwa sababu kutakuwa na idara mbali mbali zitakazoteuliwa na bodi ambazo hizi zitakuwa na wakurugenzi mbali mbali.

Mhe. Spika, nikiendelea mbele niende katika ukurasa wa 347 kifungu cha 2(a) na (c). Mhe. Spika, ukurasa huu kifungu cha pili kinasema kwamba, kwenye

nishati ya mafuta itatoa leseni (a) usambazaji, (b) uagiziaji na (c) usambazaji wa jumla na reja reja na mambo mengine yanayohusiana na nishati hiyo.

Mhe. Spika, kifungu (a) hapa pana usambazaji na (c) kuna usambazaji wa jumla na reja reja na mambo mengine yanayohusiana na nishati hiyo. Namuomba Mhe. Waziri atakapotoa majumuisho anipe ufafanuzi wa kina juu ya usambazaji huu pamoja na usambazaji wa jumla na rejareja, naona hapa lugha hii mimi inanichanganya kiasi fulani naomba ufafanuzi wa kina.

Halafu nikienda katika ukurasa wa 351 Mhe. Spika, kifungu cha 16(1) Bodi itamteua mwanasheria mwenye sifa kuwa katibu wa bodi. Naomba Mhe. Waziri atueleze hizo sifa za mwanasheria huyu mwenye sifa gani, kwa sababu sifa ziko za aina tofauti tungelijua kwamba mwanasheria huyu ni mwenye sifa ipi ambayo Bodi itamteua kwa hizo sifa ambazo atatueleza Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, niende katika kifungu cha 30(4), iwapo Mamlaka itatambua, nanukuu.

Kifungu cha 30(4) kinasema kwamba:

> "Iwapo Mamlaka itatambua kuwa mgongano unaweza kuingilia kwa kiasi kikubwa utendaji na majukumu ya mfanyakazi au mjumbe huyo, mamlaka iliyomteua itamuhamisha".

Haya aliyazungumza Mhe. Mohamed Ali Khalid kwamba kuna matatizo ya uandishi. Inasema mamlaka iliyomteua itamuhamisha, nahisi kwamba hapa imekusudiwa itamuamrisha mfanyakazi au mjumbe kujiuzulu.

Mhe. Spika, mimi hapa ningeomba marekebisho kwa sababu kuna watu wanaweza kuamrishwa kujiuzulu wakajikataza kujiuzulu lakini hapa ingekuwa kwamba mamlaka iliyohusika imuajibishe, kwa sababu kumuajibisha ni tendo ambalo litakuwa si la hiyari lakini kuambiwa tu kwamba jiuzulu anaweza kukaa asijiuzulu na badala yake kukawa na mvutano, lakini mamlaka iliyohusika imuwajibishe moja kwa moja.

Kwa hivyo Mhe. Spika, baada ya mchango huu mfupi, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chambani na baada ya marekebisho hayo ambayo nimeyaeleza hapa, naunga mkono hoja.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa ya kuweza kutoa mchango wangu kuhusu mswada huu uliopo mbele yetu. Awali ya yote Mhe. Spika, niungane na wenzangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku ya leo tukiwa hai na hatimaye kutupa

uwezo wa kuja hapa Baraza na kutoa michango yetu. Hii ni hazina kubwa aliyotujaalia Mwenyezi Mungu na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Mhe. Spika, tuungane na mjumbe aliyekaa hivi sasa kulishukuru Baraza lako kwa kuweza kushiriki katika mazishi ya Mbunge wetu aliyefariki juzi. Kwa hivyo tunaipongeza sana afisi yako kwa kuweza kushirikiana na sisi katika msiba huo. Hii ni kutokana na wewe mwenyewe unavyojali na kuthamini utu wa mwanadamu.

Mhe. Spika, nasema kwamba sheria hii au mswada huu umekuja wakati ndio kwa sababu wakati hivi tunazungumza kuna tatizo kubwa la udhibiti wa mambo haya yanayohusiana na huduma ya maji pamoja na nishati kuna matatizo mengi. Kuna watu hivi sasa wanalipia pipe, bomba zile za maji na sio maji; kila mwezi tunalipia bomba shilingi elfu mbili na mia tano bila ya maji. Ni tatizo kwa kweli.

Katika hili kwa hivyo nipongeze serikali kwa kuweza kuleta chombo hiki ambacho kitasimamia mambo haya. Lakini Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa nilikuwa nasoma madhumuni ya kuletwa mswada huu katika ukurasa wa 362 kwamba mswada huu umeletwa kwa sindikizo la nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Kwa mfano inasema Jumuiya ya Afrika ya Mashariki imezitaka nchi wanachama kuwa na chombo cha udhibiti wa nishati. Sasa haya mambo Mhe. Spika, serikali yetu ni lazima iwe makini isisubiri kusindikizwa katika mambo muhimu kama haya. Kwa hivyo ilikuwa tusisubiri mpaka Jumuiya itushindikize ilikuwa tulete tu moja kwa moja bila ya kupata sindikizo lolote. Sasa kwa sababu umekuja Mhe. Spika, mimi naunga mkono serikali katika hili na niseme tu kwamba naunga mkono mswada huu asilimia mia kwa mia.

Mhe. Spika, kwa kweli chombo hiki kuanzishwa ni muhimu lakini kuanzishwa ni upande mmoja na kuwezeshwa ni upande wa pili. Kuanzishwa chombo bila ya kukiwezesha ni tatizo kubwa. Kwa hivyo Mhe. Spika, naiomba serikali mswada huu utakapokuwa sheria na kuanzisha hiki chombo lazima kipewe uwezo wa kuweza kusimamia kazi zake.

Kwa mfano Mhe. Spika, Mamlaka ya ZAWA hivi sasa inashindwa kutenda haki kwa Wazanzibari, kwa mfano sisi katika eneo la jimbo langu kule maji hatupati, lakini ikiwa wewe umeunga maji tu katika nyumba yako japo kuwa kama wewe katika mwezi mzima hupati, lazima ulipe shilingi elfu mbili na mia tano. Lakini kuna makampuni ya ujenzi yanatumia maji mengi zaidi ya lita tano kwa siku, na wao vile vile wanalipa shilingi elfu mbili na mia tano.

Mimi nadhani ni kwa sababu hiki chombo kiliopo hivi sasa kinachosimamia mambo haya ya maji hakina uwezo, lakini naamini kuwepo kwa sheria hii na chombo hiki tukikianzisha basi kila mtu atabeba ule mzigo wake, sio kubebeshwa mzigo uliokuwa haumuhusu.

Mhe. Spika, ukiangalia umuhimu wa kuwepo kwa sheria hii na kuanzishwa kwa chombo hiki ni kwamba tunaweza kufanya utafiti wa kina juu ya kuweza kuvitambua pamoja na kuvienzi vyanzo vya maji. Kwa mfano hivi sasa Mhe. Spika, katika maeneo mengi kuna ukosefu wa maji kwa sababu tunashindwa kusimamia vizuri vyanzo vya maji. Watu wanajenga pale katika maeneo na wanafanya shughuli kwenye maeneo ya vianzio na hakuna chombo kinachoweza kuwadhibiti au sheria itakayoweza kuwadhibiti. Kwa hivyo maji yanakuwa ni tatizo.

Lakini kuwepo kwa chombo hiki naamini vyanzo vya maji tutaweza kuvitunza na sheria itawadhibiti wale wote ambao wanaoweza kuchafua au kuharibu vyanzo hivi. Kwa mfano hivi sasa Mhe. Spika, mamlaka iliopo haina uwezo wa kuweza ku-*exotic* vyanzo vya maji, kwa mfano maeneo mengi yana matatizo ya maji lakini uwezo wa chombo cha kuweza kusimamia maji hapana. Kwa mfano wenzetu katika nchi mbali mbali walio katika ukanda huu wa bahari wanatumia maji ya chumvi kuweza kupata maji safi ya kunywa na kutumia. Lakini sisi ukija wenzetu hawa hawana uwezo. Naamini kuwepo kwa chombo hiki kunaweza kuleta vyanzo mbadala vya kuweza kupata maji safi kama wenzetu wanavyoyafanyia *distillation* maji ya bahari na kuyafanya kuwa maji safi ya kuweza kutumia.

Mhe. Spika, vile vile vyanzo hivi havina uwezo wa kitaalamu, kwa mfano katika sekta hii ya mafuta. Hivi sasa kule Pemba kumekuwa na uharibifu mkubwa wa *diesel engine* kwa sababu mafuta yetu yanachakachuliwa sana. Kwa hivyo hakuna vyombo vya kuweza kupima usafi wa mafuta yale jambo ambalo ni hasara kubwa kwa wananchi.

Ni hivi juzi mafuta yanayouzwa katika vituo rasmi lakini magari mengi yameharibika injector pump kwa sababu hakuna udhibiti au chombo kinachosimamia nishati hakina uwezo wa kupima ile *percentage utility* katika mambo ya mafuta.

Sasa naamini sheria hii itakuwa ni mkombozi wa wananchi katika hili na itaweza kuweka sheria ambayo atayeyachakachua mafuta sheria itamdhibiti katika hilo.

Aidha Mhe. Spika, hakuna utaalamu wa kina katika kuyapima hata yale mafuta kwamba yana *carbon* ya *percentage* ya kiasi gani. Huku ukiangalia

kwamba kuna mabadiliko ya tabia ya nchi. Mafuta tunayoletewa kutoka huko kwao yanakuja hapa yakiwa na ma-*carbon* mengi, hayajasafishwa vizuri yanaharibi mazingira na kuletea tatizo hili la tabia ya nchi na kuleta madhara zaidi. Sasa ninaamini kuwepo kwa hili hata kiwango cha usafi wa mafuta yale basi yanaweza kujulikana na yakazuuliwa kuingia nchini.

Mhe. Spika, matarajio yangu ni kwamba mswada huu utakapopita na kuwa ni sheria na kuanzisha mamlaka hii, basi mamlaka hii itasimamia viwango vya umeme wanaopatiwa wananchi wetu. Inasikitisha sana Mhe. Spika, katika maeneo mengi umeme unakuwa hauna nguvu, watu wanalipitishwa umeme lakini mtu pengine kuna mambo mengine hayatumiki kwa sababu ya umeme ni mdogo.

Kwa hivyo ni matarajio yangu kwamba baada ya kuanzishwa kwa chombo hiki kitasimamia kiwango cha umeme utakaopelekwa kwa wananchi wetu. Ni tatizo kubwa hili Mhe. Spika, kwa sababu unaweza ukawa na umeme nyumbani kwako lakini friza halifanyi kazi kwa sababu ya umeme mdogo, maeneo mengi hasa huko kwetu vijijini. Kwa hivyo nadhani katika hili ni vyema tunaungana na serikali tukaukubali mswada huu kusudi kuweza kupata chombo ambacho kitasimamia mambo haya ya nishati pamoja na maji.

Mhe. Spika, mamlaka hii itakuwa na uwezo wa kutoa leseni kama tulivyoelezwa katika mswada lakini utoaji wa leseni huu lazima tuwe waangalifu sana, isije ikawa mamlaka kazi hii zaidi ijikite katika kutoa huduma na sio katika mambo ya biashara, kuwawezesha kila mwananchi apatiwe leseni kwa bei ambayo anaweza kuimudu, isije ikawa mwananchi anataka kuanzisha kisima au kuanzisha jambo linalohusiana na nishati ikawa tena leseni hainunuliki, hii itakuwa ni biashara na sio huduma. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Spika, katika hili mamlaka tutakayoianzisha iwe ni mamlaka ya kutoa huduma na isiwe ya kibiashara.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naunga mkono mswada huu asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi nikupe shukurani zangu za dhati kwa kunipa nafasi hii jioni hii ya leo na mimi nikaweza kuzungumza machache kuhusu mswada huu.

Mhe. Spika, mimi kwanza nataka nianze kama waliotangulia waliopita jioni kwamba mswada huu ni muhimu sana. Mswada huu ni muhimu sana kwa sababu tuna matatizo na matatizo haya yapo muda mrefu, tumekuwa tukilalamika sana kwamba tunapata bidhaa au tunapata huduma ambayo haina

ubora au haina kiwango. Sasa kwa kuanzishwa mswada huu au kwa kuletwa sheria utaweza kusaidia kuondoa hili tatizo.

Lakini Mhe. Spika, kutokana na ugumu wa mswada huu na utata wa mswada huu basi ili tusije tukamsumbua sana Mhe. Waziri katika kuupitisha mswada huu, kwa sababu mimi tu peke yangu nimejaribu ku-*quote* vifungu havipungui karibu 20 na vyote ni vya buti.

Sasa ili kuondoa hayo Mhe. Waziri angelitusaidia akatupatia muda wa ziada, akatupa ufafanuzi wa kutosha kabla ya kwenda kwenye vifungu ili mswada huu tuupitishe na maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, mimi naungana na rai aliyoitoa Mhe. Salmin Awadh, mswada huu uendelee kuwepo lakini tunaweza tukau-*suspend* kidogo ili tukapata dozi, yaani taaluma au semina kwa jina la kizungu la kisasa, *atleast* tukaweza kuelewa kwa sababu Mhe. Spika, tumeshawahi kupitisha hapa sheria baada ya miezi mitatu tu tukarudi tena kwako. Sheria tuliyoipitisha ina utata, unatuuliza kwani mulikuwa wapi kwa sababu hatukuweza kupata muda mzure wa kuweza kujadili.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Katiba na Utawala Bora alifanya suala la busara sana katika sheria hii ya kuanzisha; Sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na kuwa tulipata taaluma ndogo kwa watu wachache, lakini kwa kiasi fulani tuliweza kuboresha sana ule mswada na naamini ukija hapa Barazani pamoja na ugumu wa ule wa mswada lakini tutaweza kuuchangia katika kuuboresha zaidi, lakini mambo mengi yaliyokuwa na utata tuliweza kuyafanyia marekebisho.

Sasa si busara kuja kupitisha vifungu kwa njia ya kura, itakuwa si jambo zuri na Mhe. Spika, sasa hivi tumejenga mashirikiano makubwa sana baina ya serikali yetu na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili mambo mambo yetu yasiende tukaonekana labda tunavutana, ili tuende vizuri. Sasa mimi pamoja na kwamba nitajaribu kuupitia baadhi ya vifungu nitachangia mswada huu lakini bado ninatoa rai Mhe. Spika, kwa sababu angalia huu mswada kutokana na umuhimu wake lakini bado unakuta watu wanakuwa wagumu kusimama kuuchangia pamoja kwamba Waheshimiwa wamekuwa wazito kuuchangia kwa sababu dau limegonga mwamba mpaka sasa hivi, kwa hivyo fikra zao nyingi zipo ufukweni lakini hii pia inatokana na ugumu wa mswada huu.

Sasa nadhani ni vizuri Mhe. Spika, tukaweza kupata ufafanuzi wa kutosha. Baada ya hayo Mhe.Spika, naomba sasa niende moja kwa moja katika kuuchangia mswada huu.

Mhe. Spika, mimi moja kwa moja nitaka nianze na kifungu cha 2 kwenye tafsiri ya mwenyekiti lakini baadae baada ya kuangalia marekebisho ya kamati nikagundua imefanywa marekebisho, sina tatizo nayo. Lakini kwenye tafsiri ya neno "mtu", kifungu cha pili ufafanuzi mtu, mtu maana yake ni mtu kibailojia au kisheria. Sasa kidogo hapa mimi nimepata taabu katika hii tafsiri. Sasa nitamuomba Mhe. Waziri aje anisaidie kibailojia mtu mimi namjua moja kwa moja inajulikana kutokana na maumbile yake. Sasa hii mtu kisheria. Kuna mtu ambaye hakuumbwa kama binadamu lakini akaitwa mtu? Sasa hii nitaomba kidogo nije nipate ufafanuzi.

Mhe. Spika, nikiendelea vile vile katika tafsiri hii kifungu cha mwisho kabisa kabla ya kifungu cha 3 kwenye hiki hiki kifungu cha 2 mwisho kabisa kwenye tafsiri, naomba ninukuu kinasema "Huduma maana yake ni umeme, usambazaji wa maji, mafuta, gesi na mambo mengine yanayohusiana na hayo kama itakavyoamualiwa na waziri". Sasa lakini hii hapa mbele nilipokuja kuangalia katika zile kazi ambazo watakazoweza kuzifanya hii mamlaka, hii nitakuja kuitoa ufafanuzi wake kwa sababu niliona huduma za maji, huduma za umeme, huduma za mafuta na nishati lakini huduma ya gesi humu ndani katika kazi ya hii mamlaka naona hazikuweza kufafanuliwa. Sasa nikifika huko mbele nitakuja kuchanganua zaidi ni nini ambacho nilichokuwa nikihitajia.

Mhe. Spika, vile vile kifungu cha 3(2) naomba nikinukuu. Kifungu cha 3 (1) kinasema, "Inaanzishwa mamlaka itakayojulikana Mamlaka ya Udhibiti na Huduma ya Maji na Nishati Zanzibar. Kifungu cha (2) kinasema "Mamlaka itakuwa ni chombo kinachojitegemea kudumu chenye muhuri wake kwa kutumia jina lake na ina uwezo, halafu huku chini ikaja ya, nasema kupata au kutwaa mali inayomiliki au inayohamishika au isiyohamishika, kuingia mikataba na mtu yeyote au taasisi, kushtaki au kushtakiwa, kukopa au kukopeshwa fedha, kushiriki au kufanya shughuli yoyote kwa mujibu wa sheria ambazo zitakazoweza kufanywa na chombo chengine chochote.

Sasa hapa Mhe. Spika, nilikuwa nataka kuzungumzia jambo moja ambalo pia na baadhi ya wenzangu waliwahi kulizungumzia. Suala la Mamlaka kuajimini katika kutenda shughuli zake. Mhe. Spika, mamlaka zetu nyingi bado pamoja kwamba sheria tunapitisha kwamba wanatakiwa wajiamini aidha katika kukopa au kukopesha, lakini Mhe. Spika, mashirika yetu mengi sana bado yanakuwa yanashindwa kujiamini, yanashindwa kujiboresha kwa sababu wanashindwa kuingia mikataba au kuingia katika mikopo ambayo ya kuweza kuijenga taasisi yenyewe.

Mhe. Spika, mimi nitatoa mfano mdogo. Mfano leo tuna Mamlaka ya Maji, ukiangalia mamlaka hii kuna Mamlaka yenyewe ya Maji lakini vile vile kuna

na bodi. Lakini Mamlaka ya Maji mpaka leo wameshindwa kuweka miundo mbinu ambayo ya kuweza kutoa huduma za maji katika miji yetu mbali mbali, ikiwemo mji wa Zanzibar likiwemo na jimbo langu la Kwamtipura.

Kwanza hapa nataka nitoe pole wananchi wangu wote wa Jimbo la Kwamtipura kwa kadhia kubwa wanayoipata kutokana na huu ukosefu wa maji kwenye jimbo letu. Hapa Mhe. Spika, kwa kuwa tunaunda hiki chombo ambacho kitakachoweza kusimamia udhibiti lakini vile vile na utoaji wa leseni lakini vile vile na usimamizi. Sasa hapa Mhe. Spika, sijui huduma hii kwa kweli itakuja kusimamiwa vipi kwa sababu kama mfano ingelikuwa hii mamlaka imeundwa kusimamia taasisi ambazo ni binafsi ambazo ni zenye ushindani ingelikuwa ni jambo rahisi sana. Lakini tatizo Mhe. Spika, nafikiri na kuna baadhi ya wenzangu waliwahi kugusia kwamba mamlaka hii ambayo tunayoiunda inakwenda kusimamia taasisi nyengine ambayo tayari zipo na zimeundwa kisheria.

Sasa ikiwa mamlaka mfano nitaitolea mamlaka ya maji; ikiwa imeshindwa kutoa huduma katika ubora unaotakiwa na Mamlaka ya Maji inatoa huduma hii haina leseni isipokuwa ina sheria tu ya kusimamia ambayo tumeianzisha kusimamia kutoa huduma ya maji katika mji wetu. Sasa jee hapa watakuja kuwachukulia hatua gani. Sasa hili kidogo Mhe. Spika, pia nitahitaji nije nilipatie ufafanuzi au nipatiwe ufafanuzi.

Mhe. Spika, nikija katika kifungu cha 4 kinasema muundo. Mamlaka itakuwa na muundo ufuatao, Mkurugenzi ambaye atakuwa mtendaji mkuu wa mamlaka ambaye atakayeteuliwa na Rais. Sasa Mhe. Spika, labda niendelee na huku mbele baadae maelezo yangu niyatoe kwa pamoja.

Halafu kifungu cha 4 (2) kinasema Mkurugenzi Mkuu atakuwa ndiye mwenye dhamana ya uongozi katika utekelezaji wa kazi za uendeshaji wa mamlaka ya kila siku katika utekelezaji wa usimamizi wa mamlaka. Halafu Mkurugenzi Mkuu atakuwa na sifa hizi ambazo zilizotajwa. Nachukua hii (b) awe na taaluma ya shahada ya pili au kiwango kinacholingana nacho kutoka katika chuo kikuu kinachotambulika kati ya fani ya mafuta au maji au umeme au uongozi au biashara au uhandisi au sheria au fani nyengine zinazofanana na hizi na uzoefu usiozidi miaka mitano.

Sasa Mhe. Spika, chombo hiki ni kikubwa sana na chombo hiki ni kikubwa kwa sababu ni chombo zaidi cha kitaaluma na kinasimamia taasisi ambazo zenye taaluma mbali mbali; Taasisi ya Maji ina wakurugenzi wake, ina wataalamu wa maji, Shirika la Umeme lina wataalamu ambalo ni eneo ambalo vile vile ni eneo la nishati, lakini vile vile Mhe. Spika, ukija katika

suala ambalo halikutajwa sana hata gesi kwa sababu nishati pamoja na gesi pia ni nishati vile vile.

Sasa Mhe. Spika, mimi nadhani katika hizi sifa za Mkurugenzi. Mimi nafikiri tungelikwenda nazo mpaka kati ya fani ya mafuta au maji au umeme. Lakini sasa hii au uongozi au biashara au uhandisi au sheria; haya huku mimi nadhani Mhe. Spika, tunaweza tukaja tukapoteza ina maana ambayo ya kuweka hiki chombo. Kwa hivyo chombo hiki kinataka mtaalamu ambaye anawasimamia wataalamu. Sasa masuala ya uongozi tu, uongozi wa biashara Mhe. Spika, mtu atakaa pale kuangalia tu jee hiki chombo kinatuendesha kitapata faida na wakati mwengine hata bila ya kuangalia huduma, wao zaidi watajaribu kuangalia faida tu. Kwa hivyo mimi nadhani Mhe. Spika, katika hizi sifa za mkurugenzi mimi nadhani tungeliishia pale au umeme, hizi nyengine za chini tunaweza tukaja tukamuweka mtu kwenye mamlaka, yeye anataka kuwasimamia watu wenye utaalamu, yeye utaalamu ule atakuwa hana.

Lakini chengine Mhe. Spika, kinasema kifungu cha 4 hiki kinasema kamati imefanya marekebisho sina matatizo nacho. Lakini vile vile kifungu cha 4 (5) kinasema "Rais kama akiona ipo haja anaweza kuteuwa Naibu Mkurugenzi Mkuu". Mimi nadhani hapa tuamue kama kutakuwa na Naibu Mkurugenzi basi moja kwa moja tutaje kwenye sheria atateuliwa, kuliko kusema kwamba Rais kama akiona ipo haja, Mhe. Rais ana kazi, ana majukumu mengi, tusimpe taabu ya kuanza kumuekea kitu ambacho kina-*hang*; maana yake hii ni sawa sawa na kama itakuwa ina-*hang*.

Kwa hivyo nadhani hiki kifungu cha 4 (5) mimi nadhani tukubaliane kwamba kama ipo haja ya kuweka Naibu Mkurugenzi tumueke lakini kama haipo haja basi tukiondoe kabisa kuliko kusema Rais kama ataona ipo haja, mimi nafikiri hakuna mantiki au hakuna faida yoyote kubakia kifungu hicho.

Mhe. Spika, nikiendelea kifungu cha 4 bado nataka kidogo nitoe mchango wangu wa mawazo.

Kifungu cha 4(1)

> "Mkurugenzi Mkuu ambae atakuwa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ambae atateuliwa na Rais".

Lakini huku mbele vile vile kuna Mwenyekiti wa bodi, kifungu cha 6(1) kinasema

kifungu cha 6(1)

> “Bodi ya Wakurugenzi itakuwa na wajumbe saba ambao wataitumikia bodi kwa kipindi cha miaka mitatu mitatu na wanaweza kuteuliwa tena katika kipindi chengine cha miaka mitatu, isipokuwa Mwenyekiti wa bodi ambaye atatumikia bodi kwa kipindi cha miaka minne na anaweza kuteuliwa tena”.

Halafu hapa chini kuna (a),(b) na (c);

(a) Mwenyekiti atateuliwa na Rais.
(b) Mkurugenzi Mkuu;

Sasa huyu Mkurugenzi Mkuu itakuwa ndiye yule aliyekuwepo kule juu. Sasa hapa Mhe. Spika, mimi nilikuwa nashauri na hili nililishauri hata nilipokuwa nikichangia maoni ya katiba ya Jamhuri ya Muungano ambapo na Katiba ya Zanzibar itakapokuja kurekebishwa nitachangia tena hivi hivi, kwamba Mhe Spika, wakati wa sasa hivi ni wakati wa uwazi sana, wakati wa uwajibikaji zaidi kuliko kuangalia labda utashi.

Sasa mimi nadhani Mhe. Spika, Mkurugenzi nafasi hii ni vizuri angeliomba, isiwe moja kwa moja kuteuliwa na Rais. Mwenyekiti sina tatizo, mwenyekiti muache ateuliwe na Rais kwa mujibu wa hivi vigezo ambavyo vilivyowekwa. Lakini Mkurugenzi mimi nadhani angeomba, kwa sababu gani nikasema hivyo. Mhe. Spika, sasa hivi tumekuwa tukipata tabu sana hasa hapa Barazani, tunapochangia sheria mbali mbali, tunapofuatilia utekelezaji wa shughuli za serikali, wakati mwengine unakuta kuna makosa ya wazi wazi, makosa ya kizembe. Lakini sasa wale wasimamizi wote wanakuwa wanateuliwa na Rais, kwa kweli Baraza lako linashindwa kuwasimamia ipasavyo, kuwasimamia katika kutekeleza majukumu yake. Wakati mwengine unaposimamia uwajibikaji katika watendaji hawa na kwa kuwa mamlaka ni ya Rais ina maana huna tena pahala pa kwenda kuhoji, kwa sababu ukishasema Makamu wa Pili wa Rais yupo, taarifa zimeshafika. Ina maana Rais kama hakufanya vile basi hakuna uwezo mwengine wa kuweza kumdhibiti mtendaji yule.

Kwa hivyo, mimi nadhani hawa watendaji wengine angalau wangekuwa wao wanaomba hizi kazi, ili chombo chako hiki Mhe. Spika, tunapowasimamia kwenye uwajibikaji, tunapowasimamia katika shughuli zao za kila siku, tuwe na uwezo na nguvu za kuweza kuwasimamia katika suala zima la uwajibikaji. Suala hili nalisema kwa sababu chombo hiki Mhe. Spika, tunachokiundia hii sheria, wale ambao wanawasimamia utakuta Mkurugenzi mfano wa Mamlaka ya Maji au Shirika la Umeme wote wanateuliwa na Rais. Wenyeviti wa Bodi wa Shirika la Umeme ama Mamlaka ya Maji wanateuliwa na Rais.

Mkurugenzi wa taasisi hii tunayoiunda anateuliwa na Rais, Mwenyekiti wa Mamlaka anateuliwa na Rais.

Sasa hii Mamlaka ya Rais ni nyumba kubwa haitakiwi kutiwa mikono kila wakati, lakini katika wakati wa uwazi watendaji wanapokuwa hawafanyi vizuri wanaboronga inabidi lazima tuseme. Lakini sasa ile nguvu ya kuweka na kuondoa, ile nguvu inakuwa kwenye mikono ya mamlaka ya mtu mmoja. Sasa hili nafikiri Mhe. Spika, tungejaribu kuliangalia kwa kina ili hivi vyombo visije vikagusana.

Mhe. Spika, tumeshuhudia, kuna baadhi ya wakurugenzi, basi hata jawabu wanazowajibu mawaziri wao hazipendezi. Ukijaangalia sababu Mkurugenzi kateuliwa na Rais na waziri kateuliwa na Rais, kila mmoja mkubwa yeye. Sasa na hapa kuna wateuliwa sita wa Rais, wote wanasimamia utendaji wa shughuli hiyo hiyo. Kwa hivyo, mimi nadhani Mhe. Spika, hapa lazima tujaribu kuangalia upya.

Mhe. Spika, mimi mapendekezo yangu kwa nafasi ya Mkurugenzi kwa hizi hizi sifa zilizotajwa, basi waweze kuomba hizi nafasi ili kuwe na mashindano mazuri, lakini vile vile tupate huduma bora.

Mhe. Spika, mfano leo tuna mashirika hapa, tuna mashirika yapo muda mrefu hayatii faida yanatia hasara. Lakini tunashindwa kuwawajibisha kwa sababu gani, kwa sababu utakuta wale viongozi wao wameteuliwa na Rais. Sasa mtu akishateuliwa na Rais, kwa hivyo hahisi ule uwajibikaji wake, kama anahisi labda kuna chombo kinaweza kikaweza kumuwajibisha. Kwa hivyo, mimi nadhani hii mamlaka kwa kweli mimi naomba Mhe. Spika, kwa nafasi ya Mkurugenzi basi aweze kuomba sio kuteuliwa na Rais.

Vile vile hapa imeelezwa kwamba wajumbe hawa wengine watakaa katika vipindi vya miaka mitatu mitatu. Anaweza akateuliwa tena mara ya pili, yaani watateuliwa vipindi viwili vya miaka mitatu mitatu. Lakini Mwenyekiti au Mkurugenzi yeye atakaa katika kipindi cha miaka minne. Sasa labda hapa tufahamishwe kulikuwa kuna mantiki gani ya kuweza kufanya hivyo, ile mantiki ndio ninayokusudia. Kwa sababu unajua akishateuliwa Mwenyekiti, inateuliwa na bodi ile ambayo atakayofanya nayo kazi, lakini sasa bodi inakaa miaka mitatu, Mwenyekiti au Mkurugenzi anakaa miaka minne. Sasa huyu Mwenyekiti anakuwa ni Mwenyekiti wa bodi au Mwenyekiti wa nini, kwa sababu bodi inamaliza kwa muda wa miaka mitatu.

Mhe. Spika, kifungu cha 6(2) kinasema;

> "Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha (1) cha kifungu hiki, wajumbe wanaoteuliwa na Waziri, isipokuwa wajumbe kwa nafasi

zao watalazimika angalau kuwa na Shahada ya Chuo Kikuu katika fani ya utawala au uhandisi, au maji au sheria, inafuta sheria au fani nyengine zinazofanana na hizo, wawe na uelewa au uzoefu unaolingana na majukumu ya mamlaka ambapo wajumbe wawili kutoka sekta binafsi".

Sasa hii inafuta ndio ilivyokusudiwa inafuta, kwa sababu naona kama haileti maana. Sasa hapa sijui kama kuna *typing error* au kuna koseo la haya maandishi. Kwa hivyo, hapa kidogo nilikuwa nataka maelezo katika hiki kifungu cha 6(2), hapa katika taaluma inasema inafuta sheria au fani nyengine. Hapa kidogo nilikuwa nataka ufafanuzi Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nikija katika kifungu cha 8(1)(2) na (3) naomba nikinukuu; Kinahusu Uwezo maalum wa mamlaka katika sekta ya petroli.

Mhe. Spika, Kifungu cha 8 kinasema;

"Mamlaka itakuwa na uwezo maalum wa kusimamia huduma zifuatazo;

(1) Mafuta:
- Kutoa, kupitia na kufuta vibali vya petroli;
- Kusimamia viwango kwa kushauriana na Waziri;
- Kukosa ushindani na ufanisi bora wa uchumi;
- Kudhibiti viwango na ubora kwa kushauriana na ZBS.

Vile vile kifungu 8(2) kinasema;

(2) Maji:
- Kudhibiti ubora wa viwango vya maji kwa kushauriana na ZBS.
- Kusimamia viwango, malipo, bei kwa kushauriana na Waziri.
- Kudhibiti ubora wa maji.
- Kutoa matangazo ya usimamizi wa maji na leseni na usambazaji maji.

(3) Umeme:
- Kutoa, kupitia na kufuta leseni za kuzalisha, kugawa, kuunga.
- Kusimamia viwango kwa kushauriana na Waziri.
- Kukuza ushindani wa uzalishaji wa umeme.
- Kusimamia ubora wa viwango.
- Kusimamia uwekaji na utiaji wa umeme.
- Kupitia mikataba ya manunuzi.

Mhe. Spika, hapa mimi kidogo nilikuwa nataka nisaidiwe maelezo. Kwa mfano katika hili eneo la mwanzo, eneo la mafuta. Hapa Mhe. Spika, najua kwamba kuna leseni ambazo zinazotolewa kwa ajili ya uingizaji wa mafuta, lakini sijui leseni hizi zinavyotolewa labda kuna kikomo, pengine ule uingizaji, je anatakiwa yule muingizaji na yeye awe na vituo vyake halafu awe anauza rejareja au anatakiwa yeye alete kwa jumla halafu awauzie vituo vyengine vidogo vidogo. Kwa sababu hii biashara wakati mwengine Mhe. Spika, tunajua kuwa mafuta yapo katika *deport*, lakini huku mitaani mafuta hakuna, ukienda kwenye mageleni tunauziwa bei ya kuchupa na kuruka. Sasa katika kipindi hiki Mhe. Spika, kwa sababu wao ndio wanaoleta basi wao ndio wanadhibiti, maana yake kama wangekuwa wanaleta wengine katika vituo wako wengine basi wasingeweza kufanya jambo kama hili. Kwa hivyo, suala hili mimi nilikuwa naomba nipate ufafanuzi.

Lakini vile vile

Mhe. Spika: Una dakika tano za kumaliza mchango wako.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Sasa Mhe. Spika, mimi nafikiri mswada huu kwanza tungepewa taaluma kwa sababu sasa hivi itabidi moja kwa moja niende katika kupata ufafanuzi wa vifungu tu, ili niweze kuja kuzuia. Kwa sababu kama nilivyosema nitazuia vifungu sio chini ya 30 katika mswada huu. Kwa kuwa muda wangu utakuwa ni mdogo, sasa niombe kupata ufafanuzi wa vifungu hivi.

Mhe. Spika, naomba nipate ufafanuzi katika kifungu cha 8(1),(2),(3) halafu kifungu cha 9(a),(b), (c), (d) na (l). Vile vile nitaomba nipatiwe ufafanuzi katika Kifungu cha 10(1)(1) kwenye nishati ya umeme na kifungu cha (2), (3) na (4). Halafu vile vile kifungu cha 10(4) nipate ufafanuzi (2) na (3). Kifungu cha 10 vile vile nipate ufafanuzi kifungu cha 4(4).

Lakini pia kifungu cha 12(1) nipate ufafanuzi, halafu kifungu cha 12(3)(a),(b), (c) na (d) nipate ufafanuzi. Kifungu cha 13(d) nipate ufafanuzi. Mhe. Spika, kifungu cha 14(b) nipate ufafanuzi, pamoja na kifungu cha 14(c) na kifungu cha 15(c) na kifungu cha 21 vile vile.

Mhe. Spika, hiki kifungu cha 15(c) naomba kidogo nikizungumze ili tuweze kujua hizi sheria tunazozipitisha kama kweli tunazisimamia vizuri au ndivyo zinavyotekelezwa.

Mhe. Spika, kwenye kifungu cha 15(c) kinasema, yaani hapa inakusudiwa mjumbe wa bodi atasita kuwa mjumbe iwapo yatatokea yafuatayo. (c) kinasema, amepata nafasi katika ofisi yenye mgongano wa kimaslahi na bodi

au mamlaka. Mhe. Spika, kifungu hiki kama tutakipitisha basi tutakuwa tunapitisha vifungu katika sheria ambavyo serikali haivitekelezi, kwa nini?

Mhe. Spika, tumezungumza hapa kuna taasisi ambazo wale viongozi wakuu wana maslahi katika taasisi zile, tumezungumza, tumezungumza. Serikali haina habari haisikii wala haitaki, sasa leo tunapokiidhinisha kifungu hiki Mhe. Spika, ni sawa sawa tutakuwa tunacheza. Tutakuwa tunapitisha sheria, tutakuwa tunapitisha sheria, ndio yale ninayosema siku zote, tunapitisha sheria hapa hazitekelezwi. Kifungu hiki kama kitapitishwa basi naomba kwanza wale waliokuwepo katika nafasi, ambao wana maslahi katika taasisi hizo, kwanza wawajibishwe au waondolewe katika nafasi hizo kwanza, vyenginevyo Mhe. Spika, katika kifungu hiki nitakujakuwa mgumu sana, kitaonekana hakina maana, lakini kwa sababu hiki kina-*reflect* na taasisi nyengine.

Vile vile Mhe. Spika, tumezungumza tulipokuwa tukichangia ripoti ya Shirika la Umeme, kuna wafanyakazi wa Shirika la Umeme wao wanachukua tenda binafsi, wanawatumia watendaji wa Shirika la Umeme na wao ni Wakurugenzi katika taasisi nyengine binafsi na wanatumia zana za Shirika la Umeme, mpaka leo wako ndani ya serikali ndani ya Shirika la Umeme wanafanya kazi. Sasa leo tunapoweka kifungu kama hiki, Mheshimiwa tusiufurahishe umma, hebu tufanye kazi ya kisheria kweli kweli tuweze kuisimamia serikali. Mhe. Spika, kifungu hiki mimi nitakuja kuwa mgumu sana na katika kukipitisha kifungu hiki, itabidi tuje tupate maelezo. Kuna wale ambao waliokuwepo katika taasisi wana maslahi yao binafsi na wao ndio viongozi, mpaka leo hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa basi hata kuachia mali ile ya serikali, pia tunashindwa kumwambia achia mali ya serikali. Sasa Mhe. Spika, tusiwe tunapitisha sheria ambazo hatuzijui maana yake au vile vile zinakua hazitekelezwi.

Sasa kwa kumalizia, sio kwa kumalizia kwa kuwa sina maelezo. Kwa kumalizia kwa kuheshimu muda wako Mhe. Spika, kama nilivyosema hayo mambo mengine kama labda Mhe. Waziri atakujakukubali kuja kutupatia darsa kidogo ili tuweze kupata ufafanuzi wa kutosha.

Kwa hivyo, namalizia kwa kusema Mhe. Spika, nataka kusema kwamba tukishaipitisha tu hii sheria Mamlaka ya Maji imeshindwa kazi, haiwezi kazi na ukiangalia sheria hii Mhe. Spika. Mimi siku moja niliwahi kuzungumza hapa katika bajeti ya mwaka 2011, hetu tuwape majeshi ile idara na sasa hivi ni mamlaka. Hebu tuwape pale Mkurugenzi ateuliwe kutoka jeshini tuangalie maji yatapatikana au hayapatikani. Leo tunaunda hiki chombo kusimamia ubora na utoaji wa huduma. Leo Shirika la Umeme, umeme *Alhamdulillah*

tunaupata, lakini kuna uzembe mkubwa tena mwingi, hatuoni hatua zozote zinazochukuliwa.

Mamlaka ya Maji Mhe. Spika, sasa hivi, sisi tunapata pesa za jimbo. Mhe. Mahmoud alizungumza pale, leo kunachimbwa visima ovyo ovyo, vinachimbwa visima holela ni lazima tuchimbe visima kwa sababu wananchi wetu hawapati maji. Leo unafikiri mwananchi hapati maji na paipu ziko tele. Kuna mapaipu leo ukiangalia chini ya ardhi yaani utafikiri ni mishipa ya binadamu, lakini maji hayapatikani, sasa kama wananchi hawakuchimba visima watafanya nini.

Mhe. Spika, mimi ninakuambia ndani ya jimbo langu tumeshachimba visima sasa hivi havipungui saba, lakini bado ukienda wananchi vichwa vinaoto vipara kama mimi mwenyewe, yaani wananchi wangu wote wameshanirithi sasa hivi. Kwa hivyo, mimi nasema bado hii mamlaka ikishaundwa, basi kwanza kama kuna leseni ya Mamlaka ya Maji kusimamia, lakini je wakija kusimamishwa hawa utendaji wa kazi kuna njia mbadala. Ndio pale alipozungumza mwenzangu, angalau kungekuwa kuna *private sector* ambazo zinatoa huduma ya maji, ukasema aah wewe mamlaka ya maji huwezi kutoa huduma bora, lakini hebu tuwaweke wengine.

Jengine la mwisho kwa kumalizia Mhe. Spika, wenzetu waliokwenda Arusha wamejifunza mambo, kuhusu mamlaka ya maji wenzetu wanavyohudumia. Leo mamlaka ya maji pesa za kuendeshea shughuli zao, wakati tumepitisha ile mamlaka kwamba wao wana uwezo wa kukopa, wanaweza kukopesha, kujitegemea na kufanya kila kitu. Matokeo yake leo wanakusanya pesa za wananchi ambao hawapati maji, wakati kumbe fedha zile wangekwenda kukopa benki, wakatafuta taasisi ya fedha wakanunua mabomba wakayalaza chini ili wananchi wakaweza kulipa kidogo kidogo. Kwa hivyo, unakuta wananchi wetu Mhe. Spika, wanateseka katika suala la maji ambalo linatuharibia sana, hatuna raha. Kuna wengine tulibadilishwa majina mpaka tukaitwa Mhe. Maji, ukiwa unapita pahala unaambiwa Mhe. Maji.

Hii mamlaka pamoja na kwamba mamlaka ya maji hatukuianzisha zamani, lakini bado hatujaona mabadiliko yoyote katika shughuli zao na tuliwahi kuwashauri. Hebu basi hivi visima vilivyochimbwa na mradi wa Japan, tuweke kwa ma-*block.* Basi *block* moja safari hii Jimbo la Magomeni miezi mitatu linapata maji, muhame mnakwenda Jimbo la Kwahani linapata maji, kisha mnahama, mnakuja Jimbo la Kwamtipura linapata maji. Lakini imekuwa kama kuku anapekua, anatia mkono huku anatoa anatia mkono huku anatoa, tukichimba visima mnatuambia tunachimba visima kiholela.

Sasa Mhe. Spika, kabla hujaniambia nikae kitako baada ya hayo Mhe. Spika, mswada huu bado una utata mkubwa, tunahitaji ufafanuzi wa kutosha ili tujue hizi mamlaka zinakuja kumsimamia nani na kwa sababu zote zinateuliwa wa Rais, watendaji wengi wameteuliwa na Rais, hivyo tunahisi kutakuja kutokea migongano mikubwa katika usimamizi wa sheria hii.

Mhe. Spika, bado sijaiunga mkono hii hoja mpaka tutakapokuja kupata maelezo ya Waziri. Naamini waziri wetu ni msikivu, waziri wetu ana busara. Kwa hivyo, mimi naamini atatuweka kitako atuelimishe ili tuje tuupitishe mswada huu bila ya kuzuia kifungu chochote. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha sote wajumbe wako tukaweza kufika katika kikao hiki tukiwa ni wazima.

Vile vile naomba nitumie fursa hii nikushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ili angalau na mimi niweze kutoa mchango mdogo sana katika kuufanikisha mswada huu.

Mhe. Spika, nakumbuka kwamba katika Baraza lililopita ambapo Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali, iliwasilisha taarifa yake ile iliyoifanya kwa Shirika letu la Umeme ZECO. Nakumbuka pia kwamba moja katika mapendekezo ambayo yalitolewa na Baraza lako baadae kama ni agizo la Baraza kwa serikali, ni kuitaka serikali iunde mamlaka yenye jukumu hili. Nakumbuka hili lilikuwa ni pendekezo la Kamati, ninakumbuka baadae likawa ni agizo la Baraza kwa serikali.

Kwa hivyo, kuja kwa mswada huu kama ikiwa ni kwa serikali yetu kutekeleza masharti yaliyotolewa na nchi za Afrika ya Mashariki sina la kusema. Lakini iwapo kuja kwa mswada huu ni kwa serikali kutekeleza agizo la Baraza basi mimi naunga mkono na naipongeza sana serikali. Lakini kabla ya hapo serikali ije iseme kwamba lile agizo la Baraza ndilo hili au ndio lile pendekezo la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, maana yake tuone suala hili hasa mwenyewe ni nani, maana yake hili ni tatizo Mhe. Spika, Baraza lako hili kutoa agizo la kuunda na serikali ikashindwa kusema chochote katika suala lile. Sitaki nigeuke mganga wa kienyeji kupiga ramli, lakini nadhani Waziri katika suala lile kwa sababu ni moja katika agizo la Baraza. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja atoe kauli katika utekelezaji wake.

Mhe. Spika, kama tulivyoeleza kwamba kuwepo kwa chombo hiki kuna umuhimu mkubwa, kwa sababu katika kipindi cha hivi karibuni hadi hivi sasa tumekuwa tukishuhudia takriban mafuta mengi yanayoingia nchini mwetu

yanakuwa na matatizo, yanachanganywa na maji, kitendo kile kinapelekea athari na hasara kubwa kwa wenye vyombo vya moto.

Vile vile kama tulivyoeleza kwamba tumekuwa tukishuhudia kupandishiwa bei za umeme zilizokuwa hazina kiwango, kitendo kile kinafanywa na wenzetu kule kwa kupitia mamlaka yao ya EWURA, wakati EWURA sio chombo cha Muungano, EWURA ni chombo chenye mamlaka Bara kule, bila ya wao kwa sababu sio chombo cha Muungano hawapati taarifa zozote zinazotokana na Wazanzibari katika suala zima linalohusu matumizi ya umeme. Matokeo yake hupelekea sisi Zanzibar kupandishiwa viwango vya kodi za umeme, bila ya kujua hali halisi ya Wazanzibari tunavyoendelea. Ndio maana tukaja na wazo lile kwamba tuwe na chombo hiki basi ili chombo cha EWURA wakae na chombo hiki katika kuratibu, kupanga bei za umeme. Kwa hivyo, kuwepo kwa chombo hiki kuna umuhimu mkubwa na ninaamini kitasaidia sana kuweka mambo sawa kutokana na hizi bei za umeme zinazopanda kiholela kwa wananchi wetu.

Baada ya utangulizi huo na kama nilivyosema sitokuwa na mchango mkubwa. Nataka niende moja kwa moja kwenye kifungu cha 3 katika sheria hii ambacho kinasema kuanzishwa kwa mamlaka na kinachoeleza kuhusiana na sifa za Mkurugenzi.

Mhe. Spika, mkurugenzi katika kifungu cha 3 ameelezewa kwamba anatakiwa awe na sifa na taaluma ya Shahada kiwango cha pili ambacho kinalingana katika mambo hayo ya biashara na mengineyo. Mhe. Spika, ni lazima sasa tuende na uhalisia, tumejifunza na kwa sababu tumejifunza sasa tuchukue mafunzo tuyafanyie kazi.

Mhe. Spika, watu kama hawa ambao ni watendaji wa taasisi ni lazima tuache ubabaishaji wa kutaja masifa mengi. Maana yake unaposema au, au, au basi unampa fursa anayeteua kufanya anavyotaka yeye, matokeo yake basi ni kupata mtu ambaye hana uwezo na hana sifa. Mimi nadhani sifa mbili tu ni muhimu. Kwanza kwa sababu ni chombo cha kiufundi ni muhimu awe na elimu ya kiufundi. Lakini Mkurugenzi kwa sababu ni mwenye utawala ni lazima awe na elimu ya utawala, ni sifa mbili tu na kati ya hizo mbili basi ungeniambia kwamba nichague moja niipe umuhimu basi ningesema kwamba kwanza awe na elimu ya utawala, kwa sababu naamini kwamba atakuwa na wataalamu wengine, kama tutakavyoona baadae. Lakini Mkurugenzi huyu ambaye ndiye mtawala kutokuwa na elimu ya utawala sio vizuri kutaja mifano ya taasisi tulizonazo ambazo hatuna watawala na jinsi taasisi hizo zinavyokwenda sasa. Mtu unampa *engineer*, *engineer* na mambo ya utawala ni vitu tofauti, anaweza akawachukua wafanyakazi akawatia koleo wote, hatuwezi kwenda katika hali kama hii.

Kwa hivyo, mimi hapa napendekeza kwamba sifa mbili tu ziwekwe, yaani ni lazima awe na sifa mbili tu na kwa hizo mbili basi kwanza utawala ni muhimu kulikoni kitu chengine chochote, kwa sababu naamini kwamba watendaji wengine watakuwa na sifa zenye kuhusiana na taaluma zao. Kwa hivyo, Mhe. Spika, katika hili mimi nasimamia hapa. Biashara iende kwenye biashara huko.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 6 kinahusu sifa za wajumbe wa bodi, naomba na wajumbe vile vile tuache hizi sifa kuziacha huru, zimeelezwa hapa. Lakini mimi nadhani wajumbe na wao wawe na sifa ambazo ni *specific*, watu hao tunao, Wazanzibari jamani sasa hivi wameshasoma. Tuache kuzibabaisha sifa, tunao watu ambao wana sifa, tuwachague watu kwa sifa zao waende wakawe ni wajumbe wa bodi, ili waisaidie bodi na waisaidie mamlaka inayohusika katika kuendesha. Kwa hivyo, vile vile napendekeza kwamba kifungu hiki wajumbe wa bodi nao wawe na sifa na hasa sifa yao kubwa iwe ni mambo ya uhandisi na uhandisi nakusudia mambo ya maji, umeme au yanayohusiana na mafuta.

Mhe. Spika, kifungu cha 7 kimeeleza sifa za Mwenyekiti, naunga mkono sifa zilizotolewa za mwenyekiti, lakini naomba vile vile nipendekeze nyongeza ya sifa. Kwa sababu Mwenyekiti huyu ndiye anayesimamia bodi na bodi nio inayosimamia mamlaka, kwa hivyo lazima tuwe na Mwenyekiti ambaye yuko makini sana. Kwa hivyo, pamoja na sifa za kielimu Mhe. Spika, naomba nipendekeze na sifa ya umri, mwenyekiti lazima awe na sifa ya umri, sio kila mtu tu aliyemaliza na akapata elimu, kama ikiwa ni lazima hapa tuweke mtu basi umri wake tunasema ndio hekima yake, kwa sababu ndiye anayesimamia bodi, kwa hivyo na umri nao unahusika nao katika mambo, huwezi tu ukamchukua kijana mdogo sana ukampa kuisimamia bodi inakuwa ni tatizo. Kwa hivyo, napendekeza na sifa ya umri kwa Mwenyekiti, nayo pia izingatiwe.

Mhe. Spika, kifungu cha 18 kinaelezea kuhusiana na suala zima la kiwango cha vikao, sina tatizo na vikao vya kawaida ambapo sheria imesema kwamba vikao vya kawaida ni vitatu kwa mwaka, sina tatizo na hilo. Lakini sheria imesema kwamba Mwenyekiti akishauriana na Katibu sijui mkurugenzi wana uwezo wa kuitisha vikao. Mhe. Spika, mimi hili nalipinga, nalipinga kwa sababu uzoefu unaonesha kwamba vikao vya dharura ni vingi zaidi na zaidi. Haiwezekani vikao vya dharura tukaviachia tu, tumeona mambo mengi katika bodi vinavyokwenda vikao dharura kwa kweli ni vingi sana. Ni lazima tujue kwamba vikao hivi vinakula pesa nyingi sana katika mamlaka zinazohusika, kwa hivyo na hii tuweke kiwango katika vikao vya kawaida, lakini hata hivyo vikao vya dharura visizidi fulani, hiyo kuviachia tu haiwezekani kwa sababu

Mwenyekiti anaweza akalala na kuamka na kuitisha kikao na sheria inampa mamlaka hayo na hili haliwezekani.

Mhe. Spika, ni vyema kwa hili basi tufike pahala vikao vya kawaida tuseme ni vingapi na hata hivyo vya dharura tuseme Mwenyekiti na Katibu wake au Mkurugenzi wake wasizidi kiwango hichi katika kufanya vikao. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu kwenye kifungu cha 23 ambacho kinaelezea kuhusu bajeti. Lakini Mhe. Spika sheria zetu za fedha zinaeleza vizuri sana kuhusiana na wajibu wa kila taasisi kufunga mahesabu ya mwaka, tena kufunga mahesabu ya mwaka kuna umuhimu mkubwa Mhe. Spika, yaani ni umuhimu wa kujua ni namna gani taasisi ina uwezo katika rasilimali ama iwe fedha au rasilimali nyengine na umuhimu wa ufungaji wa mahesabu ni huo.

Mhe. Spika, tumekuwa tukishuhudia kwamba taasisi nyingi za umma hazifungi mahesabu na kutofunga mahesabu athari yake ndio hiyo, kwamba hawawapi wananchi ule uwezo wa kujua taasisi yao inakwendaje kirasilimali na *PAC* itakapowasilisha ripoti yake hayo tutayaeleza kwa kina.

Sasa pamoja na bodi kuwa na mamlaka ya kuandaa bajeti Mhe. Spika, naomba nipendekeze pia kwa sababu wenzetu katika bodi wao wakeshapewa bajeti hawaangalii umuhimu wa taasisi yao kufunga mahesabu na hilo tumekuwa tukilishuhudia tena tunalo uzoefu nalo.

Kwa hivyo, naomba pamoja na kupitia bajeti kwa maana ya mapato na matumizi, lakini bodi nayo itoe majukumu kisheria kuhakikisha kwamba taasisi yao inafunga hesabu kila mwaka kama matakwa ya sheria yalivyo.

Hili ni jambo la msingi sana Mhe. Spika, naomba hilo liwekwe kwa mujibu wa sheria na iwe ni kazi moja ya bodi kisheria kuhakikisha kuwa taasisi zao zinafunga mahesabu, kwa sababu wenzetu wa bodi wakienda posho ipo na wakishachukua posho, basi hawana habari tena na kusubiri kikao cha dharura, akienda na kuchukua posho na kuondoka na huku akamuacha Mkurugenzi na watu wake ambao wengi wao hawana uwezo wakihangaika kuvunja sheria zetu za fedha.

Mhe. Spika, naliomba hili liwekwe kwa mujibu wa sheria kwamba pamoja na kuzingatia mapato na matumizi, lakini wao wawe na dhima ya kuona kuwa taasisi yao inafunga hesabu kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, la mwisho naomba nimalizie kwa kusema kwamba serikali yetu kama kawaida yake imekuwa ina utaratibu wa kuunda taasisi ndivyo inavyotakiwa na kabla ya kuunda taasisi huleta sheria kama hizi na ndivyo

inavyotakiwa. Lakini baada ya kuleta sheria na sisi tukaipitisha kinachofuatia tena ni wenye mamlaka kufanya uteuzi na kuunda taasisi rasmi.

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Spika naomba kutoa pendekezo kwa serikali kwamba wakati wa kutayarisha sheria ya kuanzisha mamlaka au taasisi tofauti tusiangalie kwenye kuanzishwa sheria tu, pia tuangalie namna serikali inavyoweza kuzipa mamlaka fedha ama rasilimali taasisi hizo.

Kwa kweli tumeshuhudia kwamba kuna taasisi nyingi ambazo zinaanzishwa lakini kwenda kwake ni kwa kusuasua na tumeona hapa mfano wa kuanzishwa kwa *ZAWA*, ambapo hivi sasa watu wanaisema imeshindwa mamlaka, yaani imeshindwa kazi. *(Makofi)*

Lakini ukweli tuangalie *ZAWA* walipoingia pale waliingia vipi kwenye kazi zao, tutaona kwamba hivi sasa ni asilimia zaidi ya 90 ya fedha wanazolipwa wafanyakazi na wakati sheria imeshasema kuwa *ZAWA* iwe ni mamlaka inayojitegemea, lakini utegemezi wake uko wapi, yaani zaidi ya asilimia 90 ya mishahara na vitu vyengine vinatoka serikalini.

Kwa hivyo, tunaweza kuanzisha taasisi lakini lengo lisifikiwe kwa muda mfupi na yote ni kwa sababu serikali bado haijajiandaa. Vile vile tukiangalia *ZMA* mpaka leo inakuwa ni gumzo katika Baraza letu la Wawakilishi, kwamba ni mamlaka iliyopewa majukumu makubwa lakini serikali imewasaidia vipi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninachosisitiza hapa ni kwamba sambamba na kuletwa sheria katika Baraza, lakini serikali iwe na matayarisho ya mapema katika uundwaji wa taasisi kirasilimali.

Mhe. Spika, nakushukuru sana na ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia shughuli hii ya maji au nishati ya maji, ili tuweze kufaidika wananchi wote wa Zanzibar pamoja na Mswada wa Sheria ya Kuanzishwa Mamlaka ya Udhibiti ya Huduma ya Maji, Nishati na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Kwa kweli hivi sasa ni vizuri sana na ni wakati mzuri wa kuweza kuunda chombo hichi kwa ajili ya kuisaidia *ZAWA* kushughulikia maji, wakati hivi sasa tuna hakika kwamba *ZAWA* imeshindwa kuhudumia wananchi kuhusu suala hili la maji. Kwa hivyo, kama chombo hichi kitaundwa kwa manufaa ya wananchi pamoja na viumbe vyote basi tutafaidika vizuri sana na tutaweza kubadilisha hata jina likawa ZURA imeanza kuwa na sura nzuri.

Mhe. Spika, tatizo la maji hivi sasa la janga la kitaifa kwamba wazanzibari wote tatizo lao kubwa sio kula isipokuwa ni maji, kwa sababu hakuna hata mkoa mmoja wa Zanzibar ambao unaweza kusema kwamba umejitosheleza na maji. Kwa kweli katika mikoa yote ya Zanzibar ninayoifahamu mimi sijafahamu kusikia kwamba inasifu kuwa mkoa fulani umefaidika na maji mpaka wanaweza kuwasaidia mkoa mwengine kuweza kupata huduma hii ya maji.

Kwa upande wa kijimbo waliofaidika na maji ni Mji Mkongwe peke yake kwa sababu wao sijasikia kwamba Mji Mkongwe hakuna maji, lakini mikoa yote ya Zanzibar hata Mkoa wangu wa Kusini tatizo la maji ni kubwa sana na wananchi wake wote hivi sasa wanalo tatizo la maji.

Kwa hivyo, ni vizuri kama itaboreshwa hii ZURA na kuundwa na kuwepo na mpango mzuri na kuwezekana kuwa wakurugenzi wapya wazuri wa kusimamia suala hili na hilo litakuwa ni jambo zuri na sahihi kwamba nishati ya maji imegomboka na wananchi wote wamegomboka hapa Zanzibar kuweza kujihakikishia kwamba utawala wa maji umebadilika.

Mhe. Spika, itakuwa ni vizuri kwa mamlaka au nishati hii ikaanza kutumika kwa hatua mpya ambayo inategemewa na serikali na ikawa na viongozi wapya ambao wanategemewa na serikali, ili kuanzisha suala hili jipya litakapopitishwa.

Kwa kweli ni vizuri Mhe. Waziri wakati atakapokuja namuomba kupitia kwako Mhe. Spika, akatuhakikishia au kuchukua mamlaka ya kutoa tathmini ya lini ataweza kulimaliza suala hili la maji hapa Zanzibar, ili wananchi wake wakawa na tamaa kwamba ifikapo mwaka fulani tatizo la maji litakuwa limekwisha kabisa na wananchi wote watakuwa wamefaidika na suala la maji. *(Makofi)*

Vile vile ni vyema hivi sasa Mhe. Waziri akatoa tathmini kwamba hivi sasa suala la maji sio suala la kusema kuwa Mbunge au Mwakilishi atalimaliza suala la maji. Kwa kweli hakuna Mwakilishi wa Jimbo lolote ambaye ataweza kulimaliza suala la maji kama Waziri hajatoa ukweli kwamba suala la maji ni serikali peke yake hivi sasa ndio tegemeo la kulimaliza tatizo la maji. *(Makofi)*

Suala la maji hivi sasa ni jambo la kitaifa na wala sio la kimkoa au wilaya ama jimbo. Kwa hiyo, ni vizuri kuwahakikishia wananchi kwamba suala hili lisilaumike jimbo lolote kuwa linasababisha kuleta udhaifu wa maji. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala hili la nishati ya maji na mafuta hivi sasa limekuwa ni tatizo kubwa sana na lisipoangaliwa vizuri, basi ni jambo ambalo litagombanisha sana hapa nchini. Kwa mfano, hata mafuta huwa yanatokezea ghafla bila ya Waziri kuweza kutangaza kwamba leo kuna tatizo la mafuta na litakuwa kwa muda wa siku ngapi, lakini utakuta wananchi wake wanaumia zaidi na kuweza kutumia matumizi ambayo hawakujipangia kutokana na tatizo la mafuta.

Kutokana na hali kama hii Mhe. Spika unaweza kutumia mafuta ya leo ambapo ilikuwa ni bajeti yako ya wiki nzima basi ukaweza kutumia kwa siku moja kwa sababu walanguzi ni wengi na nishati hii haina uhakika na kupelekea wananchi wengi wanasumbuka katika suala la mafuta.

Mhe. Spika, hawaishii hapo kwenye suala la mafuta bali baadae wanaingia kwenye suala la maji pamoja na kuni pia nishati hizi zote zinasumbua na hata wananchi wanaweza kukosa mkate wa boflo kwa sababu nishati ya kuni nayo ina matatizo yake. *(Makofi)*

Suala la nishati hii hivi sasa ni vizuri zikapangiwa mipangilio mipya ambayo inaweza kuwasaidia wananchi wetu, kwamba hivi sasa tumepata mamlaka mpya juu ya mswada wa sheria ya kuanzishwa nishati mpya ya maji, mafuta pamoja na kuni, ili wananchi wafaidike na nishati hizi.

Mhe. Spika, hivi sasa kwa upande wa majimbo sisi Jimbo letu la Koani sasa tunayo matatizo makubwa. Kwa mfano, Jimbo la Koani ndugu zetu wa Ng'ambwa huu ni mwaka wa 49 wa Mapinduzi mpaka sasa bado hawajafaidika na maji na hili ni suala gumu sana.

Hivyo, ni vyema Mhe. Waziri kipindi hichi cha mwaka 2013 mpaka 2015 akahakikisha kwamba wananchi hawa wakaweza kupatiwa nishati hii na kufika vizuri kwenye sehemu zao, ambayo sisi tunaisimamia angalau mzigo mkubwa ukatuondokea sisi Wawakilishi na Wabunge wa sehemu hizo na suala hili likabebwa na mwenyewe Mhe. Waziri na kuhakikisha kwamba ZURA imekuwa na sura nzuri.

Kwa maana hiyo, sasa inaweza kusaidia wananchi katika jimbo hilo na kuweza kufuatilia mikoa mingine yote ya Zanzibar kuweza kupata nishati hii na kufaidika wananchi kwa wakati ambao unahitajika.

Mhe. Spika, ubora wa nishati hii hivi sasa umetoweka kabisa. Kwa mfano, utakuta sehemu nyengine wanyama wanakufa ovyo kwa sababu hakuna maji na hata ukichimba visima kwa ajili ya kupata maji, basi visima vinakauka na hatuwezi kufaidika tena wananchi wetu kuweza kufuga mifugo.

Kwa kweli hivi sasa ukienda sehemu yangu ya Mkorogo na hata leo hivi nilipigiwa simu kutoka *station* moja ya redio na kesho inaweza kusema kwamba wananchi wangu wa Mkorogo hawana maji. Hivi sasa tayari tumeshachimba visima vinne na wananchi wananisikia nasema ukweli kwamba vimekauka na wala hamna maji kabisa na wananchi wa huko wanahangaika na maji wakati huu na ingawa tumewaahidi kuchimba, lakini hata tukichimba ufundi wenyewe hatuna kama ilivyokuwa na uwezo serikali, kwa upande wa serikali wao wanazo mashine nzuri tena ni za uhakika.

Kwa hivyo, wananchi wa Mkorogo hivi sasa wanahangaika na maji na kweli visima vimekauka ambavyo vimechimbwa na Mbunge na Mwakilishi na wala hawafaidiki wananchi wa huko.

Suala hili naomba kupitia kwako Mhe. Spika, Mhe. Waziri alijue, kwamba ZURA itakapoanza tena basi isaidie wananchi hasa katika Jimbo la Koani, wananchi wana matatizo makubwa ya maji tofauti na wananchi wa jimbo la Mji Mkongwe ambao maji yake yanatiririka kutoka milimani yanafika Mji Mkongwe bila ya matatizo, na wala Mji Mkongwe husikii hivi sasa kama kuna tatizo kimechimbwa kisima na maji hayapatikani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mji Mkongwe tokea wakati wa ukoloni mpaka leo maji bado yapo, hivyo ipo haja sasa mikoa yetu ndio iwe kipaumbele katika suala la kupata huduma hii ya nishati ya maji, kama vile kuwa na mashine za uhakika, ili maji yapatikane na ZURA ianze mambo mapya na wananchi wafaidike na maji kama inavyotakiwa na serikali yenyewe.

Mhe. Spika, kwa kweli nitakuwa na furaha sana kama Mhe. Waziri atakapokuja hapa atahakikisha kutoa maelekezo zaidi au kuthibitisha juu ya wananchi wa Zanzibar vipi mipango yake itakapoanzishwa mamlaka hii. Lengo itaanzisha kuweza kupata maji na atakapotuhakikishia basi nitaunga mkono pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Koani mswada huu baada ya kutoa ufafanuzi pamoja na kutuhakikishia vipi atachukua majukumu ya kuhakikisha Wizara hii itasimamia vizuri nishati ya maji pamoja na mafuta, kwa sababu wananchi wanahangaika sana.

Kwa mfano, wananchi wengi yanapopotea mafuta basi wanashindwa kuleta mazao yao mjini na wanapoleta mjini huwa wanapata hasara kwamba gari wanalipia fedha nyingi kutokana na nishati ya mafuta imepotea.

Nadhani itakuwa ni vizuri kama hivi sasa alivyolisimamia suala la umeme linavyoweza kwisha hapa Zanzibar. Kwa hiyo, alijitolea muhanga kuweza kutoa tamko lake, basi ni vizuri kama atakapokuja leo atueleze kwamba ni lini nishati ya maji itakamilika hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, mchango wangu wa leo ni huu na wala sitokuwa na mengi zaidi, isipokuwa nitaunga mkono hoja pindi Mhe. Waziri atakapolitolea tamko suala hili la maji.

Mhe. Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima na kuweza kutekeleza majukumu yetu kama ambavyo Katiba ya nchi inatuelekeza. Vile vile nikupongeze na nikushukuru Mhe. Spika kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo, ili niweze kutoa mchango wangu mfupi kwenye mswada huu muhimu sana kwa maslahi ya wazanzibari wote na nchi kwa jumla.

Mhe. Spika, niende kwenye sababu na madhumuni. Kwa kweli mswada huu Mhe. Waziri ametueleza kwamba sababu kubwa ambazo leo hii tumeletewa mswada huu ni kutimiza matakwa yale ya Sera ya Nishati ya mwaka 2009. Mhe. Spika, nikubaliane na Mhe. Waziri kwamba Sera ile ya Nishati ya mwaka 2009 iliiagiza serikali kwamba kuwe na chombo kama hichi ambacho kitasimamia kudhibiti masuala ya nishati.

Lakini Mhe. Spika, nikumbushe tu kwamba sambamba na agizo hili sera ile pia iliitaka serikali isimamie upatikanaji wa mafunzo ya watu wetu hasa katika fani hizi za nishati. Vile vile nakumbuka serikali kupitia Wizara hii ya Maji waliwahi kutwambia kwamba wamejiandaa kuwasomesha wafanyakazi wetu wapatao 10 kwenye fani hizi za nishati hususan mafuta na gesi.

Kwa hivyo, kupitia mswada huu wa leo Mhe. Waziri, basi nadhani angetwambia na ingekuwa fakhari kubwa ni wananchi wangapi wazanzibari ambao wamesomeshwa kupitia agizo la sera ile, ili kwenda sambamba na matakwa ya serikali juu ya kuimarisha mahitaji ya wataalamu wetu kwa fani ya nishati.

Mhe. Spika, lakini nimejifunza na nimepata faida kubwa kwamba kumbe serikali kwa yale mambo ambayo wanayataka ambayo yameagizwa na Jumuia ya Afrika ya Mashariki wanao uwezo wa kufanya kazi.

Mswada huu sababu nyengine tumeambiwa ni matakwa ya Jumuia ya Afrika ya Mashariki kwamba nchi wanachama waweze kwenda sambamba na sheria za kusimamia masuala ya nishati, ili kwenda sambamba na Jumuia ya Afrika ya Mashariki. Vile vile serikali hii kwa mambo mengine ambayo hawataki husema sisi si wanachama wa Jumuia ya Afrika ya Mashariki kwa hivyo hatuna haja ya kufanya jambo hilo.

Sasa naomba nijue kwamba labda tayari tumepata uanachama mpya wa Jumuia ya Afrika ya Mashariki, kwa sababu Baraza hili tumetaka mambo mengine yasimamiwe na nchi hii chini ya serikali yetu. Lakini jibu la serikali ni kwamba sisi ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wala hatuna mamlaka, lakini kwa hili mamlaka imepatikana na tumeweza kuweka sheria yetu ya udhibiti ambayo ni sheria muhimu sana kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atuambie sasa kumbe tunao uwezo wakati tunapoamua licha ya kuambiwa si wanachama kamili wa Jumuia ya Afrika ya Mashariki, lakini tunao uwezo wa kuamua mambo yetu ya ndani kwa ajili ya maslahi yetu na vizazi vyetu kama wazanzibari, na kwa nini mambo mengine ya msingi tunashindwa kuamua, yaani tunashindwa kuwa na ujasiri kama huu kwa ajili ya kufikia maslahi yetu.

Nikiondoka hapo sasa naomba niende kwenye kifungu kimoja kimoja na nianze kwenye kifungu cha 3(2)(a) naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 3(2)(a) cha mswada kinaeleza hivi:-

> "(2) Mamlaka itakuwa ni chombo kinachojitegemea na cha kudumu
> chenye muundo wake na kwa kutumia jina lake ina uwezo wa:
>
> (a) kupata, kutwaa, au kutoa mali inayoimiliki au mali isiyohamishika".

Sasa Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atafute neno jengine ambalo ni zuri zaidi na hili kutoa naona halikukaa vizuri kwa lugha ya Kiswahili, basi ni vyema angetafuta neno zuri zaidi tukaweza kuliweka kwa ajili ya kupata neno ambalo wazanzibari wote wa Unguja na Pemba wakaweza kulitumia na lipo kwenye Kiswahili Sanifu.

Mhe. Spika, jambo jengine ni kifungu cha 3(2)(b) naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 3(2)(b) cha mswada kinaeleza hivi:-

"kuingia mikataba na mtu yeyote wa taasisi".

Mhe. Spika, ni vyema kwa sababu huko mbele kuna mswada wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na mswada ule umeamua kujiweka tayari, kwa ajili ya kusimamia mikataba yote ya serikali.

Kwa hivyo, nadhani hapa tungeongeza maneno kwamba jukumu la mamlaka hii kuingia mikataba na mtu yeyote au taasisi, lakini kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, ili kwenda sambamba na mswada wa Mwanasheria Mkuu ambao kesho kutwa utakuja na umejipanga kila jambo ambalo serikali hii, basi lazima lipitie ofisi yake kwa ajili ya mikataba ya nchi hii.

Mhe. Spika, ni vyema tungeongeza maneno hayo kwamba mamlaka iwe inaweza kuingia mikataba, lakini kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, ili kuweza kuweka ule uhalali wa kisheria.

Kifungu chengine ambacho nataka nikuzungumzie ni kifungu cha 4 na naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 4(4) cha mswada kinaeleza hivi:-

> "Mkurugenzi Mkuu atateuliwa na kutumikia Mamlaka kwa kipindi cha miaka minne na anaweza kuteuliwa tena kwa vipindi vyengine vya miaka minne".

Mhe. Spika, nadhani tusiweke muda wa Mkurugenzi, kwa sababu mkurugenzi ni mtumishi wa umma anaweza kufanya vizuri na tukamuhitaji zaidi ya miaka 40, lakini anaweza kufanya vibaya na tukatamani siku moja tumuondoshe.

Sasa nadhani tungeweka wazi na wala tusiweke kipindi cha utumishi wake, ili akiharibu mapema basi tumuondoshe mapema na iwapo atafanya vizuri tuweze kumbakisha kwenye majukumu yake, lakini kumuwekea miaka minne hata kama ameharibu basi sheria imesema asiondoke mpaka miaka minne, maana itakuwa si utaratibu.

Kwa hivyo, nafikiri tuache wazi kabisa kwamba Mkurugenzi ateuliwe na Rais na utumishi wake utaendelea kama vile Rais atakavyoona na akiharibu tuweze kumuondosha na kama atafanya ufanisi mzuri basi tuweze kumrejesha siku hadi siku.

Vile vile kifungu cha 4(5) naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 4(5) cha mswada kinaeleza hivi:-

> "Rais kama akiona ipo haja anaweza kuteua Naibu Mkurugenzi Mkuu".

Mhe. Spika, nadhani maneno haya yaondoke na kama kuna haja ya kuwepo basi tuseme wazi tu kwamba Rais atateua Naibu Mkurugenzi na pia tumuwekee sifa zake kama alivyo Mkurugenzi, lakini tukisema kwamba ataweza kuteua nadhani watu wanaweka kifungu hichi kwa ajili kutafuta ajira ya mtu na tumekuwa tukisema wazi kwamba tusitunge mswada kwa kumuangalia mtu. Kwa hivyo, tuamue wazi kwamba Rais atateua Naibu Mkurugenzi na tumuwekee na sifa na kama hakuna haja hiyo basi kifungu cha 5 kiondoke na wala tusiweze kujifunga.

Kifungu cha 4(6) cha mswada naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 4(6) cha mswada kinaeleza hivi:-

> "Mkurugenzi wa Idara atateuliwa na Bodi kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma na kanuni zake kwa kipindi kitakachoainishwa katika barua ya uteuzi".

Mhe. Spika, sina tatizo na uteuzi wa Mkurugenzi wa idara. Lakini naomba nitahadharishe kwamba tusije tukatumia mwanya huu tukawa na utitiri wa idara katika mamlaka hii, kwa sababu sheria hapa imesema kuwa ni bodi itateua idara za mamlaka na tusije tukapata mwanya huo na kuamua kuteua idara nyingi kwa maana tuka-*create* ajira ambazo hazina umuhimu huo.

Kwa hivyo, nadhani nitoe tahadhari kwamba tuteue idara ambazo zinaendana na majukumu yenyewe ya mamlaka tuliyoainisha na isijekuwa ni mwanya wa kuanzisha idara nyingi kwa ajili ya kupata ajira na wala hakuna ulazima wa suala hilo.

Kifungu cha 6(1) kuhusu muundo na muda wa bodi naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 6(1) cha mswada kinaeleza hivi:-

> "Bodi ya Wakurugenzi itakuwa na wajumbe saba ambao wataitumikia Bodi kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine cha miaka mitatu. Isipokuwa kwa Mwenyekiti wa Bodi, ambaye ataitumikia Bodi kwa kipindi cha miaka minne na anaweza kuteuliwa tena".

Mhe. Spika naomba tumalize hii sentensi ya mwisho, kwamba kuteuliwa tena iwe kwa kipindi chenyewe cha miaka minne. Kwa kweli hivi ilivyo tunaweza tukamteua miaka minne, minne, minne na tukafanya bodi ya mtu mmoja kwa

miaka zaidi ya 40. Kwa hivyo, nadhani maneno ya mwisho hapo tuyakamilishe na tuseme kwamba anaweza kuteuliwa tena kupitia kwa kipindi chengine cha miaka minne.

Vile vile kifungu chengine ambacho nataka kutoa mchango wangu ni kifungu cha 8(3) kuhusu suala la umeme naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 8(3) cha mswada kinaeleza hivi:-

(3) Umeme:

- "kusimamia uwekaji na utiaji wa umeme". Kwa mswada wa Kiingereza imeandikwa *control, installation and fitting*".

Mhe. Spika, sasa ZURA itakuwa na jukumu la kufunga na *installation* na *fitting* kama kwamba jukumu la *ZECO* la kufanya *fitting* imeshindwa. Kwa hivyo, nadhani hii isingekuwa kazi ya ZURA kwamba sasa isimamie na ifanye mpaka *fitting* za kwenye nyumba na hii si kazi ya ZURA. Mhe. Spika, nafikiri ni vyema Mhe. Waziri angetufafanulia na tukaweza kuona hiyo hali halisi ilivyo.

Kifungu cha 9(a) cha mswada naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 9(a) cha mswada kinaeleza hivi:-

"Kutumia viwango vya bidhaa na huduma zilivyotengenezwa na *ZBS*".

Mhe. Spika, hii nadhani imewekwa kijumla jumla kwamba hata kama tungeandika hapa bidhaa hizo zile ambazo zinahusiana na mafuta, maji na umeme na hivi ilivyo kwamba *ZBS* ikithibitisha kuwa hichi kina kiwango hata doti za kanga maana yake hii iko wazi sana. Kwa hivyo, nashauri Mhe. Spika kuwa bidhaa hizo ni zile zinazohusu mafuta, maji na umeme.

Jambo jengine ambalo nataka kulichangia kwa haraka ni kifungu cha 21 Mhe. Spika, naomba kunukuu kidogo.

Kifungu cha 21 cha mswada kinaeleza hivi:-

"Wajumbe wa Bodi watalipwa maslahi na posho kama inavyoelekezwa na Bodi na kukubaliwa na Mhe. Waziri anayeshughulikia masuala ya fedha".

Mhe. Spika, tumezoea kwamba Waziri wa wizara husika ndiye anayepokea mapendekezo ya bodi juu ya maslahi ya wajumbe wa bodi. Lakini hapa imewekwa kwamba Waziri wa Fedha ndiye atakayekubaliana na mapendekezo ya bodi. Nadhani Mhe. Spika, mimi nikubaliane na wazo hili. Kwa nini?

Zipo baadhi ya bodi wamekuwa wakilipana maposho kwa kujiandalia maslahi binafsi. Kumekuwa na mtiririko mkubwa wa maposho yasiyokuwa na sababu. Nadhani serikali imeona kwamba waziri wa fedha ndiye atakayepima hasa je, posho hizi zinastahiki kwa wajumbe wa bodi. Kuna bodi wanapeana maposho kiholela, wana *create* vikao kiholela. Kwa hiyo Waziri wa Fedha sasa akiridhia kwamba posho hili ni la msingi nadhani kifungu hiki mimi niwashawishi wenzangu kwamba tukubali sasa kwamba tumnyang'anye Waziri wa Nishati mamlaka haya na tumkabidhi Waziri wa Fedha mwenyewe ili awapangie wabumbe wa bodi maposho na maslahi. Vyenginevyo zipo baadhi ya bodi wanapeana pesa kama njugu, jambo ambalo si matumizi mazuri ya pesa za umma na si utawala bora. Kwa hivyo mimi nakubaliana na hili na Waziri wa Fedha aridhike kwamba maposho haya na maslahi haya yanastahiki kwa kulipwa wajumbe wa bodi kwa mujibu wa muongozo wa sheria za fedha.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba kifungu cha 22(1) (a) fedha zinazotolewa na serikali, nadhani tuongeze maneno kwamba fedha zinazotolewa na serikali baada ya kuidhinishwa na Baraza la Wawakilishi, kwa sababu fedha ya serikali ni lazima ipitie Baraza la Wawakilishi, naomba tuongeze sehemu hii. Hapo hapo kifungu cha 21, 22(1) (d) nadhani kitakuwa hakina haja kwa sababu fedha ile ya serikali ambayo itapelekwa kwa ZURA tayari itakuwa imewasilishwa katika kifungu cha 22(1) (a).

Mhe. Spika, kifungu chengine ambacho ningesema kwamba kuna suala la kifungu cha 31 Baraza la kuwakilisha wateja. Mhe. Spika, linaanzishwa Baraza litakalojulikana kama Baraza la kuwakilisha wateja. Kifungu cha 2 Baraza litaongozwa na Mwenyekiti na wajumbe wasiopungua watano na wasiozidi saba litakaloteuliwa na Waziri kutoka kwenye taasisi zinazotambulika kisheria kuwa zinawakilisha maslahi ya sekta binafsi sehemu nyengine za umma kama waziri anavyoona inafaa.

Mhe. Spika, mimi naungana kabisa na wenzangu kwamba kifungu hiki kisipewe mamlaka kwa waziri kwa sababu itakuwa hakuna tofauti. Kifungu hiki lengo lake ni kuwatetea wateja wakiwemo wananchi mmoja mmoja. Sasa tukimpa waziri ndio ateuwe wajumbe hawa nadhani tutakuwa hatuwatendei haki wateja mmoja mmoja. Naomba wenzangu wawakilishi tukubaliane kwamba kifungu hiki wateja wenyewe wateuwe wenyewe kwa utaratibu

utakaowekwa mzuri, wateuwe wenyewe wajumbe wao watakaowawakilisha hawa ndio watetezi dhidi ya ZURA na dhidi ya maslahi ya serikali.

Mhe. Spika, nadhani Waziri hapa tusimpe madaraka ya kuteuwa hawa watu, vyenginevyo itakuwa tumewalimbilikizia mzigo mkubwa wananchi wa kawaida ambao watumiaji wa nishati hizi ambazo ni muhimu sana.
Mhe. Spika, mwisho kabisa kwa mswada huu niseme tu kwamba kuna suala la kifungu cha 53 naomba nikinukuu.

Kifungu cha 53 "Mamlaka itakuwa na uwezo, majukumu, kazi na wajibu iliowekwa na Sheria hii, endapo kutakuwa na mgogoro, mgongano baina ya Sheria za kisekta, Kanuni au taratibu, Sheria hii ndiyo itakayotumika hadi pale Waziri, pale atakapoelekeza vyenginevyo"

Mhe. Spika, nadhani kazi ya Baraza la Wawakilishi ni kutunga sheria na si busara na wala si utawawala bora kwamba Baraza limetunga baadaye waziri akiona kuna mgongano yeye amue vyenginevyo. Nadhani tufute maneno yote yale ya mwisho na sheria hii na kifungu hiki kisomeke kama ifuatavyo:

Mamlaka hii itakuwa na uwezo, majukumu, kazi na wajibu uliowekwa na sheria hii endapo kuwakuwa na mgogoro, mgongano baina ya sheria za kisekta, kanuni au taratibu, sheria hii ndiyo itakayotumika. Nadhani maneno hayo yabakishe hapo ili sasa isije kuwa kazi ya Baraza la Wawakilishi kutunga sheria, hatimaye waziri atakapoona kuna mgogoro akaamua vyenginevyo, itakuwa tumeingilia mamlaka mengine ndani ya nchi na itakuwa si utawala bora.

Mhe. Spika, hapa tusimpe waziri mamlaka makubwa akaja akayakiuka mamlaka ya Baraza la Wawakilishi ambayo si mamlaka yake. Niseme tu kwamba nimshauri Mhe. Waziri kwamba wajumbe wanapodai kupatiwa semina, isionekana kwamba wanadai kupokea posho.

Mhe. Spika, nataka niwakumbushe wajumbe wanzangu kwamba mwaka juzi, tulipitisha sheria ya Mamlaka ya Maji na tulikubaliana hapa kwamba nyumba za Ibada (Misikiti) visima binafsi visitozwe malipo yoyote. Hivi leo misikiti tayari Pemba kuna malipo ya maji, nina ushahidi ni jambo ambalo ni kinyume na makubaliano yetu. Lazima atukae kitako na waziri na wataalamu wake, tuelimishane sheria hii imemlenga nani. Ili Baraza hili lisipitishe sheria zikawakwaza wananchi hatimaye ikawa malalamiko. Hivi leo nyumba binafsi na visima binafsi, hivi leo Misikiti nyumba za ibada, wananchi wanatozwa kodi fedha nyingi za maji wakati maji yenyewe hakuna. Lazima tukae

tuelimishwe hatimae tukubaliane kwamba sheria hii imekusudia nini kwa maslahi ya wananchi wetu wanyonge wa Zanzibari.

Niseme tu kwamba unapoamua kuweka leseni kila hala, maana yake unaongeza kodi kwa wanachi wetu wanyonge. Wasiwasi wangu kwamba sheria hii ikipita hata visima vyetu vya asili huko vijijini basi tayari vitakata leseni, hiyo maana yake kodi na gharama za maisha zinapanda kwa wananchi wetu. Kwa hivyo tusiwe rahisi kupitisha mswada huu mpaka pale Waziri atakapokubali kukaa na sisi tukaelimishana nini madhumuni ya Mswada huu kiundani na ili tuweze kufanyia haki Wazanzibari wetu.

Si jambo la ajabu Mhe. Spika, tuliwahi kupitisha sheria hapa, tukaahirisha, tukaelimishana zaidi kwa semina. Serikali imekaa na nia hii tangu mwaka 2009 hatimae miaka mitatu ndio tukaletewa Mswaada, Sisi tumeletewa Mswada huu miezi miwili nyuma, kwa hivyo si jambo la ajabu.

Mhe. Spika, ushauri wangu Mhe. Waziri akubali kwamba tukae kama Baraza tufanye semina ya kuelimishana madhumuni ya ndani yaliyokusudiwa kwa kina ili wananchi wetu wasije wakapata athari huu ya mswada huu muhimu, vyenginevyo isijekuwa kwamba Mswada huu unakusudiwa kuandaliwa wafanyabiashara fulani kwa ajili ya mafao yao ambayo yatatuathiri hatimaye kwa ustawi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya hapo Mhe. Waziri akinijibu maswali yangu muhimu nitaunga mkono mswada huu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, Mswada huu ambao tunaujadili hapa tunategemea kuwa utaletwa na Waziri wa Fedha au Waziri wa Biashara. Siku zote nilikuwa nikisema hapa panakuwa na migongano ya taasisi tatu au wizara tatu au idara tatu. Wizara ya Fedha ndio inayokusanya mapato haya yote ya mafuta. Waziri nimpe pole na mizigo anayojitwika hii ambayo ni mizito na sifikirii kama tutafika kwa mwenda huu tunaokwenda. Tutakuwa tunaendelea kuwatesa wananchi wetu tu.

Leo migogoro tuliyokuwa nayo kwenye Wizara ya Ardhi haisemeki, maji ndio watu wameshaota vipara, wameshafanya suguru, wameshasamehe, umeme ndio hausemeki kabisa, mpaka Mhe. Balozi shahidi alivyokwenda Pete. Mimi nilikuwa nafikiria sheria nyengine zilizokuwa hazina haja ziletwe hapa tuzifute, tusiwe tunaongeza mizigo juu ya mizigo.
Mhe. Spika, nije kwenye kifungu cha 6, naomba nikinukuu kama hivi ifuatavyo:

Kifungu cha 6 “Bodi ya wakurugenzi itakuwa na wajumbe saba ambao wataitumikia bodi kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine cha miaka mitatu, isipokuwa mwenyekiti wa bodi ambaye atatumikia bodi ya kipindi cha miaka mine anaweza kuteuliwa”

Mhe. Spika, kwa kushangaza hapa kuna sheria, Mwanasheria Mkuu anaweza kutusaidia ambayo imetungwa sheria Nam. 4 ya mwaka 2002 tunapitisha sheria wenyewe. Tunafanya nini, tunatunga sheria miaka mitatu huyu akae na huyu akae miaka mine, uhalali uko wapi? Hatuwezi kwenda namna hii. Tunatunga sheria halafu tunazigeuza wenyewe.

Mhe. Spika, nije Kifungu cha 8, kutakuwepo na chombo cha usimamizi wa sekta ya petroli na gesi, tatizo. Ukiangalia sekta ya maji chombo mahususi hichi kiliundwa kwa sheria Nam. 4 ya mwaka 2006 ZAWA, jina limebadilishwa, huduma ndio ile ile, hakuna kinachopatikana hata kimoja hivi sasa.

Mimi Mhe. Waziri huwa nampigia simu mara nyingi lakini huwa hapokei, mimi sihitaji kiwanja wala kitu gani, mimi nina matatizo jimboni ya maji na natumia gharama zangu mwenyewe Mhe. Waziri. Wale wananchi wangu mimi nimechukua jukumu la kuwatumikia, wananchi wanaumia kule. Hivi sasa Muyuni hakuna maji, pampu imeharibika, nimekwenda kuripoti mara tatu mara nne na wala hakuna lolote lililokuwa.

Sekta ya umeme ndiyo hiyo mizigo juu ya mizigo, huku wengine wapate, wengine hawapati, nguzo ikianguka miezi mitatu haijahamishwa. Hao wanaolipa huduma kwenda kuungiwa umeme haisemeki, hicho kinakuwa kitendawili. Pesa zipo umeshalipa mtu na risiti unazo.

Nije kifungu cha 11(g) uwezo wa wajumbe wa Mamlaka kupanga bei, nataka kujua Mamlaka hii tunayotaka kuianzisha hapa ni ya udhibiti au uendeshaji, kama ya udhibiti kwa nini ipange bei ya huduma zinazodhibitiwa, hii ni kinyume na sera ya soko huria na itaingilia uhuru wa wafanyabiashara, mafuta, maji na umeme kupanga bei. Mimi nadhani kifungu hiki kisomeke ni kudhibiti bei.

Kifungu cha 50, Mamlaka itaweka kanuni ya kuendesha shughuli zake. Naona tayari maelezo ya kifungu hiki yamo kwenye kifungu cha 48, kinachoeleza utungaji wa kanuni. Maelezo yanafuata kifungu cha 50 yanasema itahakikisha mamlaka ya sekta zinazozibitiwa zitafanya shughuli zake kwa njia za uwazi.

Maelezo hayo tayari yapo kwenye kifungu cha 27 ambacho kinahusu uwazi wa taasisi zinazotolewa kwa huduma na hivyo hapa kimerejewa tena.

Mhe. Spika, kwa hayo machache sitounga hoja hii mpaka nitakapopata maelezo.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipatia fursa hii ili na mimi nichangie machache katika Mswada huu. Kwanza kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kutuletea Mswada huu kwa wakati muwafaka kabisa.

Mhe. Spika, wenzangu wameshasema mengi juu ya mswada huu na yenye umuhimu kabisa, mimi nitachangia angalau machache ili na niweze kuwa nimechangia Mswada huu. Kwanza kabisa nilitaka nianze kwenye madhumuni au sababu ya kuletwa Mswada huu. Nianze katika kifungu kidogo hichi ambacho kinasema kuwepo kwa mamlaka hii kutasaidia sana kuzuia ongezeko la bei kwenye huduma hizo na pia kusimamia ubora wa huduma inayotolewa kulingana na viwango vilivyowekwa na sheria hiyo.

Mhe. Spika, madhumuni ya Mwada huu yanatupa matumaini makubwa, ingawa kwa sasa inaonekana bado huduma ingali hafifu, lakini tunapata moyo mkubwa wa kuona mamlaka sasa itajipanga vizuri na kuweza kutupatia huduma hizi. Nianze mchango wangu katika ufafanuzi, nende kwenye neno mteja.

Mhe. Spika, naomba ninukuu hapa kidogo “mteja maana yake ni mtu anaestahiki kupewa huduma muhimu kwa mujibu wa sheria hii au sheria nyengine yoyote ya huduma muhimu”

Mhe. Spika, labda mimi niseme ufafanuzi huu kama utatumika kama ulivyofafanuliwa hapa basi mamlaka hii inaweza ikafanya kazi moja nzuri. Waswahili wanasema mteja ni mfalme, sasa iwapo mteja ataweza kupatiwa huduma zilizobora na zikawa zinaonekana sidhani kama mteja huyo anaweza tena akawa mbishi wa kulipa juu ya huduma hizi.

Mhe. Spika, kinachosababisha mgongano na mgogoro ni ile kuona mteja ile huduma yenyewe haipati halafu wenye kutoa huduma wanafika kumdai. Hapa ndio unapokuja mgongano, lakini kama mteja atashughulikiwa ipasavyo basi naamini wazi Mamlaka inaweza ikafanya kazi moja nzuri.

Mhe. Spika, mimi niende na huyu huyu mteja kwa sababu mteja na mtu muhimu bila ya kuwepo mteja utakuwa huna wa kumuuzia. Kwa hiyo mimi

nilitaka hawa wateja tuweze kupatiwa elimu ambayo linapotokezea jambo ambalo hatulifahamu maana yake ni vizuri ukamuelewesha mteja wako ili akafahamu vizuri na ikakosekana hiyo migongano. Lakini pia na watoa huduma Mhe. Waziri namba serikali ichukue jukumu la kuwapa elimu watoa huduma ili waweze kuwahudumia wateja katika hali iliyo nzuri ambayo itakuwa ina lugha nzuri ya kupendezesha na ambayo hali hiyo pia itasababisha sisi kufika katika ushindani wa masoko.

Hivi sasa Mhe. Spika, tunafanya kazi kwa mazoea tu bila ya kuwa na ujuzi wowote unaoweza kutusaidia. Tunaona wenzatu katika mambo haya ya kibiashara wana huduma za kumbembeleza sana mteja ili waende sambamba na kusitokee migongano. Mimi namsihi sana Mhe. Waziri elimu ni kutu muhimu juu ya wateja wenyewe lakini na wale watoa huduma ni vizuri na wao wakawa wanapatiwa elimu ya kuelimishwa vipi waweze kuwa na lugha nzuri kwa wateja wao ili isitokee migongano.

Mhe. Spika, jengine wenzangu wamesema sana hapa lakini mimi sitaki niseme sana, nataka nichukue muda mdogo tu kwani mambo mengi yameshasemwa, tusirudie hayo kwa hayo. Napenda niiombe sana serikali juu ya usimamizi wa sheria hizi ambazo tunazitunga kila mara. Kwa sababu bila ya usimamizi mzuri hatuwezi kufika halali popote.

Tunasema kama kwenye vyanzo vya maji kunatokea watu wanajenga majumba kiholela bila ya kujua athari. Lakini serikali ipo na inaona na haichukui hatua yoyote. Mtu ataanza kujenga tangu msingi, hachukuliwi hatua huyo ya kumsimamisha kujenga mtu yule mpaka atajenga nyumba mpaka ahamia. Kwa hivyo hichi ni kitu cha kuzingatia sana, maana inakuwa baada ya kuziba ufa unakuwa sisi tuje kujenga ukuta mzima.

Mhe. Spika, mimi Mhe. Waziri nilikuwa namuomba sana tuangalie sana usimamizi wa sheria yetu hii. Kwa sababu haya ni mambo ya huduma za wananchi, kwa hivyo tunatakiwa tuzichunge vizuri ili tuwe na manufaa mazuri.

Kuna umeme, mafuta katika Sheria hii. Mhe. Spika, kwanza na mimi nichukue fursa hii nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kusimia tukaweza kuondokana sana na huu mgao wa umeme. Tunashukuru sana. Pia ni nikisema siku zote huwa napenda kutoa mchango wangu juu ya mjenzi na mjengewa, serikali ndio mjenzi wetu anayetufanyia huduma hizi.

Ningependa kuwasisitiza sana wananchi kwamba sisi wajengewa basi tuweze kwenda sambaba na malengo ya serikali yetu. Kwa sababu huu umeme tunaweza kuwalaumu labda watu wa Shirika la Umeme hatupati huduma

nzuri, hatupati hivi, hatupati hivi. Lakini na sisi wateja wenyewe ukiangalia na sisi tunakuwa tunakwenda kinyume saa nyengine, saa nyengine tunakuwa wezi, tunaliibia shirika. Sasa shirika haliwezi likawa linamiujiza ya kuzalisha wakati sisi wenyewe tunafanya ubadhilifu. Kwa hivyo tuende sambamba, tuwe waaminifu na serikali itutendee yale ambayo inapaswa kuwatendea wateja wake.

Mhe. Spika, pia nimkumbushe waziri kwamba mamlaka hii iweze kutoa taarifa kila pale linapojitokeza tatizo. Limezungumza hapa kwamba wateja ni watu muhimu. Tunakosa huduma halafu serika imekaa kimpa yaitwambii chochote pia roho kwa wateja zinafinyika kuona huduma hatupati na hatupati maelekezo yoyote kwamba nini kimetokea mpaka ikawa huduma hii tunaikosa.

Mhe. Spika, mimi huwa sina mengi ya kusema, nahisi nitauchukua muda tu bure, haya ninayoyasema yote nahisi yameshasemwa na wenzangu. Mimi nilitaka niunge mkono Mswada huu kwa asilimia 100, lakini nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba hizi sheria tumekuwa tukizitunga na kuzileta hapa kila mara lakini utekelezaji wake unakuwa wa kusua sua.

Mhe.Spika, baada ya kusema hayo napenda kuunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, na mimi baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima, tukaweza kushiriki katika kikao chetu hichi, naomba nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa ya kuchangia na mimi mchango mdogo katika hoja hii ya Mswada wa kuanzisha mamlaka ya udhibiti wa huduma za maji na nishati.

Pili naomba na mimi niungane na wenzangu kumshukuru sana na kumpongeza Mhe. Waziri na Wizara yake kwa ujumla kwa kufanya maandalizi hayo ya Mswada huu muhimu. Wenzangu waliotangulia kueleza wamesema umuhimu wa Mswada huu na mimi sitaki niyarejee tena.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu ni katika maeneo matatu tu. Nia ni kusaidia waheshimiwa katika kuupitisha Mswada labda kuna baadhi ya mambo kusaidia mawazo kwa namna sisi tuliufahamu, pengine na wao inaweza kusaidia kufahamu yale madhumuni au baadhi ya mambo ambayo yamezungumzwa. Katika hilo kwanza niungane na wenzangu kusema kwamba kwa kweli ingependeza huu Mswada watu wakapata taaluma ya jumla kuhusiana na suala hili la udhibiti wa sekta hii. Kwa sababu ya umuhimu wa sekta yenyewe.

Lakini la pili ni kwamba nadhani kwa mara ya mwanzo ambayo tunaanzisha chombo hichi cha udhibiti. Nadhani tulipitisha sera hapa na pia suala la udhibiti kwa uzoefu wa nchi za wenzetu limezoeleka sana, waheshimiwa wajumbe naamini wengi watakuwa wanafahamu na ndio maana wakasema kwamba huu Mswada ni muhimu sana. Nadhani kama tungekuwa na fursa hiyo bahati mbaya tumeshafika nao mbali basi ingeweza pengine kutusaidia sana na mengi mengine ambayo yameelezwa pengine yasingeelezwa.

Mhe. Spika, mimi nizungumzie la jumla kwanza lile ambalo amelizungumza sana Mhe. Ismail Jussa, kuhusiana na Mamlaka ya Udhibiti wa hichi chombo kudhibitiwa zaidi na Waziri. Yeye alitoa mifano mingi. Hoja yake kiukweli ina msingi, inavyoonekana kwamba biashara mbili kumbwa mpaka sasa zinafanywa na serikali, ile ya maji kupitia mamlaka ya maji na ile ya umeme kwa kupitia Shirika letu la ZECO. Labda hii ya mafuta bahati nzuri tokea ilipoanza imebinafsishwa imefanywa kwa sehemu kubwa na makampuni mbali mbali. Sasa yeye anasema itakuwa kama serikali inakuja kujidhibiti wenyewe.

Mhe. Spika, mimi naomba wenzangu labda walione kwamba hili suala la kuanzisha sheria ya Udhibiti, hili ni sehemu ya mchakato wa kuelekea katika kutoa huduma nzuri zaidi katika maeneo haya ya huduma hizi. Wataalamu wana msemo wanasema kwamba mlinzi mkubwa wa watumiaji au mlinzi mkubwa wa wateja ni ushindani. Bila ya kuwa na ushindani kwa kweli huwezi kuwa na ulinzi wa watumiaji. Sasa hii sheria kwanza tuiyone la muhimu inaelekea kuanzisha ule mchakato wa kujenga ushindani katika hizi sekta ambazo zinatolewa huduma.

Mhe. Spika, sasa tumefika pahala tunaanza huu mchakato, bahati mbaya huo ushindani wenyewe haujaja. Sasa katika mazingira hayo, maana ni lazima uwe na kitu ambacho wenzetu nao wengi walipita katika mchakato kama huo na sisi naomba niwahakikishie weheshimiwa wajumbe kwamba tumesoma kutokana na wenzetu ambao wamepita katika mchakato kama huo. Yale ambayo wameyaona, utaratibu ambao wameufuata na sisi ndio ambao tumeutumia uzoefu huo katika kufikia hapa ambapo tumefikia. Lamsingi tukiliona hilo nadhani litatusaidia kuifahamu hii hoja. Kwamba hii hoja si kwamba mchakato wa kuanzisha ZURA tu, bali ZURA ni sehemu ya mchakato mrefu wa kuanzisha utaratibu wa kuleta ushindani katika kutoa huduma hizi ili mhudumiaji apate nafuu,ili mtumiaji apate ulinzi.

Tulipokuwa na simu hapa za *Tanzania Postal and Telecommunication*, kwanza kupata simu yenyewe ilikuwa mpaka upange foleni, wakati mwengine miaka mitatu, mine ndio upate line. Ukiipata ndio ilikuwa shida hiyo hiyo. Hata ile huduma yenyewe kuipata ukapige foleni kwa jirani,

ushaambiwa unapigiwa simu pengine kama ni ishaa basi ishaa uikose unasubiri simu. Lakini sasa tumeona serikali ilianza yenyewe mchakato wa kuleta sheria ya kuruhusu makampuni binafsi kufanya biashara hii na watu wamekuja wamewekeza, wengine ulikuwa mtu unajiuliza hawa wataweza, watapata soko wapi wakati ile *Tanzania Postal Telecommunication* ilikuwa imeenea mtandao wake kila pahala. Lakini pamoja na ukubwa wote ule imepukutika kidogo kidogo mpaka sasa hivi imebaki kama ilivyo, watu wamepata nafuu si kwa sababu serikali imeleta nafuu ile lakini nafuu ile inayopatikana sasa hivi imeletwa na ushindani. Sasa na hii sheria madhumuni yake makubwa ni kuweka utaratibu wa ushindani. Yale yanayoonekana kama labda ni mamlaka makubwa ya serikali ndio kwa sababu ya hapa tulipo sasa hivi.

Mhe. Spika, historia ya udhibiti wa huduma hizi wenye historia kubwa, na dunia imesoma sana kwa Waingereza. Waingereza kwa mfano mpaka mwaka 1983 walikuwa na Kampuni moja tu ya simu BT, Kampuni moja tu ya reli, British Railway, Mamlaka moja tu ya maji. Lakini walivyoanza na wao walianza ku-*regulate* mwanzo na baada mwaka 1984 wakabinafsisha Kampuni yao ya simu BT, wao walipoanza hawakutaka hata kuunda kwanza chombo walikuwa na ofisi moja ya kudhibiti ushindani wanaita *Office of Fair Trade* wakasema kwamba ile kazi ya kudhibiti iende kule, *Office of Fair Trade* wakasema aa sisi hatuwezi kazi hiyo ni kubwa waingereza ndio maana wakaunda ofisi wanaita *Office of Telecom Oftel*, *Oftel* kazi yake ilikuwa ni kudhibiti suala la biashara au ushindani katika biashara ya simu.

Lakini walichofanya baada ya *Oftel* kuianzisha mamlaka makubwa yalibaki kwa Waziri hata ile kutoa leseni mamlaka yale yalibaki kwa Waziri wa Biashara na yeye kwa kushauriana tu na ile Ofisi ya *Oftel* na mambo mengi ya msingi yalibaki mikononi kwa Waziri kwa sababu gani wana kitu katika wanasema katika *regulation* ya *transition* kama hivi kipindi hiki cha mpito unapo-*regulate* huduma muhimu kama hizi linaweza likatokea jambo ukafeli, kwa sababu huyu anaye-*regulate* ni mpya na hawezi kuwa na *sensitivity* hawezi kuona yale ambayo raia yanawakuta kwa hivyo wana kitu wanakiita *sale safe provision* yaani kuweka vifungu au mfumo ambao utazuia usilete mtikisiko mkubwa.

Lakini sababu ya pili Mhe. Spika, ya udhibiti kubaki kwa Waziri ni kwa sababu kusema kweli haya mambo tumekwenda tu kinyume kinyume. Lakini kazi ya msingi ya serikali kupitia Waziri ni hii kazi ya kufanya *regulation* yaani kudhibiti sio biashara tunasema ile *sovereign function* ya serikali yaani kazi ya msingi hasa ya serikali ni haya masuala kuwachia watu wafanye biashara wewe serikali kazi yako udhibiti, uhakikishe kwamba hakuna mtu anayeumizwa, hakuna mtu ambaye anatumia uwezo wake katika biashara

vibaya. Sasa sisi serikali tunafanya biashara hili la *regulation* ndio linakuja sasa hivi, kwa hivyo kusema kweli ni kwamba hili la *regulation* hasa ndio ambalo serikali inatakiwa iwe na mamlaka, hili la kufanya biashra linatakiwa litoke mikononi mwa serikali.

Sasa huu mchakato wa mpito ndio huu kwamba hii sheria itawezesha hayo mambo mawili. Serikali ibaki na udhibiti atakayeweza kuingia katika kutoa huduma au kufanya biashara hii aingie na serikali ibaki kumdhibiti. Kwa hivyo hiyo kusema kwamba aa serikali labda itabaki na mamlaka ya udhibiti ni kipindi cha mpito, lakini hapa tutatoka na tutafika pahala anayeweza atakuja kutoa huduma ya umeme au atafanya biashara kutoa huduma ya umeme kama ni ku-*supply* kama ni kuzalisha umeme na *technology* ya kuzalisha inabadilika, wapo watakaoweza kuzalisha kwa upepo, watakaozalisha kwa jua, watakaozalisha kwa gesi, watakaozalisha kwa kitu gani sasa hao lazima uwadhibiti katika uzalishaji na bei ambazo watatoza.

Kwa hivyo mimi ninawaomba sana wenzangu tuone kwamba yale mamlaka aliyonayo Waziri ndio hasa mamlaka ya serikali, haya mengine haya yapo serikalini kwa mpito maadam serikali tumeshaamua ku-*engage gear* ya kwamba aa tuyawachie anayetaka, anayeweza afanye hii biashara basi haya yatabaki ni ya mpito kama wenzetu kama wenzetu walivyopita wengine vile vile. Lakini tutafika pahala serikali itabaki katika udhibiti na biashara itafanywa na watu wengine kama serikali itaweza kuendelea kumudu ushindani fahuwa, lakini kusema kweli la msingi ni hilo.

Lakini hata hili kwa mfano Mhe. Spika, utakuta kwamba kile kifungu kinachozungumzia ile mamlaka ya kumlinda mtumiaji, Waziri anateua lakini baada ya kuletewa majina kutokana na watumiaji, yeye atatangaza jamani nataka kuteua watu, halafu analetewa majina ambayo majina yale baada kushauriana ndio ambayo atateua yeye. Kwa hivyo yote haya ni kuweka utaratibu ambao utamuwezesha Waziri kuweza kuwashirikisha watumiaji wengine katika kupata chombo cha kuweza kuwalinda hawa watumiaji.

Mhe. Spika, la pili nizungumzie kidogo tu aliuliza Mhe. Mahmoud hapa kwamba aa katika hili tumesema nini maana ya nia njema kwamba mtumishi wa mamlaka kama atafanya jambo kwa nia njema basi sheria inamlinda. Nadhani kifungu hiki kinakuwepo katika takriban sheria nyingi ambazo zinaanzisha mamlaka. Hakuna sheria ambayo imetafsiri nia njema lakini kuna mifano mingi ya kisheria na kesi nyingi za kisheria ambazo zimeshatafsiri nini maana ya nia njema. Kwa hivyo huwezi kuipata kwenye sheria hii tunayotunga hapa Barazani lakini inapatikana katika tafsiri za sheria. Na tafsiri za sheria *common* zilizopo yaani nia njema yaani *good faith* inategemea na mazingira yenyewe kwanza ndio maana huwezi kuitafsiri humu. Kwa

sababu ili kujua kuna ni njema unatazama yale yaliyotokea kwanza, mazingira yaliyotokea halafu unaamua aa hili ulilifanya kwa nia njema hukuwa na nia ya kumkomoa mtu, hukuwa na nia ya kujipatia kipato, hukuwa na nia ya kutumia mamlaka yako vibaya, haya yote ni katika mambo ambayo yanazingatiwa katika kutafsiri nini maana ya nia njema.

Lakini naomba nimhakikishie Mhe. Mahmoud kwamba tafsiri yake kwa Kiingereza wanasema ni *well establish* yaani imeshatafsiriwa na inajulikana lakini si vizuri kuiweka hapa kwenye sheria kwa sababu tafsiri yake itategemeana na mazingira mbali mbali ndio uweze kupata hiyo tafsiri.

Jengine Mhe. Hamza alisema kwamba labda ile nafasi ya *deputy DG* au Naibu Mkurugenzi Mkuu kwamba pengine bora isiwepo kwa sababu imeandikwa anaweza Rais lakini tunasema kwamba hili suala la kwamba Rais imewekwa *provision* ile ni kwamba yanaweza yakatokezea mazingira, sasa hivi pengine hatuwezi kuyaona kwa sababu hii kazi ndio kwanza inaanza. Lakini inaweza ikafika pahala sote tukakubaliana kwamba kwa kweli sasa hapa Mkugurenzi Mkuu anahitaji apate msaidizi. Sasa ndio maana tukasema aa sheria isiamue kulazimisha iseme itakapotokea kuhitajika basi ateuliwe wakati huo, kuliko kwamba anahitajika halafu tukaanza kutumia Katiba kumteua Mkurugenzi Mkuu na ndio maana unakuta sheria nyingi zinazokuja sasa hivi zinaweka kifungu hiki kama ni akiba kwa sababu si vizuri wakati una sheria inaanzisha taasisi halafu unapotaka kuja kumteua mtu ukatumia Katiba, kwa hivyo ndio maana tunasema kwamba aa hii ni akiba ya maneno itakapohitajika basi kinaweza kutumika. Ipo mifano mingi ambayo sheria inazungumza hivyo na haikuhitajika na inaendelea bila ya kuwa na Naibu.

Lakini jengine hili la kwamba labda hii nafasi hizi za hawa Mkurugenzi Mkuu zisiteuliwe na Rais, mimi nadhani ni mawazo ambayo tunasema mawazo ya kimaendeleo kwa huku tunakoelekea. Lakini tu pengine wakati wake kwa kuitekeleza si vizuri kulitekeleza kwa kupitia sheria hii kwa sababu hizi nafasi ni nyingi, kama tunaamua tusiamue kwa hili hii ni kazi ambayo nina hakika na ninaelewa kwamba Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma inalifanyia kazi kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utumishi kwamba nafasi zipi labda zinahitajika kuteuliwa na Rais, zipi pengine zitahitajika kwa sifa zake kutafuta watu kwa utaratibu huu ambao anaupendekeza Mhe. Hamza, lakini hata lile suala kwa mfano masuala ya posho kwamba ku-*stream line* kwa mashirika mbali mbali pia ni jambo moja linalofanyiwa kazi. Kwa hivyo mimi nadhani hilo litafika pahala litafanyiwa uamuzi, mapendekezo aliyotoa Mhe. Hamza ni sawa ni sahihi na ni mazuri na ni ya kimaendeleo kwa ajili ya kuleta ufanisi. Lakini nadhani tukisema kwamba tunaanza tu kwenye sheria hii haitokuwa vizuri sana tusubiri uamuzi ukifanywa kwa pamoja basi ufanywe kwa taasisi zote ambazo zitakuwa zina mazingira ya namna hii.

Mwisho ni lile ambalo alilizungumzia kidogo Mhe. Abdalla Juma kuhusiana na kifungu cha 53 yeye alipendekeza kwamba ili kuondoa mgongano wa sheria tusiseme tu kwamba sheria hii itakuwa na nguvu, lakini tuitaje ile migongano ya sheria. Kusema kweli haitowezekana kwa sababu migongano mengine inaweza ikaja kwa tafsiri tu sio kwa ilivyoandikwa haya maneno, lakini inawezekana ukitafsiri sheria hii na ukitafsiri sheria hii unapata kitu kama mgongano. Kwa hivyo ndio maana tukasema tuache itakapotokea kuna mgongano kwa sababu hii kwa kanuni mbili kwanza hii ni sheria ya udhibiti kwa hivyo zile zinazodhibitiwa basi lazima ziwe chini na hii iwe ndio iko juu.

Lakini pia kwa kanuni ya pili kwamba unapokuwa na sheria mbili zina mgongano basi sheria iliyokuja baadae ndio itakuwa na nguvu kuliko sheria iliyopita. Lakini kwa kuungana na lile alilolizungumza labda kuna maneno mimi ningependekeza mwisho wa kila kifungu cha 53 ni vizuri yale maneno tukayaondoa ambayo yanasema, labda naomba niyanukuu yale maneno yanayosema Mhe. Spika, hadi pale Waziri atakapoelekeza vyenginevyo. Nadhani maneno yale sheria hii ndio itakayotumika nadhani yanatosha na yale maneno hadi pale Waziri atakapoelekeza vyenginevyo nadhani ningependekeza sana kwamba ni vizuri tuyaondoe labda yameingia kwa bahati mbaya na si vizuri yakawepo katika ile sheria, lakini vyenginevyo kile kifungu kibaki kama kilivyo nadhani ni sahihi na madhumuni yake ni hayo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi mchango wangu ulikuwa ni wa jumla pamoja na yale masikitiko waliokuwa nayo Waheshimiwa Wajumbe lakini naomba sana tuuelewe mswada huu kwamba madhumuni yake ni hayo ni sehemu ya mchakato na si tukio kwamba hapa ndio tumemalizia na naomba sana wenzangu tuuunge mkono tuupitishe ili tuweze kutengeneza kile kitu cha muda mrefu ambacho kitawasaidia wananchi katika kupata ushindani, na kwa hivyo kupata huduma nzuri katika mambo haya muhimu katika maisha na katika uchumi wa nchi yetu. Mhe. Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

Mhe. Spika: Mhe. Mwanasheria Mkuu ninakushukuru na ninawashukuru pia Waheshimiwa Wajumbe kwa kushirikiana kwa shughuli ya mjadala wa mswada huu. Nimepata mchangiaji mmoja hivi punde ambapo na muda wenyewe kwa kweli haupo, nimuombe basi kama ana lolote basi ampelekee Mhe. Waziri kwa maandishi mchango wake. Hii inathibitisha yale maelezo niliyoyatoa kabla kwamba Mwanasheria Mkuu ndiye mchangiaji wetu wa mwisho.

(Saa 1:40 Usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 04/04/2013
Saa 3:00 asubuhi